Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 11 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB - MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2008/2009.

**MHE. LUCY F. OWENYA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 362

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ilitoa Tamko kwamba itajibu Hoja zote za Kamati Teule katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili. Ninaomba kuondoa swali langu Na. 362.

Na. 363

**Mpango wa Kurasimisha mali za wananchi Vijijini**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 moja ya ahadi zilizotolewa ilikuwa ni kuitaka Serikali ianze kurasimisha mali za wananchi na hasa vijijini ili taasisi za fedha ziweze kuwakopesha wananchi ambao watataka mikopo ya kuendesha shughuli zao:-

(a) Je, ni mikoa au wilaya zipi ambazo zimekwisha anza kazi ya kurasimisha mali hizo?

(b) Je, isingekuwa vyema kwa Serikali kuanza zoezi hilo katika Mkoa wa Rukwa ambao una wakulima wengi wanaotaka kuondokana na kilimo cha jembe la mkono?

(c) Je, ni nini faida ya mpango huo (MKURABITA) kama haitasaidia kuondoa matatizo ya wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali, naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Lengo la MKURABITA ni kuwafanya wananchi wenye ardhi na nyumba ambazo hadi sasa hazitambuliwi kisheria kuweza kupata mikopo kwa kuweka ardhi na nyumba hizo dhamana na kuwawezesha kukopesheka na hivyo kuingia katika mchakato wa uchumi rasmi. Mpango huu unatekelezwa katika awamu nne zifuatazo:-

Awamu ya kwanza ilianza kutekelezwa mwezi Novemba, 2004 na ilikamilika mwezi Septemba, 2005. Awamu hii ilihusu kufanya tathmini ya sekta isiyo rasmi au sekta isiyokidhi matakwa ya sheria. Tathmini iliyofanywa ilibaini kuwa sekta isiyo rasmi ina ukubwa wa 89% ya rasilimali inayohusu ardhi na majengo na 98% ya biashara. Thamani ya rasilimali hiyo inakadiriwa kuwa dola za Kimarekani bilioni 29.3 ambao huu ni mtaji mfu.

Awamu ya pili ilianza kutekelezwa mwezi Januari, 2006 na ilikamilika mwezi Machi, 2007. Kazi zilizofanyika katika awamu hii ni kufanya maboresho ya Sheria, mifumo ya kitaasisi na Kanuni zinazofaa katika kumiliki rasilimali na uendeshaji wa biashara kwa kuondoa vikwazo vilivyopo vinavyokwamisha urasimishaji kwa haraka na kwa gharama nafuu.

Awamu ya tatu inahusu utekelezaji wa maboresho yaliyoandaliwa katika awamu ya pili na inajumuisha urasimishaji wa rasilimali na biashara vijijijni na mijini. Wilaya zifuatazo ambazo ni Bagamoyo, Handeni, Kasulu na Kinondoni walimiliki rasilimali, wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kurasimisha mali zao.

Utekelezaji wa awamu hii umeanza mwaka huu wa fedha 2008/2009 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi.

Awamu ya nne inahusu kuwawezesha wamiliki mali na biashara zilizorasimishwa kuzitumia kupata mitaji na fursa nyingine katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo juu utekelezaji wa mpango wa kurasimishaji rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania uko katika awamu ya tatu inayohusu urasimishaji wa rasilimali na biashara vijijini na mijini ambao Utaanza mwaka huu wa fedha 2008/2009 na utatekelezwa kwa miaka kumi. Kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 urasimishaji wa ardhi vijijini utafanyika katika vijiji 60 vilivyo katika wilaya kumi (10) ambazo ni:-

Mbozi, Njombe, Makete, Musoma Vijijini, Serengeti, Nachingwea, Mvomero, Mpwapwa, Wete – Pemba na Rufiji, Mkoa wa Rukwa pamoja na mikoa mingine itahusishwa katika awamu hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utekelezaji wa MKURABITA katika mikoa yote unajumuisha; mabadiliko katika sheria kadhaa za ardhi na biashara, utekelezaji wa shughuli za urasimishaji ardhi na biashara, utekelezaji wa shughuli za urasimishaji ardhi katika ngazi ya vijiji, wilaya na taifa. Kwa hiyo, mkoa wa Rukwa umo katika mchakato huo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya tafiti na uzoefu uliopatikana kutoka mataifa mengine yaliyofanikiwa kutokana na mipango inayofanana na MKURABITA yanaonyesha kuwa kuna faida kubwa zitakazopatikana kwa kutekeleza mpango huu ikiwa ni pamoja na:-

Kuwawezesha wamiliki wa rasilimali kuzitumia kujiongezea mitaji na maslahi mengine ya kiuchumi yanayopatikana katika soko rasmi.

Kuimarisha utawala bora kwa kutumia mfumo wa masijala yanayowaunganisha raia wote na anwani zao, miliki zao za rasilimali na mwenendo wa matumizi ya rasilimali hizo katika soko.

Sekta rasmi katika uchumi wa nchi itapanuka na hivyo kuongeza pato la mtu binafsi, kaya, vikundi, kampuni na taifa kwa ujumla.

Umoja wa kitaifa utaimarika kwa kuunganisha mifumo miwili ya sasa katika kumiliki mali na kufanya biashara, yaani mfumo rasmi unaowahusisha wachache na usio rasmi unaowahusu wananchi wengi wa vijijini na mijini.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mpango huu unaonekana unasuasua sana, na kwa kuwa

mpaka sasa inaonekana hati zinazopatikana kwa wanavijiji katika maeneo mbalimbali hazitambuliki na mabenki yetu.

Je, Waziri anakubaliana nami ya kwamba bila Serikali kusimamia ahadi ambazo tumezitoa katika Ilani yetu ya Uchaguzi miaka mitatu ifuatayo itashindwa kutekeleza?

La pili. Ni misingi ipi Mheshimiwa Waziri atanisaidia inayotumika katika kuamua tuanze na Mikoa ipi na mikoa ipi iwe ya mwisho? Tungependa kugezo vilivyotumika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango huu kusuasua na kwamba utekelezaji wake katika kipindi cha miaka miwili ijayo utakuwa haujaisha. Ni kwamba mpango wenyewe ulikuwa ni mpango ambao ulikuwa uende awamu kwa awamu.

Kama nilivyoeleza katika jibu langu ni kwamba kwanza ilibidi kutathmini na kujua ukubwa wa tatizo na halafu imeenda katika kuangalia sheria ambazo zinakwamisha urasimishaji wa mali hizo. Kwa sasa hivi Sheria hizo zimetambuliwa na vijiji na miji tumeona sheria zote mbili za ardhi sehemu ambazo zinahitaji marekebisho na ningependa kumfahamisha kwamba mpango huu unaenda siyo mpango ambao unafanywa na sekta moja ni mpango ambao utahusu sekta mbalimbali. Tuseme upande wa biashara, Wizara ya Ardhi, *Local Government* wote sheria hizo zitakapobadilishwa wataanza kuzitumia sheria hizo.

Kwa sasa tunajitahidi kuweza kupima, kuhamasisha Wizara ya Ardhi kutumia *Local Government* kuhakikisha kwamba mashamba mengi vijijini yanapimwa na upimaji wenyewe utafanywa kwa pamoja, wote wakiwepo, kijiji kimoja, mashamba yote yapimwe kwa pamoja na sio moja moja. Hii yote katika kuharakisha huu mpango. Swali lake la pili ambalo anazungumzia ni misingi gani ambayo inatumika. Misingi ambayo inatumika ni ile ambayo wataalam wanakaa na kuangalia jinsi gani watashughulikia hii mipango. Kama ilivyo kwa mipango ni lazima uanzie mahali pamoja, uishie mahali pengine.

Kwa hiyo, ni mipango kama ilivyo katika mipango mingine. Kwa hiyo, hakuna utaratibu maalum ambao tunaweza tukasema unatumika kwa kusema ni hivi au hivi. Lakini kila jambo lazima liende kwa mipango ili tuweze kufanya vizuri. Na kwa sasa hivi ile tuliyoanza ilikuwa ni mipango ya majaribio.

Na. 364

**Mambo ya Muungano**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, nyongeza ya kwanza Bandari na Leseni za Viwanda ni miongoni mwa mambo 22 yahusuyo Muungano:-

(a) Je, ni mambo yapi yaliyo ya Muungano kwenye eneo la Bandari za Tanzania?

(b) Je, ni viwanda vingapi na vipi vilivyopewa leseni Tanzania Visiwani na kwa utaratibu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS ( MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mambo yaliyo ya Muungano kwenye eneo la Bandari ni kama yafuatayo:-

1. Bandari *(Habour).*

2. Kupakia na kushusha mizigo Bandarini.

3. Mamlaka ya Kusimamia na Kudhibiti Vyombo vya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA).*

4. Biashara ya Meli *(Merchant Shipping).*

Hata hivyo mambo yote haya hayajawahi kuendeshwa kimuungano tokea Muungano huu uasisiwe miaka 44 iliyopita.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutoa leseni za viwanda ni la Muungano na limekuwa likishughulikiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya utoaji leseni na usajili wa viwanda. *(The National Industries Licensing and Registration, Act No. 10 of 1967)* kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 13 ya mwaka 1982. Kwa utaratibu huu jumla ya viwanda ishirini (20 vya Tanzania Zanzibar vimepewa leseni.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mambo manne aliyoyataja Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hayajafanyiwa kazi kwa muda wa miaka 44 iliyopita. Pia ni sababu zipi zilizosababisha mambo haya yasifanyiwe kazi?

Swali la pili, kwa kuwa swali langu la msingi la (b) nilitaka kujua ni viwanda vipi, ningependa sasa anitajie Mheshimiwa Waziri ni viwanda vipi ambavyo vimepewa leseni? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siwezi kujua sababu zipi za msingi kwa nini jambo hili halikuwa katika jambo la Muungano.

Lakini inawezekana kwamba jambo la msingi kwamba Serikali ya Zanzibar kwa miaka mingi sana imekuwa bandari, ndiyo chimbuko muhimu la mapato yake, ikitegemea pia karafuu, mbata na pilipili hoho.

Kwa hiyo, nafikiri jambo kubwa ni hilo, lakini mpaka sasa hivi sina sababu za msingi, kwa sababu mpaka tupate maoni ya Serikali zote mbili na kwa sababu Serikali zote mbili zimekaa kimya maana yake wameridhika na hali hiyo.

Swali la pili Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuhusu viwanda. Viwanda ambavyo vimepewa leseni ni kama ifuatavyo:-

Viwanda ambavyo vimekufa havifanyi kazi ni cha kwanza kilikuwa ni kiwanda cha Sigara, Tabia Njema. Cha pili, kiwanda cha *COTEX* Zanzibar, cha tatu kiwanda cha Mahonda, *Sugar Factory*, cha nne *State Leather and Shoe Company* cha tano, kiwanda cha *Audio and Video Cassette* cha sita kiwanda cha *Chaise Super* cha saba kiwanda cha *Tissue Paper.*

Viwanda vinafanya kazi mpaka sasa ambavyo vipo ni kiwanda cha Soda, kiwanda cha *Afro Come Limited* Viwanda vya POK. Kiwanda cha *Zainab Bottlers* kiwanda cha *Changu Soap* kiwanda cha *Drop of Zanzibar* na Kiwanda cha *Bhakresa Diary Milk.*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anakiri kabisa kwamba mambo haya hayajawahi kufanyiwa kazi hata siku moja.

Sasa, kwa nini Serikali isiamue kuyafuta kuliko kubaki kwenye vitabu yakaonekana ni ya Muungano? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye na wazo la Bwana Zambi, kwamba yanaweza yakafutwa.

Lakini mpaka wenyewe waseme yafutwe. Huwezi kufuta mwenyewe tu. Kwa hivyo kama jambo hili kama lifutwe, basi Kamati ipo ya Kero itakaa kitako na kuyafuta tu basi.

Na. 365

**Kata ya Ngulla kupewa walimu wa Sayansi**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Ngulla, Wilayani Kwimba, wamechangia ujenzi wa shule ya Sekondari na ujenzi wa maabara nzuri:-

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha wa sayansi katika shule hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wanachangia ujenzi wa shule za sekondari na ujenzi wa maabara yakiwemo ya Kata ya Ngulla Wilayani Kwimba. Aidha, ujenzi huo unaambatana na mahitaji makubwa ya walimu na hasa walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Serikali imeajiri jumla ya walimu 3,861, kati ya hawa 3,460 ni wa kiwango cha stashahada na 401 ni wa kiwango cha shahada. Katika kipindi hicho walimu wa sekondari waliopangwa mkoa wa Mwanza ni 219 kati ya walimu hawa wa sayansi ni 57 na sanaa ni 162.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule ya sekondari ya Ngulla imepangiwa mwalimu 1 wa sayansi na imeongezewa walimu 4 wa mazoezi kati ya hawa 2 ni wa sayansi na 2 ni wa sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Julai, 2008 jumla ya walimu 12,692 wamehitimu katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu hapa nchini na zoezi la kuwapangia vituo vya kazi linaendelea.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika swali langu la msingi niliomba walimu wa kutosha katika Kata hii ya Ngulla. Bahati mbaya sana nimepelekewa mwalimu mmoja. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia kwamba sasa shule hii ya Kata ya Ngulla mlifikiria vipi kutokana na kiasi walichoomba walimu mkapeleka mwalimu mmoja. Huyo mmoja amekidhi mahitaji yao?

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa wananchi wamepata uelewa mzuri sana wa kuchangia katika kujenga shule zao, kwa mfano wa Kata ya Ngulla wamejenga na maabara nzuri. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kudumu wa kuhakikisha sasa tunapeleka walimu sambamba na vifaa vya maabara katika maeneo haya yanayojengwa na wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na tunakiri kwamba walimu hawatoshi na kama nilivyoeleza walimu waliopangwa mkoa wa Mwanza ni wachache na kwa hali hiyo ilibidi shule ya Ngulla ipatiwe mwalimu mmoja kutokana na idadi ya shule zilizoko mkoa wa Mwanza na kama tulivyosema tena tunazidi kuandaa walimu wa sayansi, ili kuendana na maabara zilizojengwa na hapa naomba nimpongeze Mheshimiwa Ndassa ambaye alichangia maabara ya shule ya Ngulla shilingi laki tano (500,000) na tunawahimiza wote muendelee kufanya hivyo.

Kwa kweli tuendelee kuwa na uvumilifu walimu watapatikana. Kuna jitihada kubwa sana za kuendeleza walimu wa sayansi pamoja na kuandaa walimu tarajali.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwanza na mimi nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana.

Lakini naomba niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na kuzipatia shule hizi walimu wa sayansi, lakini bado kunahitajika vifaa vya kutosha katika shule hizo pamoja na wataalam wa maabara.

Je, Serikali ina mpango gani kutoa wataalam wa kutosha kwenye shule hasa zile ambazo zina maabara kama hiyo iliyotajwa pamoja na Ngulla na Nyamiramba katika Jimbo la Kwimba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ningefikiri Mheshimiwa Mbunge angevumilia swali la pili linalokuja linahusu wataalam wa maabara ambao tunawaandaa lakini najua hawatoshi.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo majibu yake asilikize kwenye swali linalofuata. Haya.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kilio kikubwa cha walimu ni kutolipwa baadhi mishahara na wengine marupurupu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuacha kuendelea kukopa nguvu za walimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimaro lakini swali hilo ni jipya. Mwenzako anasema walimu hawatoshi. Wewe unasema hawatoshi kwa sababu ya mishahara? Au ndivyo hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nakubaliana na wewe kwamba hili ni swali jipya. Lakini hata hivyo kama tulivyozungumza hapa mara

nyingi, walimu wetu tunajitahidi kuwalipa mishahara mapema hasa wanaporipoti na taarifa zile zinapokuja Wizarani, tunajitahidi kulipa.

Lakini taarifa zisipofika mapema hapo ndipo matatizo yanapoanzia. Kwa hiyo, tunawaomba Wakuu wa Shule wawe wanaleta taarifa hizi mapema na kwa madeni sasa hivi tunajitahidi kuwalipa walimu wetu kama ipasavyo.

Na. 366

**Kuongeza Wakutubi na Mafundi wa Maabara Kwenye Taasisi Zote za Elimu**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA a**liuliza:-

Kwa kuwa, utoaji wa elimu kwenye ngazi zote za elimu huhitimishwa kwa kuwepo na Maktaba za Elimu zilizo na zana na vifaa vyote vinavyohitajika na wataalamu wa kutosha shuleni na vyuoni:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuongeza ajira ya wakutubi na mafundi wa maabara kwenye Taasisi zote za elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mwalimu na Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa maelezo mafupi kwamba kuna uhaba mkubwa wa wataalamu wa kada ya ukutubi na wataalamu wa maabara *(Laboratory Technicians)* hapa nchini kutokana na vyuo vinavyotoa mafunzo ya taaluma hizi kuwa vichache. Vyuo vinavyotoa taaluma hizo ni Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka *(School of Library, Archives and Documentation Studies (LADS)* kilichopo Bagamoyo, ambacho hutoa mafunzo ya ngazi ya cheti na stashahada.

Kwa ngazi ya shahada, mafunzo hayo hutolewa na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Chuo Kikuu cha Tumaini. Kwa upande wa wataalamu wa maabara *(Laboratory Technicians)* mafunzo yake hutolewa katika chuo cha Ufundi Dar-es-Salaam *(Dar-es-Salaam Institute of Technology).* Aidha, wahitimu katika vyuo hivyo wanaajiriwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Asasi nyinginezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa pamoja na mambo mengine, ubora wa elimu hutegemea kuwepo kwa maktaba na maabara zinazojitosheleza kwa vifaa na wataalamu wake. Kwa kuzingatia umuhimu huo Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 itaendeleza ujenzi wa kuimarisha Chuo cha Ukutubi na uhifadhi nyaraka Bagamoyo, ikiwa ni pamoja na kutoa Mafunzo ya cheti, stashahada na mafunzo ya muda mfupi.

Aidha, Wizara itaendelea kukabiliana na changamoto ya upungufu wa maabara na wataalamu wa maabara *(Laboratory Technicians)* kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kupitia chuo chake cha ufundi cha Dar-es-Salaam *(DIT).*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA**: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi. Kwa vile Serikali imekiri kabisa kwamba hawa wataalam wa aina hii ni wachache. Ni kwa nini tulipoandaa mpango wa kupanua elimu ya sekondari hatukutia kipengele hiki kwenye mradi wetu kwamba na wataalam hawa waongezeke? La kwanza.

Swali la pili. Kutokana na uchache wao huo ambao utaendelea muda mrefu na Serikali imekiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani sasa wa dharura zaidi wa kuwaandaa wataalam hawa kwa sababu maabara zetu zitabaki tu kama ni majengo, mwalimu mmoja na wa kumsaidia kufundisha sayansi hatakuwepo na hivyo kukosa wataalam wa sayansi kwa muda mrefu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango uliopo wa dharura wa kuongeza wataalam hawa na kwamba hatukuweka katika mpango wetu wa elimu ndiyo huo nilioutaja kwamba tunategemea hivyo vyuo ambavyo nimevitaja, Chuo Kikuu cha Tumaini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pamoja na *DIT* kutuandalia hawa wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshazungumza na *DIT* kwamba wajaribu kuwaandaa hawa wataalam kadri iwezekanavyo kulingana na Bajeti iliyopo na tutashirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kufanya hivyo.

Kwa hiyo naamini kabisa kwamba tunaweza kutosheleza kwa kiasi kadri tunavyoendelea. Lakini hata hivyo ningeomba Wakuu wa Shule waweze kuwatumia vizuri walimu waliopo wa Sayansi pamoja na vijana wengine ambao wanaweza wakawa-*train* kwa haraka ili waweze kukidhi mahitaji ya maabara na ufundishaji wa Sayansi katika mashule yetu hapa nchini, wakati tunasubiri hawa wataalam kuandaliwa. *(Makofi)*

Na. 367

**Uanzishwaji wa *SACCOS* za Wakulima**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa taifa na kwamba moja ya mikakati ya uhamasishaji wa sekta ya kilimo ni kuhimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya kuweka na kukopa – *(SACCOS)*:-

(a) Je, ni *SACCOS* ngapi zimeshaanzishwa kwa ushawishi wa Serikali?

(b) Je, maendeleo ya *SACCOS* hizo yako vipi na Serikali inatoa msaada gani na imepokea malalamiko mangapi tangu mpangohuo ulipoanza?

(c) Je, ni *SACCOS* ngapi zimeanzishwa kwenye Jimbo la Iramba Mashariki na zimepewa mikopo inayofikia kiasi gani?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hufanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuanzisha na kuendeleza Vyama vy Ushirika Nchini. Kufuatia wito wa Serikali wa kuwahimiza wananchi kuanzisha *SACCOS* ili waweze kupata huduma za fedha ikiwemo mikopo inayotolewa chini ya mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi idadi ya *SACCOS* nchini imeongezeka kutoka 2,028 mwezi Mei 2006 hadi 4,445 mwezi Mei 2008. Kati ya *SACCOS* zilizoanzishwa *SACCOS* 2,629 ni za vijijini na 1,816 ni za Mijini.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya *SACCOS* zilizoanzishwa bado ni changa, zina idadi ndogo ya wanachama, mitaji midogo na viongozi ambao hawana ujuzi wa kutosha katika masuala ya uendeshaji wa *SACCOS*. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine inasaidia maendeleo ya *SACCOS* hizo kwa njia mbalimbali zikiwemo hizi zifuatazo:-

(i) Kuhamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga na *SACCOS* na kushiriki kuweka akiba, hisa na amana ili kuimarisha mitaji.

(ii) Kutoa elimu na mafunzo kwa wanachama, viongozi na watendaji, kutoa miongozo ya uendeshaji na kufanya ukaguzi na usimamizi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika nchini. Hata hivyo mahitaji ya Vyama hivi ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali wa kuvisaidia vyama vyote mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahimiza wananchi kuunda *SACCOS* zenye nguvu kubwa za kiuchumi ili ziweze kumudu kuajiri watendaji wenye sifa za kutosha kuziendesha kama inavyostahili kwa manufaa ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malalamiko yanapotolea kuhusiana na matatizo ya uendeshaji hushughulikiwa na Maafisa Ushirika wa Wilaya pamoja na Warajis Wasaidizi wa Mikoa. Hadi sasa yametokea malalamiko machache ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, *SACCOS* zipatazo nane zimeanzishwa katika Jimbo la Iramba Mashariki zenye jumla ya wanachama wapatao 1,284 wenye hisa za shilingi 14,007,300 na akiba shilingi 41,727,962 *SACCOS* hizo zimetoa mikopo ya shilingi 58,213,500 kwa wanachama wake kwa kutumia mitaji ya ndani. Aidha mikopo ya shilingi milioni 25 imetolewa kutoka asasi ya *Pride Tanzania.*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Killimbah, anatoka Jimbo la Iramba Magharibi na kwa kuwa Mhweshimiwa Waziri, amezitaja *SACCOS* za Iramba Mashariki. Je, atazitaja za Iramba Magharibi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *SACCOS* zote Iramba zimeanzishwa na zinakwenda vizuri ila Maafisa Ushirika hawatoshi kwenda kuhimiza wananchi wachangie zaidi. Na kwa kuwa sasahivi tunaloomba ni msaada kutoka Serikali tuweze kupata mikopo ya kuwakopesha wananchi wetu. Waziri, anasemaje juu ya hayo?

**NAIBU SPIKA:** Maswali hayo yako matatu lakini mawili tu yanapaswa kujibiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kuzitaja *SACCOS* hizi za Jimbo lake zinahitaji *data.* Kwa hiyo, baada ya kutoka kipindi cha Maswali na Majibu nitamwandalia jibu lake nitamwasilishia kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili katika suala lake la kutotosha kwa Maafisa Ushirika, tutafuatilia tujue kwamba Maafisa Ushirika wako wangapi na ni wangapi tuweze kuangalia uwezekano wa kuongeza ili waweze kufanya kazi hii ya uhamasishaji wa wananchi kujiunga na *SACCOS.*

Lakini la tatu ninahimiza kwamba vyama hivi vya *SACCOS* katika Jimbo lake na jimbo la Mheshimiwa Killimbah, wanachama tunawahamasisha waweze kuwa wengi ili mitaji iwe mingi na amana ziwe nyingi kusudi waweze kukopa kwa kiasi kikubwa. Lakini pia waweze kuajiri watendaji wenye ujuzi wa elimu ya Ushirika na wanaoelewa biashara ili waweze kuendesha *SACCOS* zao vizuri.

Bila kuwa na wanachama wa kutosha, bila wao Waheshimiwa Wabunge, kuhamasisha kuwa na wanachama wa kutosha ni dhahiri kwamba hata mikopo kwasababu *CRDB* walikuwa wameshaonyesha nia ya kuwakopesha lakini wakaona kwamba mitaji yao ni midogo na hawana watendaji.

Kwa hiyo, wakishakuwa na mitaji mikubwa, wakishakuwa na wanachama wengi, *CRDB* iko tayari kabisa kuwakopesha *SACCOS* hizi za Iramba. *(Makofi).*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, ustawi wa *SACCOS* hizi pamoja na utendaji wake unategemea sana elimu ya Ushirika.

Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa Chuo cha Ushirika Kizumbi, kilichoko Shinyanga Mjini, ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na *Studies* za Biashara, kinatumika ipasavyo ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na viongozi na watendaji walio imara kwa ajili ya ustawi wa *SACCOS* nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Charles Mlingwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kabisa kwamba Chuo hiki mpaka sasa hivi kinatoa Maafisa Ushirika na tutakachoendelea kukifanya ni kukiimarisha na kuwapeleka wanafunzi wengi zaidi ili kiweze kutoa wanaushirika wanaotosha.

Lakini katika mikoa ama katika kanda mbalimbali, tutakuwa na vituo mbalimbali ambavyo vitakuwa vinatoa elimu kwa wana Ushirika kusudi *SACCOS* zetu na vyama vya Ushirika viweze kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba mimi mwenyewe niliongea na Mkuu wa Chuo cha Ushirkka Moshi, wiki mbili zilizopita, kile Chuo cha Ushirika na Biashara Moshi, alinidhihirishia kabisa kwamba chuo hiki cha Kizumbi, kinatakiwa kiongezewe uwezo kwa maana ya wafanyakazi pamoja na majengo kukarabatiwa ili tuweze kupata uwezekano wa kuingiza wanafunzi wengi zaidi kukidhi mahitaji ya Ushirika ikiwa ni pamoja na vile vituo vya Kanda.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa swali la msingi la Mheshimiwa Juma Killimbah, ambaye ametoka Jimbo la Iramba Magharibi, ni wazi kwamba majibu ya msingi yalikuwa yajibiwe kuhusu Iramba Magharibi.

Je, Mheshimiwa Waziri, anakosaje *data* za Jimbo la Iramba Magharibi wakati wananchi wa Iramba Magharibi sasa hivi wanasikiliza hili swali?

**NAIBU SPIKA:** Hapana, nilivyoelewa mimi, aliyeuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Killimbah, anatoka Jimbo lingine lakini katika Wilaya ile ile.

Kwa hiyo, aliyojibu Waziri ni yale ya Mbunge aliyeuliza, lile lilikuwa ni swali la nyongeza. Ndivyo nilivoelewa mimi na ndio maana akasema *data.* Tunaendelea, Wizara ya fedha na uchumi. Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, kwa niaba yake Mheshimiwa *Professor* Idris Mtulia.

Na. 368

**Kushuka Kwa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA K.n.y. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha fedha yetu kushuka thamani wakati uchumi unakuwa?

(b) Je, hali ya kushuka kwa thamani ya fedha yetu ikoje ikilinganishwa na nchi zingine za *SADC?*

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, wakati uchumi wetu ulikuwa kwa asilimia 6.7 mwaka 2006 na asilimia 7.1 mwaka 2007 thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani ilishuka thamani kwa asilimia 2.2. Hali hii ilitokana hasa na athari za ukame ambapo nchi iliathirika kwa namna mbili. Kwanza, uzalishaji wa mazao yote ya kilimo hasa mazao ya chakula ulipungua sana na hivyo kulazimika kununua chakula kutoka nje.

Pili, uzalishaji wa umeme ambao unategemea mito na mabwawa nao ulipungua sana na kulazimika kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta kutoka nchi za nje, wakati bei za mafuta katika soko la dunia zilikuwa zimeongezeka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii fedha nyingi tulizotumia kununua mafuta na chakula zilisababisha ongezeko la mahitaji ya dola za kimarekani. Kwa kuwa mauzo yetu nchi za nje yaliongezeka kwa asilimia 3.8 tu ukilinganisha na ongezeko la manunuzi nje ya nchi la asilimia 25.2 tulipata nakisi kubwa sana katika urari wa biashara. Hali hii ilisababisha thamani ya shilingi kushuka kwasababu mahitaji yetu ya fedha za kigeni yalikuwa ni makubwa sana kuliko mapato yetu ya fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miezi ya hivi karibuni thamani ya shilingi imekuwa ikiimarika. Kwa mfano thamani ya shilingi ikilinganishwa na dola ya kimarekani iliimarika kutoka wastani wa shilingi 1,290.52 mwezi Januari, 2007 hadi kufikia uwiano wa dola moja kwa wastani wa shilingi 1,179.60 kwa mwezi Juni, 2008.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizosababisha kushuka au kupanda kwa tahamani ya fedha katikia nchi za *SADC* ni zilezile nilizozitaja awali ingawa kila nchi huathirika kwa kiwango tofauti. Hata hivyo, sababu mojawapo kubwa inayofanana katika nchi zote hizi imekuwa ni kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na Benki Kuu *(BOT)* mwaka 2006, ulionesha kuwa kati ya mwezi Machi 2005 na Septemba 2006, sarafu za nchi zote za *SADC* zilishuka thamani japo kwa viwango tofauti. Wakati shilingi ya Tanzania ilishuka thamani kwa asilimia 15.3 ikilinganishwa na dola moja ya Kimarekani. Sarafu ya Msumbiji iliporomoka kwa kwa asilimia 54.0 na pula ya Botswana kwa silimia 36. Kwacha ya Zambia ilishuka kwa asilimia 33.0 na Randi ya Afrika Kusini kwa asilimia 22.0.

Aidha, sarafu ambazo hazikupata msukosuko sana ni dola ya Namibia 15%, na sarafu ya Angola 7.0%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utafiti huo, ni wazi kwamba sarafu ya Tanzania ilishuka thamani kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na sarafu za nchi nyingine za *SADC*. Bila sera imara za fedha, *monetary and fiscal Policies*, uwiano wa shilingi na dola ya kimarekani usingekuwa kama ulivyo sasa.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini sababu zilizotajwa ndio zilizopunguza thamani ya shilingi, ukitazama Afrika Mashariki, Kenya ina *natural resources* chache kuliko Tanzania. Au unadhani ni mikataba mibovu ya madini hela zetu zimekwenda nje ndio maana fedha yetu imeshuka thamani? La kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Upandaji wa shilingi kwa miezi michache sio kwasababu shilingi imepata thamani kubwa ni kwasababu dola ya Marekani imeshuka. Kwa hiyo, kwa kuwa sisi hatukushuka, tumebaki pale ndio maana inaonekana imepanda thamani. Je, unasemaje katika hili?

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ya Kenya ikilinganishwa na fedha ya Tanzania. Ni kweli fedha ya Kenya inaonekana kwamba ina nguvu kuliko ya kwetu, lakini

tukumbuke kwamba nguvu ya fedha ya nchi yoyote inategemeana na uimara wa uchumi wake. Na ni lazima tukubali kwamba wenzetu Kenya, uchumi wao hasa kwenye viwanda una nguvu zaidi kuliko uchumi wetu hapa. Hiyo ndiyo changamoto moja ambayo tunayo, uzalishaji kwenye viwanda na vilevile uzalishaji kwenye Kilimo. Lakini pia sio lazima kwamba kwasababu shilingi ya Kenya 67 ni sawasawa na dola moja na shilingi 1,179 ukilinganisha na sarafu ya Marekani ni hiyohiyo basi moja ni dhaifu kuliko nyingine, hapana hiyo siyo mantiki ya ulinganishi.

Mheshimiwa naibu Spika, lakini la pili kuhusu thamani ya sasa ya Tanzania, si kweli kwamba sarafu ya Tanzania sasa ina nguvu kuliko ilivyokuwa kwasababu dola ya Marekani imeshuka thamani. Ni kweli dola ya Marekani imeshuka thamani ingawaje sasa imeanza kuimarika. Ilishuka thamani kwasababu uchumi wao ulitetereka hasa sekta ya nyumba hasa katika soko la mitaji lakini katika kuimarika kwa shilingi ya Tanzania, ilikuwa uimarishaji wa makusudi uliotokana na usimamizi mzuri wa sera za fedha za nchi yetu unaosimamiwa na Benki Kuu. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza Gavana na watendaji wa Benki Kuu na Benki Kuu yetu kwa kusimamia vizuri thamani ya shilingi yetu. *(Makofi)*

Na. 369

**Mpango Kabambe wa Ujenzi wa Reli Nchini**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE K.n.y. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania inategemea kilimo na kwamba reli ndiyo njia bora na rahisi kusafirisha mazao kati ya mkoa kwa mkoa na kusafirisha mazao nje ya nchi:-

Je, Serikali itawasilisha lini mpango kabambe wa ujenzi wa reli nchini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imetayarisha mpango wa miaka 10 ya Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi ama *Transport Sector Investiment Programme (TSIP),* ambao pamoja na mambo mengine unajumuisha reli.

Mpango huu umegawanywa katika awamu mbili: Awamu ya kwanza ya mwaka 2007/2008 – 2011/2012 na awamu ya pili ya mwaka 2012/2013 – 2016/2017. Kwa upande wa reli, mpango huu utahusisha mambo yafuatayo:-

(i) Mtandao wa reli uliopo sasa na huduma zinatarajiwa kuimarishwa.

(ii) Kuifanyia upembuzi yakinifu reli itakayounganisha Mtwara – Lindi – Mchuchuma/Liganga.

(iii) Kuendelea kuifanyia upembuzi yakinifu, Reli ya isaka – Kigali na Bujumbura, kuandaa michoro, *detailed designs,* na kuanza ujenzi.

(iv) Kuendelea kutafutia fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa reli ya Arusha – Musoma chini ya mpango wa *East African Community*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya dola za kimarekani 946.46 milioni zinakisiwa na kuhitajika ili kuwekeza katika miundombinu ya reli katika awamu ya kwanza ya *TSIP*. Serikali kwa kushirikiana na washirika wa kimaendeleo wanajadiliana namna ya kutekeleza mpango huu wa *TSIP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, waliagiza kwa pamoja uandaliwe mpango kabambe wa Maendeleo wa *EAC Railway Master Plan.*

Mtaalamu Mshauri, anaendelea kuandaa mpango huo ili hatimaye uidhinishwe katika ngazi zote husika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mpango huo kabambe wa reli wanchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki utawezesha nchi husika ikiwemo Tanzania kuwa na mtandao wa reli unaounganisha nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa ratiba ya Mtaalamu Mshauri, anyendaa mpango huo inatarajiwa kwamba rasimu yake itawasilishwa kwa serikali za nchi husika mwishoni mwa Mwezi huu Agosti 2008, ili kupata maoni ya nchi hizo.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Mpanda inalima sana tumbaku na usafiri wanaoutegemea ni reli. Na sasahivi mabehewa hayatoshi kabisa mpaka inabidi magari yatumike kuchukua tumbaku Wilaya ya Mpanda kupeleka Morogoro. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza mabehewa ili wananchi wa Wilaya ya Mpanda waweze kusafirisha tumbaku yao salama.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa naibu Spika, ningependa kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Anna Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia shirika la Reli *TRL*, sasa hivi ina mpango wa kuboresha miundombinu ya reli kwa reli nzima ya kati ikiwemo eneo hili la kipande kile kinachoenda Mpanda. Tunategemea ndani ya mwezi huu wa Agosti, 2008, tutapokea mabehewa 23 ambayo yataboresha zaidi usafiri wa reli. Lakini pia tuna mpango wa kuongeza injini zenye uwezo mkubwa zaidi ili kufungua karibu eneo lote na njia zote zinazohusiana na usafiri katika reli ya kati.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Njia ya reli ni njia ambayo ni muhimu kwa nchi kama Tanzania kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta. Je, kabla ya kumaliza programu au ripoti ambayo inaandaliwa Ndugu Waziri,

haoni umuhimu wa kufikiria reli ya Mlimba – Liganga – Tunduma – Kasanga na Mpanda – Kalema? Ahsante. *(Makofi).*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Makweta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango huo na sasa hivi tuko katika majadiliano na nchi au wahisani wa kimaendeleo kutejkeleza hayo ambayo Mheshimiwa Makwetta ameyazungumza. Na sasahivi nchi ambayo tuna mawasiliano nayo ya karibu ni Serikali ya China, ili kuweza kufungua machimbo yale ya Liganga na Mchuchuma. Mali zile ziweze kutufaidisha Watanzania. Kwa hivyo tuko katika mpango huo wa kujenga reli katika maeneo hayo, lakini tuko katika hatua za awali za maongezi na washirika wetu.

Na. 370

**Usafiri – Mwambao wa Ziwa Nyasa**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA K.n.y. MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi waishio kando kando ya Ziwa Nyasa Wilaya za Kyela, Ludewa na Mbinga wanategemea sana usafiri pekee wa meli na kwa kuwa, meli zilizopo zimechakaa sana.

(a) Je, ni lini Serikali itatafuta mwekezaji atakayenunua meli mpya zitakazowaokoa wananchi wa Wilaya hizo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati sasa wa kujenga na kuboresha miundombinu muhimu katika Bandari zote za Ziwa Nyasa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu kifasaha swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuhamasisha wawekezaji kwenye Ziwa Nyasa, ingawa juhudi hizo bado hazijazaa matunda. Hata hivyo, jukumu la kuwapatia wananchi usafiri salama Ziwani utaendea kuzingatiwa kwa kutumia meli zinazomilikiwa na Kampuni ya Huduma za Meli, *MSCL*, ambayo inamiliki meli mbili za kubeba za kubeba abiria na mizigo, nazo ni *MV Iringa* na *MV Songea.*

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha miundombinu ya kibandari katika Ziwa Nyasa ambayo baadhi imechakaa au haipo

kabisa. Mwaka huu wa fedha 2008/2009 Serikali itaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya Gati ya *Mbamba Bay* ambao unategemewa kukamilika mwezi Agosti, 2008.

Upimaji wa kina cha maji kwenye magati ya Manda, Liuli, Kiwira na Itungi unaendelea ikiwa ni matayarisho ya kuboresha miundombinu hiyo mara fedha zitakapopatikana. Utafiti wa kuboresha miundombinu hiyo unafanywa kwa udhamini wa Benki ya Dunia. Aidha, vifaa vya mawasiliano vimewekwa katika vituo vya *Mbamba Bay,* Itungi na Liuli ili kuboresha mawasiliano ziwani.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa sasa kuna uhusiano mzuri kati ya Serikali ya Tanzania na serikali ya Malawi, na kwa kuwa wale wenzetu wana meli nyingi za usafirishaji wa mizigo na usafirishaji wa abiria, Serikali haioni ni kwanini sasa tusiongee nao ili waweze kutusaidia kusafirisha mizigo yetu na kusafirisha abiria wetu kama ilivyokuwa zamani?

Mheshimiwa naibu Spika, swali la pili. Ni kweli kwamba kuna meli mbili zimebaki katika ziwa lile na si meli ni boti mbili kubwa, *MV Iringa* na *MV Songea.* Na kwa vile *MV Iringa* ni mbovu, ni lini itatengenezwa ili angalao iweze ku-*boost* usafiri katika ziwa Nyasa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Captain* Komba, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kushirikiana na nchi ya Malawi, serikali imepokea na sisi Wizarani tutalifuatilia ili tuone namna ya kuimarisha ushirikiano huo na kuondosha kero ya usafiri kwa wananchi katika ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili linahusiana na *MV Iringa. MV Iringa*, ina uwezo wa kubeba abiria 138 na mizigo tani tano. Hii meli imeshafanyiwa matengenezo makubwa na kwa sasa inaendelea na kazi kama kawaida. *MV Songea* nayo ina uwezo wa kubeba abiria 212 na mizigo tani 40.

Meli hii imefanyiwa matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja na matengenezo ya injini huko Malawi na kwa sasa inaendelea na kazi na inafanya kazi na ipo katika hali nzuri.

Na. 371

**Ukarabati wa Barabara ya Iringa Mikumi**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kwa kutambua kuwa Barabara ni kiungo muhimu sana cha mawasiliano na usafirishaji katika nchi yetu, imeahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 kuzikarabati Barabara zetu nchini na kwa kuwa kwenye barabara ya

Iringa – Mkumi eneo la daraja mbili – Ruaha Mbuyuni imetoboka, darajani na wasimamizi wa Barabara nchini wameridhia kuweka mapipa kwa takriban mwaka mzima sasa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati eneo hilo na inatumia fedha kiasi gani kwa kazi hiyo?

(b) Je, Serikali inafahamu ni ajali ngapi zimetokea kwenye eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali namba 371 la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya daraja la mto Iyovi, II ama Daraja Mbili, yalianza mwezi Desemba 2007 kwa kujenga jukwaa, *Scaffold*, na kukarabati njia ya zamani kwa ajili ya mchepuo wa kupitisha magari kwa muda wakati daraja linakarabatiwa.

Aidha, matengenezo ya mchepuo yalihusisha daraja moja la zamani. Barabara ya mchepu ilikuwa ni urefu wa mita 600. Kazi ya kuziba jamvi, *bridge deck*, ilikamilika mwishoni mwa mwezi Januari, 2008. Kazi zote ziligharimu jumla ya shilingi milioni 10.125.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ajali zilizotokea barabarani katika eneo la Mikumi hadi Ruaha Mbuyuni kwa mwaka 2006 hadi 2008 ni 91 na eneo la daraja la Mto Iyovi II ajali 3. Lakini ajali zote tatu hazikusababishwa na ubovu wa daraja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba, kwa kuwa barabara ya kutoka Mikumi moja kwa moja mpaka Songea ni Barabara Kuu na ni barabara ambayo inatumika sana kwa mizigo mikubwa pamoja na mabasi; na kwa kuwa maeneo hayo hayana usafiri wa ndege; kwa hiyo abiria wake pamoja na Wabunge wanatumia barabara hizo kila wakati; lakini barabara hizo zina mashimo sana kila ukipita kama unaelekea Iringa lazima utakutana na mashimo yamechimbwa na wenyewe pengine hawapo yanakaa hata wiki hayajazibwa na hivyo kusababisha hali ya hatari sana; je, haoni sasa ni wakati muafaka ikiwezekana barabara hiyo ifanyiwe tathmini ya kina na ijengwe kwa lami moja kwa moja badala ya kuendelea kuzibaziba mashimo na kuyaacha muda mrefu na kusababisha hasara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu tafadhali, hiyo barabara ni mbaya kabisa ajali nyingi zinatokea.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, kama ifuatavyo:-

Serikali ina mpango wa kuifanyia ukarabati Barabara Kuu ya TANZAM na Mradi huu wa ukarabati utaanzia Mkoani Morogoro eneo la Mbiovi hadi Iringa Mjini, yenye jumla ya kilomita 150. Mradi unafadhiliwa na mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Denmark kupitia Benki yao ya Biashara ijulikanayo kama Dansk Bank ikidhaminiwa na DANIDA. Mjenzi wa Mradi huu amekwishapatikana na anajulikana. Mkataba ulitiwa saini tarehe 19 Machi, 2008 na kwa sasa mkandarasi amekwishakabidhiwa eneo la Mradi na yupo kwenye hatua za awali za utekelezaji au *mobilisation*.

Mradi unasimamiwa na Mhandisi Mshauri wa *Denmark Consultant Engineers and Planners.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 28, kifungu cha 46 …

**NAIBU SPIKA:** Ukurasa wa Kanuni?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu gani?

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Kifungu cha 46.

**NAIBU SPIKA:** Naomba usome.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Maswali kujibiwa kwa ukamilifu; Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa isipokuwa kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampa Mbunge muuliza swali, nakala ya jibu mapema kabla ya kuanza kikao na kabla muda wa kujibu swali hilo haujafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali namba 364 alisema kwamba, hivi sasa ni miaka 40 Tanzania au Jamhuri ya Muungano haijatekeleza yale mambo 22 ya Muungano na akasema kwamba, suala la Bandari kupakia Mamlaka ya Biashara ya meli halijatekelezwa kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, utaratibu umevunjwa wa Kanuni hii kwa sababu ndani ya miaka hiyo 40 si kweli kwamba, mambo haya manne hayajatekelezwa. Hivi sasa Bandari ya Zanzibar inajengwa na *European Union*, ndiyo waliotoa fedha hizo kwa dhamana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

lakini biashara ya meli hivi sasa ndani ya Tanzania inafanywa kwa kushirikiana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali irudi ikaliarifu Bunge hili na wananchi kwa ujumla ili wasipotoke kwamba katika suala hili, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashirikiana vizuri na tupate jawabu muafaka kama Kanuni inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, Kanuni hii haisemi tuanze kujadili swali sasa; ipo Kanuni muuliza swali kama hakuridhika anaweza kutumia nafasi hiyo kuuliza swali lingine kwamba hakuridhika na majibu. Hii Kanuni haisemi ulivyoeleza wewe.

Kanuni inasema, Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa isipokuwa kama jibu linalohusika ni refu au lina takwimu nyingi, Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao kuanza, kabla ya muda wa kujibu swali hilo kufikiwa. Kwa hiyo, hapa anasema kama ni refu Waziri atoe majibu na kama lina takwimu nyingi atoe nakala.

Ya pili inasema, endapo Mbunge muuliza swali atamwomba Waziri ampatie nakala ya jibu la swali lake kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujafikiwa, basi Waziri anaweza kumpa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu kama ilivyoombwa, tena ni nakala tu.

Ya tatu, Waziri Mkuu au Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anaweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri.

Sasa naona hoja yako haifiti katika hoja hizi zote, sasa kama yule aliyeuliza swali hakuridhika na ninafikri ni Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, kifungu cha 28(11) kinamruhusu yeye kutumia nafasi ya maelezo binafsi kupata maelezo ya ziada kuhusu swali lake. Hapa haihusiki hiyo uliyosema wewe.

Ninapenda pia kutoa ufafanuzi kidogo, wakati Mheshimiwa Diana Chilolo anauliza swali la nyongeza kuhusu swali namba 367, inaelekea kulikuwa na matatizo. Swali namba 367 ambalo lilikuwa linaulizwa na Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi; Waziri alimjibu kama ni Mbunge wa Iramba Mashariki. Kwa hiyo, Waziri alijibu kuhusu Iramba Mashariki ambako ni kwa Mheshimiwa Mgana Msindai. Mheshimiwa Mgana Msindai aliuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Juma Killimbah, jimbo lake ambalo Waziri hakujibu. Kwa hiyo, kumekuwa na *confusion* ya majibu yakijibiwa kwa mtu mwingine na swali la nyongeza.

Mimi nilidhani kwamba, kwa sababu Mheshimiwa Mgana Msindai anatoka Iramba, kweli Mheshimiwa Juma Killimbah aliuliza kuhusu eneo lake, kumbe majibu yalikuwa eneo la Mheshimiwa Mgana Msindai, lakini muuliza swali alikuwa eneo lingine.

Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Diana Chilolo lilikuwa sahihi kwamba, inawezekanaje Mheshimiwa aseme hajui *data* za swali la muuliza swali, *it was unusual.*

Sasa tunapenda Mheshimiwa Waziri, akashauriane tena na ofisini kwake tuone alichokuwa anajibu, yaani lilikuwa ni swali la Mheshimiwa Juma Killimbah au swali a Mheshimiwa Mgana Msindai na tutapenda kupewa maelezo hayo baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika kuwatambulisha wageni. Wa kwanza kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Hawa ni wageni maalum anasema ni Mheshimiwa K. B. Banglat; *when I call your name please you can raise up so that we can see you.*

*Then* tuna Bwana Joshiyahu, *thank you very much*, kuna Ndugu Japhet Mlagala huyu ni wa kutoka *SIDO* tunamfahamu, kuna Bwana Nyiti Tembo, Dr. Samuel Nyatahe, Prof. A. I. Pereka kutoka *TBS*. Mnakaribishwa nyote. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wengine wa Wizara hiyo hiyo ambayo ni sekta binafsi chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; huyu ni Bibi Kilindu, Bwana Aloyce Mwamanga, nafikiri huyu ni Mwenyekiti wa *Chamber of Commerce and Agriculture,* Bwana Machemba, Dr. Evance Meikiza, nyote mnakaribishwa. Hawakuandikwa vyeo vyao, kwa hiyo, sisi hatujui ila ninasoma kama ilivyoandikwa.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, yaani familia yake ambao ni Edmund Makota, Fina Duai, Alice Kaaya na Philbert Christopher na hawa nao uhusiano wao hatuujui.

Kuna wageni wanane kutoka Jimbo la Hanang, hawa nao sasa ni wageni wa Jimbo. Naomba wasimame pale walipo.

*(Hapa wageni waliotajwa walisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Yupo Mkurugenzi Mkazi wa *Face Tanzania*, Peter Hausa asimame.

*(Hapa mgeni aliyetajwa alisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Vilevile yupo Afisa wa Face, Ndugu William Kapenjama, karibuni sana.

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, ana wageni wake ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Sumbawanga; naomba wasimame pale walipo.

**WABUNGE FULANI:** Kesho!

**NAIBU SPIKA:** Ahaa! Ni kesho siyo leo? Ahsante.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, ambao ni mtoto wake Dorah Haule na mwingine ni Emmanuel Kayombo. Kuna Meneja wa Mradi wa Mazingira Wilaya Mbinga, ambaye ni Panus Ndunguru na mdogo wake.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi, nafikiri kuna Keneth Sampampa na Edward Zambi. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Herbert James Mntangi ambao ni Diwani Makame wa Kata ya Mbaramo Muheza, halafu kuna wakereketwa sita wa CCM Muheza Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari; yupo Mchungaji Saimon Nasari. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami; hao ni wakereketwa wa maendeleo 14 kutoka Jimbo la Moshi Vijijini, tunaomba wasimame.

*(Hapa wageni waliotajwa walisimama)*

**NAIBU SPIKA:** Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Said Amour Arfi; hawa wanatoka Baraza la CHADEMA Jimbo la Mpanda, ambao ni Ndugu Seif Ibrahim Ntije, Bwana Raphael William na Bwana Mwangoka Asumbike. Mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi kutoka *Kizota Primary School* na Walimu wao wasimame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 40 kutoka Mlimwa B wasimame na walimu wao, nafikiri wengine watakuwa kule chini.

Halafu Bwana George Mlawa, Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu, alikuwa Mbunge Mwenzetu na Katibu wa Bunge kwa kipindi kirefu sana. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kama nimewaruka wageni wengine, basi nyote mnakaribishwa.

Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza kwamba, wakutane mara baada ya kupindi hiki cha maswali saa nne katika Chumba Namba 117. Kwa hiyo, hawataki kusikiliza Hotuba ya Viwanda? Mimi ningeshauri wakutane baada ya kusoma Hotuba ya Viwanda, maana yake ni wengi, hivyo ni vizuri wakasikiliza kwa sababu Mwanza ni Mji ambao una viwanda pia.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi ya pekee, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kuteuliwa kwake kumedhihirisha imani waliyonayo Viongozi wa Nchi za Afrika kwake na kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitishwa kwa kishindo na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa niaba yangu na ya Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Naibu Waziri, kwa nafasi ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa na imani nasi, kwa kututeua kuiongoza Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Vile vile napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote wapya, walioteuliwa katika nafasi zao baada ya Bunge la Bajeti lililopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mbunge wa Jimbo la Rombo, ambaye alikuwa Waziri wa Wizara hii na Mhe. Hezekiah N. Chibulunje, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Wizara

hii, ambaye sasa ni Naibu Waziri katika Wizara ya Miundombinu, kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika kipindi walichoiongoza Wizara. Kwa namna ya pekee, napenda pia kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Hanang, kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa kama Mbunge wao. Wananchi wa Hanang, wanaendelea kunionyesha upendo mkubwa, nami kwa upande wangu, nitajitahidi katika jukumu langu la kuwawakilisha. Shukrani nyingi sana kwa familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi Prof. Joseph Nagu, kwa upendo wao, ushirikiano na mshikamano wao nami na hivyo kufanya kazi yangu kuwa nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Samuel J. Sitta, Spika wa Bunge letu kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola *(Commonwealth Parliamentary Association).* Uteuzi huu unathibitisha uwezo wako mkubwa katika kuongoza shughuli za Bunge. Aidha, kuteuliwa kwako ni uthibitisho zaidi wa uwezo mkubwa, ukomavu na imani kubwa kwa Jumuiya za Kimataifa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kukupongeza na kukushukuru wewe kwa kuendelea kumsaidia Spika wetu katika kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa. Wabunge wote ni mashahidi kwa namna unavyoendesha kwa uzuri Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kipindi cha bajeti cha mwaka jana, tumeshuhudia matukio mbalimbali hapa Bungeni. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wapya, ambao ni Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma na Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare, Wabunge wa Viti Maalum (CCM); Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro; Mbunge wa Jimbo la Kiteto; na Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir, Mbunge wa Kuteuliwa. Nawatakia mafanikio katika majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majonzi makubwa, naungana na wenzangu katika kuwaombea marehemu Mheshimiwa Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto (CCM), Marehemu Mheshimiwa Salome J. Mbatia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) na Marehemu Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime (CHADEMA). Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amina.*

Napenda pia kumpa pole nyingi Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum (CUF), kwa kufiwa na mwanawe mpendwa na wengine waliokuwemo katika ajali ya gari wakati Bunge hili linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya Hotuba hii, Wizara yangu imefuatilia kwa karibu sana changamoto na masuala ya msingi yanayoihusu Wizara yangu, yaliyoainishwa katika Bunge lako Tukufu kupitia Hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda na zile za Hali ya

Uchumi na Bajeti ya Serikali zilizowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo.

Nawapongeza kwa hotuba zao nzuri, zilizoweka mwelekeo wa shughuli za Serikali na dira ya Bajeti ya Serikali katika mwaka wa 2008/2009. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, masuala na changamoto hizo zimezingatiwa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ninayoiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kutoa Hotuba za Bajeti ambazo zimefafanua mafanikio, shabaha na malengo ya sekta ambazo Wizara zao zinasimamia ambazo pia zinachangia katika maendeleo ya sekta ya viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi (CCM), akisaidiwa na Makamu wake Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Jimbo la Mkinga (CCM); ambao wamechambua kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii na kutoa ushauri na mapendekezo muhimu yanayolenga katika kuboresha utendaji katika kuiendeleza sekta ya viwanda, biashara na masoko. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hoja na michango ya Kamati, imezingatiwa katika bajeti ninayowasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, nikianzia na Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Dr. Stergomena L. Tax; Katibu Mkuu, Dr. Florens M. Turuka; Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara; Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. *(Makofi)*

Pia, napenda kuzishukuru jumuiya za wenye viwanda, wafanyabiashara; waendeshaji wa shughuli za masoko na asasi zisizo za kiserikali, kwa michango yao katika kuendeleza sekta za viwanda, biashara na masoko ambazo Wizara yangu inasimamia. Vilevile napenda kumshukuru mchapishaji wa hotuba hii kwa kuichapisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008, yalizingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2005 na utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), ambapo Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko zinatakiwa kuwa miongoni mwa mihimili mikuu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini, kwa kuifanya Tanzania ifikie kiwango cha kati cha maendeleo ya uchumi wa viwanda unaoongozwa na mauzo nje *(semi-industrialised export-led economy),* kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Ili kuweza kufikia malengo haya, Sekta ya Viwanda inatakiwa kukua kwa asilimia 15 ifikapo mwaka 2010 na Sekta za Biashara na Masoko zinatakiwa ziiwezeshe nchi kukuza biashara ya ndani na nje na hivyo, kunufaika na mifumo ya biashara za kitaifa, kikanda na kimataifa, kwa

kuzifahamu na kuzitumia fursa za masoko zilizopo. Aidha, Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko inatakiwa kuhamasisha na kuwezesha sekta binafsi kuimarisha viwanda ambavyo vipo na kujenga vipya; kuboresha miundombinu ya masoko na mifumo ya upatikanaji na utoaji taarifa za biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya Wizara yangu katika mwaka 2007/2008, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda; Sera ya Taifa ya Biashara; Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo; na Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo; zimezingatiwa kama miongozo mikuu ya utekelezaji. Aidha, shughuli zilizopangwa kutekelezwa zilizingatia hali halisi ya kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 imebainisha kuwa Sekta ya Viwanda ni sekta kiongozi, yenye jukumu la kubadilisha uchumi kuwa uchumi wa kisasa unaojitegemea na viwanda kueneza teknolojia za kisasa katika uzalishaji wa sekta nyingine zote muhimu zikiwemo za kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili. Katika kufikia azma hii, malengo yafuatayo yamepewa kipaumbele:-

(a) Ukuaji wa Sekta ya Viwanda kufikia asilimia 15 ifikapo 2010;

(b) Kuongeza ushiriki wa sekta isiyo rasmi na Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati katika uzalishaji wa bidhaa na kuitazama upya Sera ya Viwanda Vidogo ili kuhakikisha kuwa, inakidhi lengo kuu la kujenga msingi wa uchumi wa kisasa;

(c) Kuendelea kushirikiana na asasi mbalimbali kuboresha zaidi mazingira ya uzalishaji viwandani, ikiwa ni pamoja na miundombinu, sera za fedha na kodi na kujenga maeneo maalum kwa ajili ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;

(d) Kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani ya mazao mbalimbali ya kilimo, mifugo, madini, uvuvi, maliasili na kadhalika;

(e) Kuongeza juhudi za uanzishaji wa viwanda mama;

(f) Kuongeza uwezo katika uwezeshaji wa kitaalamu na mitaji katika Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati;

(g) Kutoa umuhimu katika kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta za kipaumbele, yaani sekta ndogo za nguo, ngozi na usindikaji wa mazao, mkazo ukiwekwa katika mipango ifuatayo:

- Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi.

- Kuendelea na utekelezaji wa programu inayolenga katika kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo.

- Serikali kuendeleza jitihada za kuwapata wabia wa kuwekeza katika Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na Mradi wa Chuma wa Liganga ndani ya mfumo wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara.

- Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya uuzaji nje *(Export Processing Zones - EPZ)* na uwekezaji katika viwanda ndani ya maeneo hayo.

- Kuanzisha utaratibu wa kutenga maeneo maalum ya kiuchumi *(Special Economic Zones – SEZs),* kwa ajili ya uzalishaji utakaolenga masoko ya ndani na ya nje.

- Kubuni mpango wa kuandaa mabingwa katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia ya viwanda.

(h) Serikali kutafuta wabia wa kuendeleza miundombinu ya kiufundi iliyopo nchini, yenye uwezo wa kutengeneza mashine na mitambo *(machine tools)* na kukuza uwezo wa kutengeneza vipuri mbalimbali; na

(i) Kulinda, kuimarisha na kutumia uwezo wa kiteknolojia uliojengwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa, ulifikia asilimia 9.2 mwaka 2007, ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2006 kwa bei za mwaka 2001. Aidha, kiwango cha ukuaji cha Sekta hii kilikuwa asilimia 8.7 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2006. Ongezeko hilo limetokana na kutengamaa kwa upatikanaji wa umeme na kuongezeka kwa uwekezaji viwandani, hali ambayo imechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa viwandani katika kipindi cha mwaka 2007 ikilinganishwa na mwaka 2006. Hata hivyo, juhudi zaidi na mikakati mipya inatakiwa ili kufikia ukuaji wa kiwango cha asilimia 15 ifikapo mwaka 2010 kama nitakavyoelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Wizara imeanza kuandaa Mkakati Unganishi na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda *(Integrated Industrial Development Strategy and Master Plan).* Kama hatua za mwanzo za kuleta matokeo ya haraka (*quick wins*), Mpango huu umeibua Mwambao wa Pwani kuwa Kitovu cha Kuendeleza Viwanda na Kukuza Mauzo Nje (*Water Front Industrial and Export Frontiers*). Mpango huu unalenga kufanya usindikaji wa mwanzo *(primary processing)* mikoani, usindikaji wa kati na usindikaji kwa ajili ya mauzo nje kufanyika katika maeneo ya Mwambao wa Pwani ambao utakuwa Kitovu cha Kuendeleza Viwanda na Kukuza Mauzo nje. Uanzishwaji wa Kitovu cha Kuendeleza Viwanda na Kukuza Mauzo Nje unalenga kuendeleza na kutumia bandari zetu kiuchumi na maliasili zilizopo katika Kanda za Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda hizo ni Ukanda wa Maendeleo wa Tanga ukiwa na Bandari ya Tanga, Ukanda wa Maendeleo wa Kati unaohusisha Bandari ya Dar es Salaam na itakayojengwa Bagamoyo ikiwa ni sehemu ya EPZ na Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara unaohusisha Bandari ya Mtwara. Viwanda ambavyo vitaendelezwa katika Mwambao wa Pwani katika Miji ya Tanga, Bagamoyo na Mtwara ni vile vitakavyotengeneza bidhaa ili kuendeleza biashara ya ndani na kukuza mauzo nje kwa kutumia malighafi zinazotoka katika kanda hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukanda wa Maendeleo wa Tanga utahusisha ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea kitakachotumia fosfati kutoka Minjingu na ammonia kutoka mitambo ya gesi asilia. Viwanda vingine ni Kiwanda cha Magadi *(Soda Ash)* kwa kutumia malighafi kutoka Ziwa Natron, viwanda vya kusindika vyakula na viwanda vitakavyotengeneza singa na bidhaa za singa kutokana na zao la katani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukanda wa Maendeleo wa Kati utakuwa na Maeneo Huru ya Biashara *(Free Trade Zones)*, Eneo Maalum la *EPZ,* viwanda vya kusindika vyakula, ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusindika mbegu za mafuta ya kula. Uchambuzi wa kina utafanyika ili kuandaa Sera na Mkakati wa kuendeleza sekta ya mbegu za mafuta ili kuzalisha mafuta kutokana na mbegu zinazozalishwa hapa nchini, kwa lengo la kutosheleza mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje ya nchi. Pia kutakuwa na Kituo cha Viwanda vya Nguo (*Textile Centre),* ambacho kitakuwa na viwanda vya kuanzia ngazi ya kutengeneza nyuzi hadi mavazi, Kituo cha viwanda vya ngozi vitakavyoanzia na usindikaji wa ngozi na viwanda vitakavyotengeneza bidhaa za ngozi, Kituo cha Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo *(SME Park)* na Kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT Centre).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara utahusisha Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, Kiwanda cha Saruji, Kiwanda cha Mbolea kutokana na gesi asilia na viwanda vingine vitakavyotumia malighafi ya kemikali zitakazotokana na gesi asilia na viwanda vya ubanguaji wa korosho na usindikaji wa bidhaa zitokanazo na zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendeleza juhudi za kuvutia wawekezaji na kukamilisha mazungumzo kati ya Serikali na wawekezaji waliokwishajitokeza, hususan katika kuendeleza Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, Kiwanda cha Saruji, Kiwanda cha Mbolea na kuanzisha Ukanda wa Maendeleo wa Bagamoyo *(Bagamoyo Economic Development Zone).*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vina mchango mkubwa katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Hivyo, katika kuandaa Mkakati na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Viwanda, msisitizo umewekwa katika kuanzisha viwanda vitakavyowezesha usindikaji wa mazao ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakiuzwa yakiwa ghafi na mengine kuharibikia mashambani. Hivyo, pamoja na mambo mengine, uendelezaji wa viwanda vya kusindika vyakula unalenga kuviwezesha viwanda kupata malighafi kwa viwango vya ubora unaotakiwa na kuwawezesha wakulima kupata soko na bei nzuri ya

bidhaa zao kwa kufuata mifumo ya kilimo cha mikataba *(contract farming).* Maandalizi yanafanywa katika Mikoa ya Morogoro na Pwani ili kuwawezesha wakulima kupata mafunzo ya kuzalisha mazao kwa wingi na viwango vya ubora vinavyokubalika kwa ajili ya kiwanda cha usindikaji matunda cha *Unnat* kilichopo Morogoro, ambacho ni miongoni mwa viwanda katika mfumo wa *EPZ.* Aidha, katika mwaka 2008/2009, Wizara itawahamasisha wamiliki wa viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula na wakulima, kuingia mikataba ya kilimo *(contract farming),* yenye tija ili kuwawezesha kuzalisha mbegu za mafuta kwa wingi na kwa viwango vya ubora vinavyohitajika ili kutosheleza mahitaji ya viwanda. Maeneo mengine yatafikiwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na lengo la kutumia malighafi tulizonazo katika kuanzisha viwanda vyetu nchini kama chachu ya kukuza uchumi, msisitizo wa kuvutia uwekezaji na uanzishaji wa viwanda vya pembejeo, hususan viwanda vya mbolea unatokana pia na kutambua umuhimu wa pembejeo katika kuongeza uzalishaji na hivyo kuleta mapinduzi ya kilimo. Katika kutekeleza azma hii, Wizara imeendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vipya vya mbolea na kupanua uzalishaji wa mbolea ya fosfati ya Minjingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi hizi zinatokana na ukweli kwamba, katika siku za hivi karibuni, bei ya mbolea imeongezeka sana na hivyo kutishia kupungua kwa matumizi ya mbolea katika kilimo hapa nchini, jambo ambalo litaathiri azma ya Serikali ya kuleta mapinduzi ya kilimo. Kwa mfano, bei ya mbolea ya aina ya *Di-ammonium Phosphate (DAP)* hivi sasa ni kati ya shilingi 95,000 na shilingi 120,000 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya shilingi 41,000 katika msimu wa kupanda wa 2007/2008.

Kwa kuitambua hali hii na ili kuwawezesha wakulima kupata mbolea, Serikali imeweza kukihamasisha Kkiwanda cha *Minjingu Mines and Fertilizers Limited,* kuongeza uzalishaji wa mbolea ya *Minjingu Rock Phosphate* ili wakulima waweze kupata na kutumia mbolea kwa viwango vinavyokubalika. Hivi sasa *Minjingu Mines and Fertilizer Limited* inaweza kuzalisha tani 60,000 za mbolea kwa mwaka kulingana na makubaliano yaliyofanywa kati ya Kampuni hiyo na Kampuni ya Mbolea Tanzania. Kiwanda hiki kimeihakikishia Serikali kuwa taratibu za kuongeza uzalishaji zimekamilika ili kutosheleza mahitaji. Lengo la kiwanda ni kuongeza uzalishaji hadi kufikia takriban tani 300,000 za mbolea kwa mwaka. Aidha, kiwanda kinaandaa na kukamilisha taratibu ambazo zitakiwezesha kuzalisha mbolea zenye virutubisho vingi zaidi kwa kutumia malighafi na virutubisho maalum (*micro-nutrients*) badala ya kuendelea kuzalisha *Minjingu Rock Phosphate* pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itawezesha kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija katika mazao ya kilimo kwani wakulima wataweza kuongeza virutubisho vya aina ya fosfati kwa kutumia mbolea ya *Minjingu Rock Phosphate* kwa gharama nafuu ikilinganishwa na gharama ya kuongeza virutubisho hivyo kwa kutumia *Di-ammonium Phosphate* ambayo bei yake imepanda sana. Kuongezeka kutumiwa kwa mbolea hiyo siyo tu kunatarajiwa kupunguza gharama za matumizi ya mbolea katika uzalishaji wa mazao kwa zaidi ya asilimia 50, bali pia kutavutia uwekezaji zaidi katika

viwanda vya mbolea katika maeneo ambayo malighafi hiyo inapatikana. Hivyo, nakipongeza sana Kiwanda cha *Minjingu Mines and Fertilizers Limited* kwa kukubali wito wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa wakulima katika mikoa yote Tanzania wanapata mbolea ya fosfati na nyinginezo, Serikali imekamilisha taratibu ambazo zitaiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania *(Tanzania Fertilizer Company - TFC)*, ambayo ina mtandao mkubwa wa usambazaji wa mbolea hapa nchini, kununua na kusambaza mbolea hiyo. Hadi kufikia mwishoni mwa Julai, 2008, *TFC* ilikwishasambaza takriban tani 9,100 za mbolea ya *Minjingu Rock Phosphate* katika mikoa mbalimbali iliyohitaji mbolea hiyo kwa ajili ya kupandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni, Tanzania kama ilivyo katika sehemu nyingine duniani, imekumbwa na mfumko wa bei. Miongoni mwa sababu zinazopelekea mfumko huu wa bei ni bei kubwa za vyakula na bidhaa za viwandani zinazotumika kwa wingi nchini. Hivyo, tutaongeza juhudi hizi za kuendeleza viwanda vitakavyochangia katika kuongeza uzalishaji na kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza usindikaji na uhifadhi wa mazao ya kilimo na hivyo upatikanaji wa bidhaa. Hizi ni miongoni mwa juhudi za Serikali za kudhibiti mfumko wa bei. Juhudi hizi za kuendeleza viwanda zinahitaji sana dhamira ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu imefanya tathmini ya maendeleo ya viwanda nchini na uperembaji wa viwanda vilivyobinafishwa vilivyokuwa chini ya Wizara yangu (uperembaji wa viwanda vilivyobinafsishwa imefanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam, ambao unavyo viwanda vingi na itafanyika katika Mikoa mingine katika mwaka ujao wa fedha). Uperembaji wa viwanda vya Dar es Salaam unaonyesha kuwa hivi sasa zaidi ya asilimia 97 ya viwanda vinamilikiwa na sekta binafsi kwa asilimia 100 au kwa ubia na Serikali. Viwanda ambavyo bado vinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 ni vile ambavyo taratibu za ubinafsishaji bado hazijakamilishwa. Aidha, tathmini ya utumiaji wa uwezo *(capacity utilization)* katika viwanda ambavyo vimebinafsishwa, inaonyesha kuwa utumiaji huu umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 51 kutoka wastani wa asilimia 37 katika mwaka 2006. Pamoja na kuongezeka kwa utumiaji wa uwezo kwa viwanda *(capacity utilization)*, hivi sasa viwanda vingi vinatengeneza bidhaa *(manufacturing)*, badala ya kufanya usindikaji wa awali tu. Aidha, hata katika mikoa ambayo uperembaji haujakamilika, takwimu za awali zinaonyesha kuwa, viwanda kadhaa vimefufuliwa ikiwa ni pamoja na viwanda vya *Morogoro Polyester Textile Mill Ltd* (sasa *21st Century Textile Mill Ltd*), *Morogoro Canvas Mills, Tanzania Packages Limited* (sasa *TPM 1998 Ltd*), na *Morogoro Tanneries (*sasa *EastHides Company Limited)* Mkoani Morogogoro na viwanda vya *Tanga Steel Rolling Mills (*sasa *Unique Steel Rolling Mills*) na *Sabuni Industries Ltd (*sasa *Sabuni Detergents Ltd*) vilivyoko Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2007/2008 kati ya Miradi ya Viwanda 194 iliyopewa *Certificate of Incentives*, asilimia 32 ya miradi hiyo ilihusu

kuongeza thamani mazao ya kilimo na mifugo. Vilevile kati ya miradi 194, miradi 150 ilihusu uwekezaji katika miradi mipya ya viwanda na miradi 44 inahusu upanuaji wa miradi iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itatoa taarifa ya kina kuhusu hali ya viwanda vilivyobinafsihwa mara baada ya zoezi la uperembaji kukamilika. Zoezi hili linatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2008/2009. Taarifa hiyo itaonyesha kwa kina utekelezaji wa makubaliano, mafanikio, changamoto na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta za kipaumbele, Wizara imeanza kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini, ambao unatekelezwa kwa pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania *(Leather Association of Tanzania),* ambayo inawakilisha sekta binafsi.

Mkakati huu unakusudia kukuza uwezo wa viwanda vya ndani ili viweze kusindika ngozi zote hapa nchini badala ya kuuza nje zikiwa ghafi kwa kuhakikisha kuwa, ngozi inayozalishwa ni bora, utaalamu wa kuendeleza sekta ya ngozi na bidhaa zake unajengwa na mauzo ya bidhaa za ngozi nje yanaongezeka. Mkakati huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo ambazo zinatokana na ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje. Kwa kuanzia, Wizara imeanza mchakato wa kufufua na kuimarisha Chuo cha Taaluma ya Ngozi *(Tanzania Institute of Leather Technology)* kilichopo Mwanza; kuimarisha vituo vya mafunzo ya utaalam wa ngozi na utengenezaji wa bidhaa za ngozi vilivyopo Dar es Salaam na Morogoro; na kuanzisha Kituo cha Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi *(Common Leather Goods Manufacturing Facilities Centre)* kwa ajili ya Viwanda vya Kati na Vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuendeleza viwanda mama, Wizara inakamilisha mchakato wa kuwapata wawekezaji katika Miradi ya Mchuchuma na Liganga. Lengo la Serikali ni kupata wawekezaji mahiri watakaoweza kuunganisha miradi hii (miradi ya makaa ya mawe na kuzalisha umeme ya Mchuchuma,na Mradi wa Chuma cha Liganga) na uendelezaji wa miundombinu inayotakiwa kwa kushirikiana na Serikali, ikiwa ni pamoja na barabara, reli na bandari ya Mtwara.

Miundombinu hii itawezesha uendelezaji wa haraka wa miradi hiyo na uibuaji wa miradi mingine ya kiuchumi kwa kutumia mfumo unganishi (*strategic integrated approach)*. Hadi sasa, wawekezaji 81 (38 kwa ajili ya Mradi wa Liganga na 43 Mradi wa Mchuchuma), kutoka ndani na nje ya nchi, wameonyesha nia ya kutaka kuwekeza katika miradi hiyo *(unsolicited bids)*. Makampuni kumi yamethibitisha nia ya kuwekeza katika Miradi ya Mchuchuma na Liganga kwa utaratibu huu. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa, uwekezaji katika miradi hii unafanyika kwa kasi, kwa kutumia mfumo unganishi unaojumuisha ujenzi wa miundombinu muhimu na kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

Aidha, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wabia wa maendeleo kadhaa ili kuwezesha uendelezaji wa haraka wa miradi hii muhimu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeendelea kuvutia wawekezaji kuanzisha mradi wa kutengeneza chuma ghafi katika Mradi wa Kasi Mpya. Mchakato wa kuwapata wawekezaji wa Kitanzania watakaoingia ubia na Shirika la Taifa la Maendeleo *(National Development Corporation - NDC),* umefikia hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kutekelezwa kwa Miradi ya Mchuchuma na Liganga, siyo tu kutaiwezesha Tanzania kuanzisha viwanda mama, bali pia kutaiwezesha nchi yetu kuondokana na uhaba wa mali ghafi zinazotumika hivi sasa katika viwanda vya kuyeyusha chuma. Kwa sasa, viwanda hivi vinategemea sana upatikanaji wa chuma chakavu. Katika miaka ya hivi karibuni, mahitaji ya chuma chakavu yameendelea kuongezeka katika viwanda vya kuyeyusha chuma hapa nchini na nje ya nchi. Uwezo wa kuyeyusha chuma katika viwanda vya hapa nchini umeongezeka hadi kufikia tani 450,000, ikilinganishwa na uzalishaji wa miaka iliyopita wa tani 37,000. Uwezo huu umeongezeka kutokana na kuwepo kwa viwanda 18 kwa sasa, ikilinganishwa na kiwanda kimoja kilichokuwepo katika miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Mahitaji makubwa ya chuma chakavu yamekuwa ni changamoto kubwa, siyo tu kwa viwanda vinavyoyeyusha chuma kutopata malighafi ya kutosha, lakini pia yamehusishwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu unaofanywa na wafanyabiashara na wadau wasio waaminifu. Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika kusimamia biashara ya chuma chakavu, ikiwa ni pamoja na uharibifu mkubwa wa miundombinu unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu, katika mwaka 2007/2008 Wizara imefanya maandalizi ya kutunga sheria itakayosimamia biashara hii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuendeleza viwanda na kukuza mauzo nje, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (*Export Processing Zone Authority - EPZA*), imeendelea kuelimisha na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika maeneo ya *EPZ*. Idadi ya viwanda vipya katika maeneo ya *EPZ* imeongezeka na kufikia 18 ikilinganishwa na viwanda vitano (5) vilivyokuwepo mwaka uliopita. Aidha, wawekezaji katika miundombinu ya *EPZ* wameongezeka na kufikia wanane (8) ikilinganishwa na wawekezaji watano (5) waliokuwepo mwaka uliopita (Jedwali Na. 3 la kitabu cha hotuba). Kwa ujumla, wawekezaji wengi wameonyesha nia ya kuendeleza maeneo hayo kama nitakavyoeleza hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa maeneo ya *EPZ* yanakuwa na huduma zote muhimu, Wizara inawashirikisha wadau wote muhimu katika utengaji na uandaaji wa maeneo ya *EPZ* ikiwa ni pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (*Tanzania Electric Supply Company Limited -TANESCO*), *Tanzania Telecommunication Company Limited* (*TTCL*), Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya

Nishati na Madini, TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira. Hadi sasa, mikoa 12 kati ya mikoa 13 iliyopendekezwa kutenga maeneo ya *EPZ*, imetenga maeneo hayo ikilinganishwa na mikoa mitano (5) ambayo ilikuwa imetenga maeneo hayo mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuleta ufanisi katika uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya uzalishaji na mauzo nje, Serikali iko katika mchakato wa kuunganisha *EPZs* na *SEZs* na kuanzisha Kanda za Maendeleo ya Kiuchumi yaani *Economic Development Zones* (*EDZ*). Uzoefu wa nchi nyingi zinazotekeleza mipango ya maeneo ya uwekezaji kama hii umeonesha kuwa ili mfumo huu uwe wenye tija ni muhimu kuunganisha mipango hiyo na kuwa na maeneo makubwa ambayo yana mfumo wa *Satelite Towns* yakiunganisha viwanda, vituo vya biashara, makazi, mabenki, mahoteli na kadhalika. Mchakato huu utakamilishwa katika mwaka wa fedha 2008/09 ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa *EDZ* ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutoa msukumo mpya katika kuendeleza viwanda, Shirika la *NDC* limekamilisha utayarishaji wa mwelekeo wa Shirika katika misingi ya mfumo wa soko unaolenga kuibua miradi na program mahsusi katika kupanua na kuongeza ufanisi katika uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma; kubuni miradi ya uendelezaji miundombinu kwa ufanisi wa uchumi; kuwatambua na kuwaandaa Watanzania katika uendeshaji wa uchumi wa kisasa na kulinda maslahi ya Taifa katika miradi mikubwa kwa kuwezesha ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Shirika limejielekeza katika utekelezaji wa miradi itakayoanza kujenga misingi ya maendeleo ya viwanda mama, ikiwa ni pamoja na kukamilisha mchakato wa kuwapata wawekezaji katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma kwa uzalishaji wa umeme, uzalishaji wa chuma huko Liganga, kukamilisha uchambuzi wa masuala ya mazingira ili kukamilisha maandalizi ya uzalishaji wa magadi soda katika Ziwa Natron, na kukamilisha uhuishaji wa uzalishaji katika viwanda vya *Kilimanjaro Machine Tools* na *Nyanza Container Glass*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mkakati Unganishi na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini; itaendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji katika Mwambao wa Pwani kama Kitovu cha Kuendeleza Viwanda na Kukuza Mauzo Nje (*Water Front Industrial and Export Frontiers)*, itakamilisha maandalizi ya sheria ya *EDZ* itasimamia ujenzi wa miundombinu muhimu katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuendeleza viwanda na biashara (ikiwa ni pamoja na maeneo ya *EDZ*, *EPZ* na *SEZ*); itakamilisha zoezi la uwekezaji katika miradi ya chuma ya Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kufufua Chuo cha Taaluma ya Ngozi cha Mwanza na vituo vya mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi vya Morogoro na Dar es Salaam; itakamilisha uandaaji wa sheria ya Chuma Chakavu; itaandaa *project profiles* za viwanda, hususan vile vitakavyowezesha usindikaji wa malighafi zinazozalishwa hapa nchini ikiwa ni pamoja na mazao ya kilimo

kwa ajili ya kuvutia wawekezaji zaidi; itaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya maendeleo ya viwanda na itakamilisha zoezi la kuperemba viwanda vilivyobinafsishwa. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia uibuaji wa miradi mikubwa ya kiuchumi na kuendeleza viwanda mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo na biashara ndogo. Malengo yaliyopangwa katika kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo katika mwaka 2007/08 yalikuwa ni pamoja na kufanyia mapitio ya sheria iliyoanzisha Shirika la Viwanda Vidogo (*Small Industries Development Organization - SIDO*) ili iweze kuendana na mahitaji ya sasa ya uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo na kuhamasisha uendelezaji wa ubunifu na usambazaji wa teknolojia muafaka. Aidha, Wizara ililenga kuimarisha upatikanaji wa mitaji, masoko na uwezeshaji wa kitaalam kwa wajasiriamali; kutekeleza programu ya viatamizi ili kuwawezesha wananchi kuibua bidhaa mpya na kujenga vituo vya biashara kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na kuongeza ushiriki wa sekta isiyo rasmi na sekta ya viwanda vidogo na vya kati katika uzalishaji wa bidhaa. Vilevile, Wizara ilipanga kutekeleza programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) ambayo inalenga katika kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara imekamilisha mfumo wa Kitaifa wa kusimamia maendeleo ya viatamizi vya teknolojia na biashara nchini ili kuendeleza na kueneza teknolojia. Programu ya viatamizi imeanza kutekelezwa hapa nchini na taasisi za *SIDO*, *Tanzania Industrial Research Development Organization* (*TIRDO*), *Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization* (*TEMDO*), *Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology* (*CAMARTEC*) na Kituo cha Ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taasisi za utafiti na maendeleo za *TIRDO, TEMDO* na *CAMARTEC* zimeendelea kubuni na kuendeleza teknolojia zinazofaa kwa mazingira ya Tanzania kwa kushirikiana na *SIDO* ambayo imeendelea na juhudi za kueneza teknolojia hizo. Katika mwaka 2007/08, teknolojia 182 zilisambazwa kwa wajasiriamali na mashine 594 zilitengenezwa. Vilevile, *TIRDO* imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 657 kuhusu teknolojia mbalimbali na utengenezaji mashine za uzalishaji bidhaa bora katika viwanda vidogo. Teknolojia hizo zimesaidia kuimarisha uongezaji wa thamani na ubora wa bidhaa katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo na ujenzi. Aidha, Wizara kupitia *SIDO* ilitoa ushauri kwa wajasiriamali 8,717.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri uliotolewa ulilenga katika kuwaelimisha mbinu za kufanya biashara, kutengeneza bidhaa bora na utunzaji wa mitambo. Vilevile, *SIDO* kwa kushirikiana na wadau wengine, ilitoa mafunzo ya ujasiriamali katika nyanja za ufundi na biashara kwa wajasiriamali wapatao 5,700. Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*University of Dar es Salaam Enterpreneurship Centre)* pamoja na *Technoserve,* iliendesha mashindano ya uandaaji wa mipango ya biashara. Mashindano haya yamewajenga washiriki kujiamini na kushiriki katika kuandaa mipango ya biashara katika ngazi ya Kimataifa. Miradi 12 imepata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi hiyo. Aidha, mmoja wa washiriki wa mashindano

haya aliweza kuibuka kuwa mshindi wa kwanza katika mashindano ya Kimataifa yaliyofanyika nchini Netherlands.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na masoko ya bidhaa wanazozizalisha, Wizara kupitia *SIDO* ilifanya maonyesho saba (7) ya bidhaa ya kikanda hapa nchini. Kanda hizo ni Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kati, Kanda ya Kusini na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Maonyesho hayo yalishirikisha jumla ya wajasiriamali 2,271 ambao walifanya mauzo ya bidhaa zenye thamani ya jumla ya shilingi milioni 226.1. Aidha, Wizara yangu kupitia *SIDO*, ilitayarisha na kusambaza kwa wadau Toleo la Pili la Kitabu cha Orodha ya Bidhaa za Wajasiriamali Wadogo (*SME Products Catalogue*). Vilevile, Serikali imeendeleza juhudi za kuwawezesha wanawake katika ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kuonyesha bidhaa zao ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Taasisi na Asasi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo mwaka 1996, wajasiriamali wanawake waliwezeshwa kuonyesha bidhaa zao katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara kupitia Wizara ya Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto. Juhudi hizi za Serikali zimeendelea kuungwa mkono na Taasisi nyingine ikiwa ni pamoja na *Equal Opportunity Trust Fund* (*EOTF*), *SME Competitiveness Facility, Tanzania Gatsby Trust; Pride Tanzania,* Benki za *CRDB* na *NMB*. Juhudi hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa kuwainua wajasiriamali wanawake katika kuendeleza biashara wanazozifanya. Nachukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliounga mkono juhudi hizi na kutoa rai kwa Taasisi nyingine kuungana na Serikali katika kuwaendeleza Wajasiriamali wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha utendaji wa *SIDO*, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza mchakato wa kufanyia mapitio ya sheria ya *SIDO* ili iendane na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea nchini. Kuhusu kuongeza uwezo wa *SIDO* katika kutoa mitaji kwa wajasiriamali, Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wadogo (*National Entrepreneurship Development Fund)* katika mwaka 2007/08 uliongezewa mtaji kwa shilingi 500,000,000. Hadi kufikia Machi 2008, Mtaji wa Mfuko huo umefikia Sh. 3.397bn/=. Jumla ya wajasiriamali 3,219 walipewa mikopo ya thamani ya Sh. 2,287,300,000/= kupitia mfuko huo ambapo kiwango cha marejesho kilifikia asilimia 88 na ajira mpya 5,719 zilipatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara, kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo imekamilisha maandalizi ya msingi kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI). Maandalizi hayo ni pamoja na kuendesha mafunzo kwa watekelezaji wa mradi; kukamilisha mchakato wa kuwapata wataalam waelekezi watakaohusika na utekelezaji wa mradi na kununua vifaa muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itafanya utafiti wa msingi kuhusu viwanda vidogo na biashara ndogo (*SME Baseline Survey*) ili kuanza kujenga benki ya takwimu ya viwanda vidogo na biashara ndogo (*SME Database*) ambayo itakuwa ni kiungo muhimu katika uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara

ndogo. Wizara inaendelea na mazungumzo na wadau ili kuandaa mkakati wa kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo nchini.

Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha ubunifu na usambazaji wa teknolojia muafaka kama vile mitambo ya uchimbaji mdogo wa madini; teknolojia za kusindika mazao ya kilimo, asali na bidhaa zake; vifaa vya ujenzi; teknolojia ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa; na kuendeleza programu ya viatamizi ili kuwezesha wananchi kushiriki katika kuibua mawazo ya kutengeneza bidhaa mpya *(incubators*). Wizara itaendelea kujenga vituo vya biashara kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na itaendelea na utekelezaji wa mradi wa Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya biashara na masoko. Ili kuendeleza na kuimarisha mafanikio tuliyoyapata katika sekta ya biashara, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 inasisitiza masuala yafuatayo:-

(a) Kuweka mikakati itakayoliwezesha Taifa kuhimili ushindani wa biashara kimataifa na kuwa na uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya Kimataifa katika mazingira ya utandawazi;

(b) Kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda (*EAC*, *SADC*) na wa kimataifa (*WTO*) kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji;

(c) Kuhimiza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) katika biashara;

(d) Kuweka mfumo utakaoweka mtiririko mzuri wa masoko ya ndani;

(e) Kuelimisha wananchi kuhusu hakimiliki; na

(f) Kuendeleza Programu Maalum ya Uuzaji Bidhaa Nje (*Export Development Strategy- EDS*), na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mauzo Nje (*Export Development Fund – EDF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya mifumo bora ya masoko yanategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa miundombinu bora ya masoko, kupatikana kwa mitaji na mikopo, kuwepo kwa stadi za biashara na mahusiano kati ya wadau ambayo yanaongozwa na taarifa sahihi za masoko. Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu huo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 inaendelea kuelekeza:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao kwa walengwa;

(b) Kuandaa kitabu cha orodha ya wanunuzi na wasindikaji wa mazao (*Agri-business Directory*) na kuisambaza kwa wadau;

(c) Kutoa mafunzo ya jinsi ya kutumia taarifa mbalimbali za masoko kwa vikundi vya wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara wa kati ili waweze kuzalisha na kuuza kwa kufuata mahitaji ya soko;

(d) Kuwezesha Halmashauri za Miji na Wilaya kuwa na vitendea kazi vya kukusanya, kuchambua na kutunza taarifa za masoko katika maeneo yao;

(e) Kutoa elimu ya kanuni na taratibu za masoko na biashara na nchi za nje, hususan nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na nchi nyingine ambazo zinatoa upendeleo kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zinazoendelea;

(f) Kuandaa mikakati ya kuendeleza soko la ndani;
(g) Kuratibu na kufanya tathmini ya ubora wa miundombinu ya masoko;

(h) Kuweka mfumo utakaowezesha matumizi ya maghala kama dhamana ya kukopea; na

(i) Kuhimiza matumizi ya maghala kwa kuhifadhia mazao ya wakulima kama mkakati wa kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 mauzo ya bidhaa nchi za nje yalifikia Dola za Marekani milioni 2,006.6 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1,736 mwaka 2006. Masoko makuu ya bidhaa hizo yalikuwa Jumuiya ya Ulaya, Bara la Asia, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*Southern Africa Development Community* - SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community* - EAC) (Jedwali Na. 4 la kitabu cha hotuba). Ongezeko hilo la asilimia 15.6, kwa kiwango kikubwa, limetokana na mauzo ya bidhaa zisizo asilia. Mauzo ya bidhaa za viwandani yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 195.8 mwaka 2006 hadi Dola za Kimarekani milioni 309.2 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 58. Thamani ya mauzo ya mazao asilia yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 267.1 mwaka 2006 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 305.1 mwaka 2007 sawa na ongezeko la asilimia 19.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa mauzo nje wa bidhaa za viwandani unaonyesha kasi kubwa zaidi (asilimia 58) ikilinganishwa na ukuaji wa mazao asilia (asilimia 19.5). Aidha, mwelekeo wa biashara katika sekta ya kilimo ambayo kwa miaka mingi imekuwa tegemeo la uchumi wa Taifa letu ni uuzaji wa bidhaa za kilimo badala ya malighafi. Hii ni kuepuka kuendelea kushuka na kuyumba kwa bei za mazao ya kilimo (malighafi). Hivi sasa na siku za usoni tutaongeza juhudi katika kuongeza thamani ya mazao na bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na madini ili kuongeza mchango wa bidhaa hizo katika pato la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa bidhaa kutoka nje umeongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 3,864.1 mwaka 2006 hadi Dola za Kimarekani milioni 4,826.9 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 24.9. Bidhaa za mashine na mitambo

(*capital goods*) zimeongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,435.1 mwaka 2006 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,738.7 mwaka 2007. Ongezeko hilo la takriban asilimia 21 limetokana na kuongezeka kwa ununuzi wa vifaa vya usafirishaji, mashine na bidhaa za ujenzi kulikochangiwa na ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika sekta za madini, mawasiliano na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa malighafi za viwandani kutoka nchi za nje uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 376.5 mwaka 2006 hadi Dola za Kimarekani milioni 428.7 mwaka 2007 ikiwa ni ongezeko la takriban asilimia 14. Hii imetokana na kukua kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda kufuatia mageuzi ya sera za uchumi jumla (*macro-economic reforms*) ambayo yamevutia vitega uchumi vya ndani na nje. Kuendelea kupanda kwa bei za mafuta duniani kumekuwa ni moja ya sababu za kuongezeka kwa gharama za ununuzi wa bidhaa za matumizi ya kawaida (*consumption goods*) kwa asilimia 29.5 kutoka Dola za Marekani milioni 2,052.5 mwaka 2006 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,659.5 mwaka 2007 (Jedwali Na.5 la kitabu cha hotuba).

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kutumia fursa za masoko ya upendeleo (*preferential market access*) yakiwemo yale ya Jumuiya ya Ulaya, AGOA, China, India, Korea ya Kusini na Japan. Jumuiya ya Ulaya ikiwa ni moja ya masoko makuu na pia ya upendeleo, imenunua kutoka Tanzania bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 759.3 katika mwaka 2007 ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 755.7 katika mwaka 2006.

Katika soko la AGOA, bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,518,000 ziliuzwa katika mwaka 2007 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani 3,697,000 zilizouzwa katika mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 18. Katika soko la China, Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani 175,726,700 mwaka 2007 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani 149,327,300 mwaka 2006 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.6. Mauzo ya bidhaa katika nchi ya India yalifikia Dola za Kimarekani milioni 77.3 katika mwaka 2007 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 63.8 katika mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 21.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara katika Jumuiya za Kikanda (*EAC* na *SADC*) inaonyesha mwenendo huo huo na Tanzania imeweza kuongeza mauzo yake katika masoko hayo. Kwa mfano, Tanzania imeweza kuuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 173.1 katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 117.7 mwaka 2006, ikiwa ni ongezeko la asilimia 47.1. Tanzania imenunua kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 106.6 katika mwaka 2007 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 174.4 katika mwaka 2006, kiasi ambacho ni pungufu kwa asilimia 39. Vivyo hivyo, biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) imeongezeka kwani Tanzania imeuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 656.2 mwaka 2007 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 625.9 katika mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongezeka kwa biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine, hususan zile ambazo zinatoa fursa za upendeleo, kwa ujumla Tanzania imeendelea kununua zaidi kuliko kuuza katika nchi hizo na hivyo kuongezeka kwa urari hasi wa kibiashara. Hali hii inapunguza uwezo wa Tanzania kukidhi mahitaji yake ya ununuzi wa bidhaa kutoka nje na ya uwekezaji na hivyo kutegemea zaidi misaada na mikopo. Baadhi ya sababu za kuongezeka kwa urari hasi wa biashara ni pamoja na uzalishaji mdogo, bidhaa zetu kutomudu ushindani katika masoko, hususan katika nyanja za ubora na ukubwa wa gharama za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kuendelea kupanda kwa gharama za uzalishaji kama vile bei za mafuta na uhaba wa umeme. Ili kukabiliana na hali hiyo lazima Tanzania iongeze tija na ufanisi ili kujiimarisha kiushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya biashara ya ndani katika mwaka 2007 ilichangia kwa kiasi cha asilimia 13.8 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 13.5 mwaka 2006. Baada ya kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa biashara ya ndani katika mwaka 2004 ambacho kilifikia asilimia 5.8, sekta hii inaonyesha kukua mwaka hadi mwaka na kufikia asilimia 9.8 katika mwaka 2007 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.5 katika mwaka 2006 (Jedwali Na.6 la kitabu cha hotuba). Hata hivyo, sekta hii bado ina nafasi kubwa sana ya kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa kisasa ambapo viwanda na biashara vinatakiwa kuwa mhimili wa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia kuongezeka kwa bidhaa zitokazo nje katika soko la ndani. Bidhaa nyingine zinazoingizwa nchini ni duni na zimeleta ushindani mkubwa kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Kuimarishwa kwa soko na biashara ya ndani ni muhimu sana katika kujenga uwezo wa kampuni za hapa nchini kuzalisha na kuuza bidhaa nje ya nchi; kuongeza ajira katika sekta za uzalishaji wa bidhaa ambazo zitauzwa hapa nchini; na kuwa na soko la uhakika kwa mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini badala ya kutegemea masoko ya nje ambayo yamegubikwa na vikwazo na ushindani mkubwa. Uimara wa soko la ndani ndiyo utakaojenga uwezo wa nchi yetu kukabiliana na mitikisiko inayotokea katika masoko ya nje ya nchi yetu. Uzoefu unaonyesha kuwa nchi nyingi zilizopiga hatua ya maendeleo ya kiuchumi zilianza kwa kuimarisha soko la ndani katika uuzaji wa kiasi kikubwa cha bidhaa zinazozalishwa katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa soko la ndani naomba kunukuu maneno ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia Wananchi kupitia Hotuba zake za kila mwezi hapo tarehe 30 Juni, 2004, mwanzo wa kunukuu “Soko la ndani ndio mhimili mkuu wa uchumi wa taifa lolote, na ndio mwazo wa ushiriki wetu katika uchumi wa kisasa na utandawazi. Tusione fahari kununua bidhaa kutoka nje. Kufanya hivyo ni sawa na kusema tunachochuma sisi ndani ya nchi tunakipeleka kunufaisha wengine nje ya nchi.............Ningependa mwaka hadi mwaka kiwango cha bidhaa kutoka nje kwenye maduka yetu kipungue, na bidhaa zetu ndizo ziwe nyingi” mwisho wa kunukuu. Kwa hiyo, wananchi wa Tanzania tunatakiwa kuenzi bidhaa zinazozalishwa nchini ambazo zinaendelea kuwa bora zaidi mwaka hadi mwaka ili tujenge soko la ndani imara kwa bidhaa zetu. Kauli mbiu yetu ni “Nunua bidhaa za Tanzania jenga Tanzania”.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa soko na biashara ya ndani katika ujenzi wa uchumi, Wizara imefanya mapitio ya muundo wake ili kuhakikisha kuwa soko na biashara ya ndani zinawekewa utaratibu wa usimamizi unaostahili. Aidha, kama nitakavyoeleza hapo baadaye, Serikali inafanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Halmashauri ya Biashara ya Nje ili kuihuisha na kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*Tanzania Trade Development Authority – TANTRADE*) ambayo itakuwa na jukumu la kuendeleza biashara ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa bei za mazao ya kilimo. Bei ya mkulima kwa baadhi ya mazao asilia zimepanda katika msimu wa 2007/2008 ikilinganishwa na msimu wa 2006/07. Kwa mfano, kahawa aina ya *Arabica* iliuzwa kwa shilingi 1,800/kg ikilinganishwa na shilingi 1,450/kg msimu wa 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 24. Bei ya mkulima wa kahawa aina ya robusta iliuzwa kwa shilingi 600/kg ikilinganishwa na shilingi 500/kg mwaka 2006/2007, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20. Bei ya pamba iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 350/kg mwaka 2006/2007 hadi shilingi 450/kg msimu wa 2007/2008, ikiwa ni ongezeko la asilimia 28.5

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bei ya tumbaku ya mvuke ilipanda kutoka shilingi 983 msimu wa 2006/07 hadi shilingi 1,170/kg msimu wa 2007/08, sawa na ongezeko la asilimia 19. Bei ya korosho iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 600 msimu 2006/07 hadi wastani wa shilingi 724/kg mkoani Mtwara na shilingi 610/kg msimu wa 2007/2008 kwa mikoa mingine ambayo haikutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 21 na asilimia 2 sawia. Kwa kiasi kikubwa ongezeko la bei ya mkulima kwa mazao haya lilitokana na kuimarika kwa bei ya mazao hayo katika soko la nje, lakini pia kutokana na kuboreshwa kwa usimamizi wa ununuzi wa zao la korosho kupitia mfumo wa Stakabadhi za Maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa bei za mazao makuu ya chakula katika masoko ya ndani msimu wa 2007/2008 umepanda kwa ujumla kama hali inavyoendelea hivi sasa katika soko la dunia. Kwa mfano, kati ya mwezi Januari - Mei 2008, bei za mazao makuu ya chakula zimeongezeka kwa viwango vifuatavyo ikilinganishwa na wastani wa bei za mazao hayo kwa kipindi cha Januari – Desemba 2007: Mahindi asilimia 88, mchele asilimia 36, maharage asilimia 39, ngano asilimia 57, uwele asilimia 17, ulezi asilimia 32, mtama asilimia saba na viazi mviringo asilimia 15. Aidha, bei ya nyama ya ng'ombe iliongezeka kwa asilimia 26 katika kipindi hicho. Bei ya mazao mengine zimeonyeshwa katika Jedwali Na. 7 la kitabu cha hotuba.

Aidha, ongezeko la bei ya mazao makuu ya chakula limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao hayo ndani na nje ya nchi. Sababu kubwa zilizoongeza mahitaji ya chakula ni pamoja na mabadiliko ya mahitaji ya aina za vyakula, hususan katika nchi za Asia, ongezeko la matumizi ya nafaka kwa kulisha mifugo na kuongezeka kwa kasi ya uzalishaji nishati mbadala kwa kutumia mazao ya chakula. Aidha, ongezeko hili la bei

linahusishwa na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji wa mazao kulikosababishwa na kuongezeka kwa bei ya nishati ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa bei za mazao makuu ya chakula na mazao asilia nako kunatoa fursa kwa wakulima wa mazao hayo kuongeza kipato ingawa upandaji wa bei za mazao makuu ya chakula unaleta changamoto kubwa kwa wananchi wengi wanaotegemea kununua chakula, hasa wale wenye kipato cha chini na hasa waishio mijini. Hata hivyo, kwa kuwa bei za mazao ya kilimo hupanda na kushuka mara kwa mara na kwa kuwa mwenendo wa muda mrefu wa bei za mazao ya kilimo unaonyesha kushuka kwa bei, ni vyema nchi yetu ikatumia fursa hiyo kujiimarisha na kutumia mapato hayo kuwekeza katika kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo na miundombinu ya masoko bila kuathiri mapato ya wakulima na mazingira. Hii ni kutokana na ukweli kuwa biashara na bei ya malighafi zitokanazo na kilimo zimeonyesha kuyumba zaidi na hazitabiriki pamoja na kwamba bei zimepanda hivi sasa. Hata hivyo, biashara ya bidhaa za viwandani inaongezeka kwa kasi zaidi na bei zake zinaweza kutabirika na kuaminika zaidi kuliko zile za malighafi zitokanazo na kilimo, hasa kinachotegemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, kufuatia kukamilika kwa Kanuni za Sheria ya Stakabadhi za Maghala mwezi Desemba 2006, Wizara yangu ilihamasisha kuanza kutumika rasmi kwa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Kuanza kutumika kwa Mfumo huu ni moja ya jitihada za kupunguza athari za kushuka kwa bei za mazao, hasa mara baada ya mavuno; kufikisha huduma za mikopo vijijini na kupunguza uharibifu na upotevu wa mazao baada ya mavuno. Wizara tayari imekwishaunda Bodi ya Stakabadhi za Maghala (*Tanzania Warehouse Licencing Board*) ambayo ipo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, yenye jukumu la kusimamia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Bodi hii imeshaanza kufanya kazi mwaka 2007/08. Kama ilivyo katika Bodi za Mazao, ugharimiaji wa shughuli za Bodi hii unatokana na ruzuku toka Serikalini. Bodi hii kwa siku za usoni itasaidia kuunganisha ushirika wa wakulima moja kwa moja na masoko badala ya kutegemea wafanyabishara wa kati (*middlemen*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutatua tatizo la soko na bei ya mkulima kwa zao la korosho, Wizara yangu ilianzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika ununuzi wa korosho mkoani Mtwara katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2007/2008. Mfumo huu umekuwa na mafanikio makubwa katika zao la korosho katika Mkoa huu. Kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, hadi kufikia mwezi Mei 2008 jumla ya tani 62,056 za korosho zilikuwa zimenunuliwa kutoka kwa wakulima ikilinganishwa na malengo ya ununuzi na uuzaji wa tani 61,689 katika msimu huo. Wakulima walilipwa wastani wa shilingi 724 kwa kilo ya korosho za daraja la kwanza ikilinganishwa na bei ya shilingi 400 hadi 600 kwa kilo msimu wa 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi 164 vilishiriki katika ununuzi wa korosho kwa kutumia Mfumo huu na kununua korosho zote za wakulima katika maeneo yao kwa kipindi kifupi. Vilevile, Mfumo huu umehamasisha wakulima kupanga na kuuza korosho kulingana na madaraja kwa kuwa asilimia kubwa

ya korosho zilizonunuliwa kutoka kwa wakulima ni za daraja la juu (*standard grade*) ikilinganishwa na hali ya hapo awali ambapo kiasi kikubwa cha korosho zilizonunuliwa kilikuwa hakipangwi kwa madaraja na hivyo kununuliwa kwa bei ya daraja la chini (*under grade*). Faida nyingine iliyotokana na matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni udhibiti wa matumizi ya vipimo visivyo rasmi maarufu kama *kangomba* ambavyo vilikuwa vikitumiwa na wanunuzi binafsi kuwaibia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Maghala umewezesha Vyama vya Ushirika vya Msingi 164 kupata mikopo kutoka benki za biashara, hususan *NMB* na hivyo kuimarika kimitaji, kimapato na kuvijengea uwezo wa kujitegemea. Vilevile, Mfumo huu umevutia na umeongeza ushiriki wa taasisi za fedha, hususan benki za biashara, katika kupeleka huduma za mikopo vijijini katika sekta ya kilimo. Kwa mfano, kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, sekta ya korosho imeweza kupata mkopo wa takriban shilingi bilioni 61.3, kutoka *NMB* na tayari mkopo huo umekwishalipwa. Inatarajiwa kuwa kuongezeka kwa ushiriki wa benki za biashara katika Mfumo huu kutaongeza ushindani katika utoaji wa mikopo na hatimaye kupunguza gharama za mikopo inayotolewa na benki hizo. Hivyo, ninaamini kabisa kuwa pale ambapo kuna mipango na usimamizi madhubuti katika Vyama vya Ushirika, vyama hivyo vinakopesheka, vinaweza kufanya biashara kwa faida na kuondoa umaskini kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala mapato ya Halmashauri yaliyotokana na ushuru wa asilimia tano unaotozwa katika zao la korosho yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 250 kati ya mwaka 2006/2007 na mwaka 2007/2008. Hii inaonyesha kuwa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kupitia ushuru wa asilimia tano unaotozwa katika zao la korosho unaweza kufanywa kwa ufanisi zaidi na kwa gharama nafuu endapo Halmashauri zitashiriki kikamilifu katika kusimamia matumizi ya mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio katika matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika zao la korosho yametokana na ushirikiano mkubwa tulioupata toka kwa wadau mbalimbali. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Kanali Mstaafu Anatoli Tarimo, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, viongozi na watendaji wengine katika Mkoa na Wilaya zake. Aidha, ninashukuru sana Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; *NMB*; Bodi ya Korosho Tanzania; Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vikuu vilivyoshiriki katika kutumia Mfumo huu; Wakala wa Vipimo na Mizani; wafanyabiashara walioshiriki katika kutumia Mfumo huu ikiwa ni pamoja na waendesha Maghala na Taasisi nyingine kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa katika kutekeleza Mfumo huu katika zao la korosho Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeanza maandalizi ya kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika mikoa yote inayozalisha korosho kwa ajili ya msimu wa ununuzi wa mwaka 2008/2009 hatua kwa hatua. Hata hivyo, natoa rai kwa mikoa hii inayozalisha korosho, kuhakikisha kuwa inakamilisha maandalizi muhimu ili kuwezesha mfumo huu kufanya kazi, ikiwa ni pamoja na kuwaandikisha wakulima wote na kuandaa

taarifa kuhusu wakulima, ikionyesha wakulima wote, idadi ya miti ya mikorosho inayomilikiwa na mkulima, kiasi kinachotarajiwa kuvunwa na kuainisha vyama vya msingi vitakavyotumika katika kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala umekuwa wa mafanikio pia katika ununuzi na uuzaji wa mazao mengine kama vile kahawa inayouzwa mnadani, pamba, mpunga na mahindi. Katika zao la kahawa, maghala ya *Tanzania Coffee Curing Company Limited* (TCCCO), Vyama vya Ushirika vya Msingi 32; *Mbinga Coffee Curing Company Limited (MBICCCO)*, Vyama vya Ushirika 10 na *Kanyovu Coffee Curing Joint Enterprise*, Vyama vya Ushirika vinane vimeendelea kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa manufaa makubwa. Maghala mapya matatu yaani Makampuni ya *City Coffee* (Mbeya), *DAE Limited* (Mbinga) na *MBICCCO* (Makambako) yameomba kusajiliwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika kahawa kwa msimu wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Maghala umetumika pia katika ununuzi wa pamba katika Mkoa wa Manyara kupitia Chama cha Ushirika cha Oridoy na Mkoa wa Shinyanga kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Sengwa, Witamhilya na Mwanadilanha ambavyo vinaunganishwa moja kwa moja na kinu cha kuchambua pamba. Wakulima wameweza kulipwa malipo ya awali ya wastani wa shilingi 500 hadi 555 kwa kilo. Malipo ya awamu ya pili ya wastani wa shilingi 55 kwa kilo yanatarajiwa. Maandalizi ya kutumia mfumo huu katika zao la pamba katika mikoa ya Manyara, Shinyanga na Mwanza yanaendelea kufanywa. Uhamasishaji na utoaji wa elimu umefanywa katika Mkoa wa Shinyanga kufuatia mwamko mkubwa wa wakulima wa mkoa huo ambao ulitokana na mafanikio yaliyopatikana katika Vyama vya Ushirika vitatu vilivyotumia utaratibu huu katika ununuzi wa pamba katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2007/2008.

Aidha, mafunzo ya matumizi ya mfumo huu yamefanywa kwa vyama vya ushirika mkoani Shinyanga na Mwanza ili kuviandaa Vyama vya Ushirika katika mikoa hiyo kushiriki katika mfumo huu msimu ujao wa ununuzi wa pamba. Hata hivyo, natoa rai hasa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Shinyanga na Mwanza kuunga mkono juhudi hizi za kuwakomboa wakulima katika minyororo ya wanunuzi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wanapata manufaa zaidi kuliko wakulima katika ununuzi wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Mfumo yameongezeka pia katika mazao ya nafaka, hususan mpunga. Wakulima wa mpunga wilayani Ifakara kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi 29 wamenufaika na Mfumo huu kwa kuhifadhi kilo 122,020 za mpunga katika ghala la *Kilombero High Quality Rice* na kujipatia wastani wa bei ya Sh. 374/= kwa kilo ya mpunga ikilinganishwa na bei ya Sh. 280/= kwa kilo wakati wa mavuno. Hili ni ongezeko la mapato la asilimia 34 baada ya kuondoa gharama za hifadhi. Aidha, tani 40 za mchele zilihifadhiwa katika ghala la *TCCCO* na baadaye mchele huo kuuzwa kwa Sh. 800/= kwa kilo baada ya kuondoa gharama nyingine ikilinganishwa na wastani wa bei ya Sh. 550/= hadi Sh. 600/= kwa kilo wakati wa mavuno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nieleze kwa ufasaha suala la matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kutokana na umuhimu wa Mfumo huu katika maendeleo ya kiuchumi ya wananchi ambao Wabunge tuliopo hapa tunawawakilisha. Ni imani yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge tutakuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kusimamia matumizi ya mfumo huu ili wakulima waweze kupata manufaa zaidi kutokana na shughuli za kilimo wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kukuza mauzo nje. katika mwaka 2007/2008 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ililenga kukamilisha maandalizi na kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Kukuza Mauzo Nje. Vilevile, Serikali ilipanga kukamilisha Mpango Unganishi wa Biashara (*Tanzania Trade Integration Strategy - TTIS*) ambao unalenga katika kuhakikisha kuwa masuala yote kuhusu maendeleo ya sekta ya biashara yanaainishwa na kutekelezwa na kuratibiwa kwa pamoja na kwa ufanisi ili kuiwezesha sekta ya biashara kuwa na nafasi kubwa ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imekamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Kukuza Mauzo Nje. Mwelekeo wa Mkakati huu ni kutatua changamoto za uzalishaji (*supply side constraints*); kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani; kujiimarisha katika masoko yenye masharti nafuu, masoko ya kikanda na masoko ya upendeleo. Kwa kuanzia Mkakati huu umebainisha maeneo yanayoweza kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kuleta matokeo ya haraka (*quick wins*). Maeneo yafuatayo yamebainishwa:-

(a) Sekta ya Kilimo: Korosho, pamba, kahawa, chai, matunda, maua na mboga;

(b) Sekta ya Mifugo: Nyama na mazao yake, na ngozi na bidhaa zake;

(c) Sekta ya Misitu na Nyuki: Bidhaa zitokanazo na misitu, asali na nta;

(d) Sekta ya Utalii: Mahoteli ya viwango katika maeneo maalum ya kitalii, utalii katika hifadhi za taifa, mapori ya akiba, fukwe na hifadhi za bahari;

(e) Sekta ya Uvuvi: Mazao ya maziwa (*lakes*) na bahari, na mashamba ya samaki;

(f) Sekta ya Madini: Vito vya thamani, dhahabu na almasi; na

(g) Bidhaa za pamba: Nyuzi, vitambaa vya marudufu, vitambaa vilivyotiwa rangi na mavazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mkakati Unganishi wa Biashara Tanzania umeandaliwa kwa kushirikiana kwa karibu sana na sekta binafsi na sasa umekamilika. Mkakati huu utatekelezwa kuanzia mwaka 2008/2009 hadi mwaka 2013/2014 na kugharimu takriban Dola za Kimarekani milioni

175. Mkakati unalenga kupambana na changamoto za biashara za kiuzalishaji, kukuza sekta ya biashara ya ndani na ya nje, na kujenga uwezo wa wafanyabiashara na hatimaye kuongeza mchango wa sekta ya biashara katika ujenzi wa uchumi wa kisasa utakaosukumwa na sekta ya biashara. Tayari kiasi cha Dola za Kimarekani 1,000,000 zimepatikana. Aidha, nchi za Sweden, Switzerland na Denmark zimekubali kuchangia kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huu na kufikia malengo yake, sekta mbalimbali za uchumi zimeainisha maeneo muhimu yatakayohusika. Katika hatua za mwanzo, Mkakati huu umelenga kuimarisha huduma za kukidhi ubora na kujenga uwezo wa biashara ya ndani kwa madhumuni ya kukuza biashara ya nje ili kuuza bidhaa zenye viwango vya ubora unaotakiwa na hivyo kuongeza uwezo wa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za biashara katika zama hizi za ushindani. Ninatoa rai kwa wafanyabiashara na sekta binafsi kwa ujumla wake kuunga mkono juhudi hizi kwa kuzitumia fursa za biashara na masoko kikamilifu. Hii ndiyo namna pekee ya kuwezesha ukuaji wa biashara ya ndani na nje na hivyo kuhakikisha kuwa sekta ya biashara inachangia ipasavyo katika kukuza uchumi na kuondoa umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uendelezaji wa masoko na biashara ya ndani katika mwaka 2007/2008 Wizara ililenga kukamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo; kuandaa mkakati wa utekelezaji na kuhamasisha umma kuhusu Sera hiyo; na kukamilisha taratibu na kanuni za kuanza kutumika kwa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (*Business Activities Registration Act – BARA*). Aidha, Wizara ililenga kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa masoko ya Kimataifa (*Integrated International Markets*) ya mazao ya kilimo; kufanya tathmini ya mahitaji ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko ya mazao na kuzishauri Halmashauri kuendeleza miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo inayolenga kutoa mwongozo mpana wa jinsi ya kuboresha mfumo wa masoko ya mazao na bidhaa za kilimo imeridhiwa na Serikali. Vile vile, rasimu ya Kanuni za Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (*BARA*) ambayo iliridhiwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2007 imeandaliwa. Inatarajiwa kuwa Kanuni hizi zitakamilika katika robo ya kwanza ya mwaka 2008/2009 ili Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara ianze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa masoko ya kimataifa ya Segera na Makambako. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Wizara yangu itaendelea na mchakato wa kukamilisha michoro ya masoko hayo na kuendeleza jitihada za kuvutia wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Halmashauri za Wilaya husika. *Kilimo Trust* yenye makao yake nchini Kampala, Uganda imeonyesha nia ya kusaidia juhudi za kukutanisha wawekezaji watarajiwa wa miradi hii katika mwaka 2008/2009 na ni imani yangu kuwa tutapiga hatua kubwa katika mchakato wa ujenzi wa masoko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilipanga pia kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za kibiashara utakaounganisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi (*Global Electronic Data Interchange Network*); kuvutia wawekezaji katika kuanzisha miji/vitovu vya kibiashara na kiviwanda (*industry and trade hubs*). Pia, Wizara ililenga kukamilisha mazungumzo na wawekezaji kwa lengo la kuanzisha kituo cha kwanza cha kibiashara cha kimataifa (S*atellite Town and Trade Hub*) huko Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kupata mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za kibiashara utakaounganisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi unaendelea. Changamoto iliyopo ni kupata makampuni ya ndani yatakayoshirikiana na makampuni ya nje yenye utaalamu na uwezo wa kuanzisha mfumo huu. Wizara inatarajia kuwa katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 mtaalamu wa kuanzisha mfumo huu atakuwa amepatikana na mfumo huu utakuwa umeanzishwa. Aidha, mfumo huo utaunganishwa na mfumo uliopo sasa wa kutoa taarifa ambao unakusanya taarifa katika masoko 96 ya mazao ya kilimo na masoko 30 ya mifugo. Hii itawezesha kuendelea kukusanya na kutangaza bei za mazao mara tatu kwa wiki katika vyombo vya habari,  hususan magazeti na kupitia ujumbe mfupi wa simu za mikononi (*sms*). Ni azma ya Wizara kufanya tathmini ya kina kuhusu mahitaji ya taarifa za masoko yetu na kutumia ushauri wa wadau wa taarifa za masoko ili kuboresha na kurahisisha upatikanaji na matumizi ya taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na maandalizi ya kuanzisha Ujenzi wa Kitovu cha Biashara na Mji Mpya wa Kisasa *(Trade Hub and Satellite Town)* katika eneo la Mbegani, Bagamoyo. Mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na wawekezaji waliojitokeza ikiwa ni pamoja na kutoka nchi za Falme za Kiarabu. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea na azma ya kuvutia wawekezaji ili kuanzisha miji/vitovu vya kibiashara *(trade hubs)* na kukamilisha mazungumzo na wawekezaji ya kuanzisha ujengwaji wa kituo cha kibiashara cha Kimataifa (S*atellite Town and Trade Hub*) huko Bagamoyo. Vilevile, Wizara itaendeleza mchakato wa umilikishaji wa eneo la *Kibaha Re-Export Centre* lililopo Chamakweza na kuwatafuta wawekezaji wa kuendeleza kituo hicho kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo kufuatia kuridhiwa kwa Sera hiyo na Serikali; itahamasisha umma na kuisambaza Sera husika; itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za masoko zilizopo; na kuendeleza tathmini ya ubora na mahitaji ya miundombinu ya masoko. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji taarifa za masoko na biashara utakaounganisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika maelezo yangu, Sekta za Biashara na Masoko zinao mchango mkubwa katika kuendeleza kilimo na hivyo kukuza uchumi na kuondoa umasikini, kwani mazao ya kilimo hayana budi kusindikwa na kukidhi viwango vya ubora ili kuweza kupata bei nzuri na masoko ya uhakika ya ndani

na nje.  Mikakati iliyoandaliwa na Wizara yangu itachangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Hivyo, ni dhahiri kuwa jitihada za kuleta mapinduzi ya kilimo hazina budi kujielekeza pia katika kuendeleza sekta za biashara na masoko ya mazao na bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa. Ili kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji katika mwaka 2007/08, Serikali iliazimia kukamilisha taratibu za kuanzisha eneo huru la kibiashara katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na kukamilisha majadiliano ya Ubia wa Uchumi na Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*Economic Partnership Agreement - EPA*).  Pia, Wizara ilipanga kuendelea kuhamasisha wafanyabishara kutumia kikamilifu fursa za masoko nafuu tulizonazo. Katika kujiimarisha na kupanua masoko ya bidhaa nje ya Jumuiya zetu, Serikali ilipanga kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na nchi mbalimbali ambazo ni masoko ya kutegemewa, ikiwa ni pamoja na yale yaliyopo Mashariki ya Mbali na Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeshiriki kikamilifu katika kuimarisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na kuendeleza jitihada za kuondoa vikwazo visivyo vya kiushuru (*non-tariff barriers*) na kuendelea kurahisisha vigezo vya Uasilia wa Bidhaa (*rules of origin*) kwa nchi wanachama. Aidha, Wizara yangu iliendelea kushiriki kikamilifu katika maandalizi na majadiliano na nchi wanachama wa *SADC* kwa lengo la kupanua masoko ambapo mwezi huu wa Agosti mwaka 2008 nchi wanachama wa *SADC* zitazindua Eneo Huru la Biashara (*Free Trade Area*).  Tanzania imekwisha kamilisha maandalizi ikiwa ni pamoja na kupunguza viwango vya ushuru wa bidhaa kufikia asilimia 85 na kuondoa vikwazo visivyokuwa vya kiushuru. Hivi sasa Tanzania iko katika maandalizi ya majadiliano ya kuunda Umoja wa Forodha wa *SADC*. Ili tuweze kufanya majadiliano yenye maslahi ya Taifa, Wizara yangu katika mwaka 2008/09 itakamilisha chambuzi zote zinazotakiwa ili Tanzania iweze kujipanga vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kufikia mwisho kwa makubaliano ya Cotonou (*Cotonou Agreement*) ambayo yalikuwa yanatoa fursa ya upendeleo katika soko la Jumuiya ya Ulaya kwa nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (AKP), nchi zilitakiwa kuingia katika makubaliano mapya yatakayoendana na taratibu za kibiashara chini ya Shirika la Biashara Duniani (*WTO*). Katika utaratibu huu mpya, nchi wanachama wa AKP zinatakiwa kuwa na Mkataba wa Ubia wa Uchumi *Framework Economic Partnership Agreement - EPA*) zikiwa katika Makundi ya Kiuchumi ya Kikanda. Ili kuhakikisha kuwa makubaliano hayo mapya yanakuwa na manufaa kwa Tanzania, uchambuzi wa kina ulifanyika kuainisha faida na hasara kwa Tanzania kushiriki majadiliano ya Ubia wa Uchumi na Jumuiya ya Ulaya; kubainisha kundi linalofaa zaidi kwa Tanzania, ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na kuainisha njia nyingine mbadala. Uchambuzi ulionyesha kuwa njia muafaka na yenye manufaa kwa Tanzania ni kuendeleza majadiliano ya *EPA* kwa kupitia kundi la *EAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania na nchi nyingine wanachama wa *EAC* zimetia saini Mkataba wa Mpito wa Ubia wa Uchumi (*EPA*) mwezi Novemba, mwaka 2007 Mjini Kampala, Uganda. Maandalizi na majadiliano yanaendelea kati ya nchi za *EAC* na *EU* ili kuwezesha kukamilishwa kwa Mkataba wa Ubia wa Uchumi unaotarajiwa kusainiwa ifikapo mwezi Julai, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili katika uchumi na maendeleo ya Tanzania, Wizara imefanya mikutano na wadau na imeendelea kutoa elimu ili kuwezesha umma kufahamu maana ya Mkataba unaotarajiwa kutiwa saini mwaka 2009 na kupata maoni ya wadau toka sekta mbalimbali. Katika kutoa elimu kwa Umma, Wizara imetoa machapisho mbalimbali, na imefanya Semina za Kanda ya Dar es Salaam; Kanda ya Mashariki; Kanda ya Kaskazini; Kanda ya Ziwa; Kanda ya Kati; Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; Kanda ya Kusini na Zanzibar. Aidha, Wizara iliandaa Warsha ya Wabunge iliyofanyika tarehe 23 Aprili 2008 ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kulifahamu suala hili vizuri zaidi na kutoa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao muhimu iliyotolewa katika Warsha hii. Pia, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hoja zilizotolewa zitafanyiwa kazi na ushauri utazingatiwa katika kukamilisha Mkataba wa Ubia wa Uchumi unaotarajiwa kusainiwa ifikapo mwezi Julai, 2009. Katika mwaka 2008/09, Wizara yangu imepanga kuendelea na majadiliano na wadau; kukamilisha chambuzi za masuala muhimu ili kujipanga vema katika kukamilisha majadiliano yanayoendelea na kutoa elimu kwa umma kupitia machapisho, vipindi vya redio na luninga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya Doha yanayoendelea chini ya Shirika la Biashara la Dunia. Hii ni pamoja na Tanzania kuwa mwenyeji wa mikutano muhimu ya *WTO* hapo Novemba 2007 iliyohusu masuala ya misaada ya biashara (*aid for trade*). Pamoja na mazungumzo hayo kuvunjika tena, Tanzania itaendelea kujipanga ili kujadiliana kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano na nchi nyingine. Tanzania ilisaini mkataba wa biashara na Algeria mwezi Desemba mwaka 2007 kwa nia ya kukuza na kuendeleza biashara. Aidha, Wizara iliratibu mkutano wa wafanyabiashara na wawekezaji wapatao 60 kutoka Jimbo la Guangdong, China. Wafanyabiashara wa Tanzania na China walifikia makubaliano na kusaini hati za makubaliano katika maeneo ya kutengeneza viatu na bidhaa za ngozi; uendelezaji wa biashara ndogo na za kati; bidhaa za mbao; madawa; uvuvi; madini na vito; na ujenzi. Aidha, Wizara iliwezesha wadau kushiriki katika maonyesho na Kongamano la Biashara la Kimataifa lililofanyika mwezi Oktoba 2007 mjini Xiamen, China. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea na juhudi za kuendeleza uhusiano wa kibiashara na uwekezaji na nchi nyingine ikiwa ni pamoja na zile za Mashariki ya Mbali, Asia na Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Biashara cha Dubai. Mwezi Novemba 2007, Wizara kupitia Kituo cha Biashara cha Dubai kilichoanza kufanya kazi tangu mwaka wa fedha 2006/07 kwa kushirikiana na *Sharjah Chamber of Commerce and*

*Industry* iliandaa kongamano la kuhamasisha biashara na uwekezaji. Taasisi za *EPZA*, *State Mining Corporation* (*STAMICO*), *Zanzibar National Chamber of Commerce*, *Industry and Agriculture* (*ZNCCIA*), *Tanzania Horticulture Association* (*TAHA*), *Tanzania Petroleum Development Corporation* (*TPDC*), *Tanzania Airports Authority* (*TAA*) na *Zanzibar Investment Promotion Agency* (*ZIPA*) zilishiriki. Pia, Kituo kiliandaa maonyesho ya bidhaa za Tanzania zikiwemo matunda, viungo, samaki, mbao, madini, vito, korosho na mazao mengine ya kilimo kwa ajili ya kutafuta masoko huko Sharjah katika Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada hizi zimewezesha kuvutia wawekezaji ili kuendeleza sehemu ya *EPZ* Mbegani. Aidha, wawekezaji wameonyesha nia ya kuendeleza eneo la Kigamboni kwa kujenga majengo ya maofisi, maduka ya kisasa (*shopping malls*), makazi, na kushiriki ujenzi wa daraja la Kigamboni. Maandalizi ya awali ya ujenzi wa mahoteli yameanza. Mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na wawekezaji katika uchimbaji wa dhahabu, jasi (*bauxite*), miradi ya kuzalisha umeme toka *Stigler's Gorge* na uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma. Pia, Kampuni za ndege katika nchi za Ghuba zinaangalia uwezekano wa kuanzisha safari za ndege kuja Tanzania. Wizara, kupitia Kituo cha Biashara cha Dubai na kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii Tanzania kiliratibu ushiriki wa Tanzania katika maonyesho ya kutangaza utalii (*Arab Travel Market*) mjini Dubai ambayo yalihudhuriwa na taasisi na kampuni mbalimbali kutoka Tanzania. Ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa, Kituo kimezindua tovuti yake kwa ajili ya kupashana habari na kimeandaa na kusambaza matoleo mawili ya jarida la biashara linalolenga biashara na nchi za Falme za Kiarabu na Mashariki ya Kati. Katika mwaka 2008/2009, Kituo cha Biashara cha Dubai kitaendeleza juhudi za kuwaunganisha wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania na wale wa nchi za Ghuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Biashara cha London. Katika mwaka 2007/2008 Kituo cha Biashara cha London kimeendelea kutangaza bidhaa za Tanzania kwa kutumia sampuli kupitia maonyesho na mikutano na hata kushirikisha kampuni kutoka Tanzania ili kuzipatia masoko ya Uingereza na nchi nyingine za Ulaya. Kituo kiliwezesha makampuni manane (8) kutoka Tanzania Bara na Visiwani kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ya bidhaa za chakula yaliyofanyika London. Bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na viungo vya chakula, asali, mvinyo na bia zilitangazwa katika maonyesho hayo. Aidha, katika mwaka 2007/08 Kituo cha Biashara cha London kwa kushirikiana na *BET, SIDO* na Kampuni ya Uingereza ya *The Village Collection* kilinadi vinyago vya Tanzania vilivyochongwa kutokana na miti na mawe, vikapu, mikoba, nguo za ufumaji, batiki, khanga, bidhaa za uchoraji na mapambo mbalimbali katika maonyesho ya *Birmingham Spring Fair*. Aidha, Kituo hicho kimeratibu pia ziara za wawekezaji wanaokuja Tanzania na wafanyabiashara wa Tanzania waendao Uingereza. Vilevile, Kituo kimekuwa kiungo muhimu katika kutangaza utalii. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Kituo hiki kitaendelea kuvutia wawekezaji na kutafuta masoko ya bidhaa zitokazo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Halmashauri ya Biashara ya Nje *(Board of External Trade – BET)*, iliandaa Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kati ya tarehe 28 Juni hadi 8 Julai 2007. Maonyesho ya mwaka huu yalivutia

nchi 28 ikilinganishwa na nchi 25 kwa mwaka 2006, makampuni 1,500 ya ndani yalishiriki ikilinganishwa na 1,400 mwaka 2006. Aidha, makampuni 320 kutoka nje ya nchi yalishiriki katika mwaka 2007 ikilinganishwa na makampuni 108 yaliyoshiriki mwaka 2006. Maonyesho hayo yalitembelewa na watu wapatao 600,000 ikilinganishwa na 560,000 mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha matumizi ya uwanja wa maonyesho, *BET* imekamilisha maandalizi ya *Master Plan* na hivi sasa mazungumzo na vyombo mbalimbali vya fedha na wahisani yanaendelea ili kuendeleza uwanja huo. Aidha, *BET* imeanzisha maonyesho ya kisekta. Maonyesho ya kisekta yanatoa fursa maalum ya kuwawezesha wajasiriamali, wafanyabiashara na wawekezaji kujifunza kwa kina mbinu muhimu na kuweka mikakati thabiti katika kukuza biashara na uwekezaji ndani na nje ya nchi katika sekta husika ikilinganishwa na maonyesho ya jumla. Hadi kufikia Juni 2008, *BET* imeweza kuratibu maonyesho katika sekta za Elimu na Uchapishaji; Chakula na Usindikaji; Sanaa za Mikono na Samani za Majumbani; Usafiri na Usafirishaji; na Sekta ya Nguo na bidhaa za Ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukuza masoko na biashara nje ya nchi, *BET* iliwezesha wafanyabiashara na wajasiriamali wa Tanzania kushiriki katika maonyesho 12 ya biashara ya kimataifa. Kati ya maonyesho haya, tisa (9) yalikuwa Barani Afrika, hususan katika Kanda ya *EAC* na *SADC*; na maonyesho matatu (3) yalikuwa katika bara la Asia (India, Japan na China). Aidha, *BET* kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya InWent ya Ujerumani ilianza kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali yenye lengo la kuwawezesha kuingia katika masoko ya nje. Mafunzo hayo yanatolewa kwa wajasiriamali 30 katika vituo vya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuimarisha biashara baina ya Tanzania na Comoro, *BET* iliratibu ziara ya wafanyabishara 30 kwenda Comoro ili kufanya mazungumzo na wenzao katika kisiwa hicho. Aidha, baada ya kukamilisha utafiti kuhusu biashara kati ya Tanzania na Msumbiji, *BET* iliandaa mkutano wa wadau waliopo mkoani Lindi na Mtwara ili kuwajulisha fursa na changamoto zilizopo katika kuendeleza biashara baina ya nchi mbili hizi. Ili kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kimataifa zinazoendeleza biashara, *BET* imeshiriki katika mikutano iliyoandaliwa na *Global Association of Exhibition Industry –* UFI; *Bureau of Intenational Exhibition* (*BIE*) na *World Trade Point Federation*. Aidha, *BET* imeshiriki kikamilifu katika majadiliano yanayohusu maendeleo ya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi za kukuza biashara, bado zipo changamoto nyingi hasa katika kuendeleza biashara ya ndani. Kwa kuzitambua changamoto hizi, Wizara imeanza mchakato wa kuweka mfumo mzuri utakaoimarisha soko na biashara ya ndani ili kuwa chachu ya kuendeleza ujasiriamali na kukuza mauzo nje. Serikali imeridhia kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - T*ANTRADE* ambayo itasimamia maendeleo ya biashara ndani na nje ya nchi. Wizara imepitia muundo wake ili kuhakikisha kuwa shughuli za kisera za kuendeleza masoko na biashara ya ndani na nje zinazingatiwa na kushughuliwa kikamilifu. Katika mwaka wa

fedha 2008/09, maandalizi ya kuanzishwa kwa T*ANTRADE* yatakamilika, lengo ni kwa *TANTRADE* kuanza shughuli zake katika mwaka wa fedha wa 2008/09. Maandalizi haya ni pamoja na kufanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Halmashauri ya Biashara ya Nje ili Mamlaka itakayoundwa isimamie biashara ya ndani na nje kwa ukamilifu na upeo stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Elimu ya Biashara *(College of Business Education - CBE)* kiliendelea kutoa mafunzo katika fani za Uhasibu, Masoko, Ugavi, Mizani na Vipimo, Elimu ya Biashara, kompyuta na ujasiriamali. Katika mwaka 2007, *CBE* ilitoa wahitimu 1,440 katika fani mbalimbali ikilinganishwa na wahitimu 1,134 mwaka 2006. Aidha, Chuo hiki ni Chuo pekee kinachotoa masomo ya Vipimo na Mizani katika nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika. Fani hii ni adimu na muhimu sana katika biashara. Chuo kinaendelea kuimarisha fani hii ili hatimaye kuifanya *CBE* kuwa *Centre of Excellence* katika fani ya vipimo na mizani katika eneo hili la nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CBE* pia imeongeza Kampasi moja Jijini Mwanza, Kanda ya Ziwa katika azma ya kufikisha elimu ya biashara karibu zaidi na Watanzania, hususan wale waishio katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara, Kagera, Manyara, Arusha na Singida. Aidha, Chuo kinatarajia kuanza kutoa masomo ya shahada ya kwanza katika kipindi cha masomo cha mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma. Katika mwaka 2007/2008, Serikali ililenga kukamilisha Kituo cha Ufungashaji, kuendelea kuweka viwango ikiwa ni pamoja na viwango vya utunzaji wa mazingira, ubora wa ardhi, mbolea; kuboresha maabara za Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards - TBS*) ili ziweze kukubalika kimataifa; kurekebisha Sheria ya Shirika hilo; na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji (*tracebility*). Aidha, Serikali iliazimia kuanzisha vituo na kuweka wakaguzi wa *TBS* sehemu za mipakani ili kudhibiti uingizaji wa bidhaa bandia na zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyopangwa, *TBS* imefungua vituo mipakani katika miji ya Horohoro, Holili na Bandari ya Tanga ili kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini. Kituo cha Sirari kinatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni. Vile vile, *TBS* inafanya majaribio ya Kituo cha Ufungashaji (*Packaging Technology Centre*) ambacho kitatoa huduma za mafunzo ya upimaji wa sampuli za viwanda vya vifungashio na kuhakiki vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zinazotoka nje kwa lengo la kuongeza na kudumisha ubora wa bidhaa. Aidha, mwezi Desemba 2007 Maabara ya Chakula (*Food Microbiology*) ya *TBS* ilipata cheti cha umahiri (*Laboratory Accreditation to* ISO 17025) na hivyo kuwa maabara ya pili nchini kufikia hatua hii. Bunge lako litakumbuka kuwa Maabara ya Ugezi (*Metrology Laboratory*) ilipata cheti cha umahiri mwezi Desemba 2006. Hivyo, bidhaa zinazohakikiwa na TBS kupitia maabara hizo sasa zitakuwa zinakubalika kimataifa. Hali kadhalika, marekebisho ya Sheria ya Viwango (*The Standards Act* of 1975) yapo katika hatua za juu ili iweze kuendana na mazingira ya wakati huu ya kiuchumi na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2008, *TBS* ilikuwa imetayarisha viwango 1,013 katika sekta za kilimo na chakula, nguo, kemikali, uhandisi, mazingira na sekta nyingine. *TBS* imeendelea na jukumu la kusimamia viwango kwa kutumia mifumo iliyopo. Hadi kufikia mwezi Machi 2008, *TBS* ilikuwa imetoa jumla ya leseni 837 za ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda vya hapa nchini. Aidha, jumla ya viwango 58 vya mazingira vimetayarishwa na mafunzo yametolewa kwa wamiliki wa viwanda katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira kulingana na viwango vya kimataifa yaani *ISO* 14000 *Standards*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania liliendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi 2008, TBS ilikuwa imetoa jumla ya leseni 10,506 za ubora wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Aidha, TBS inaendelea kushirikiana na mashirika ya viwango ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan Kenya na Uganda katika kuweka viwango vya Afrika Mashariki. Hadi kufikia Februari 2008, viwango 757 vya Afrika Mashariki vilikuwa vimetayarishwa katika sekta za uhandisi, chakula, nguo na kemikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, *TBS* itaendeleza jitihada za kutayarisha na kusimamia viwango ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa viwango vya huduma; kukamilisha majaribio na kuanza kutumia Kituo cha Ufungashaji; kupanua wigo wa nyanja za uthibitishwaji wa umahiri wa maabara za ugezi na chakula; kuboresha miundo mbinu yake, hususan maabara ili kukidhi mahitaji ya soko, viwanda na biashara ya ushindani. Aidha, *TBS* inakusudia kufungua vituo vya ukaguzi katika miji ya Namanga na Tunduma. Vile vile, *TBS* itakamilisha taratibu za kupima ubora wa bidhaa kabla ya kuletwa nchini Tanzania (*Pre-shipment verification of conformity to Standards*). Wizara itakamilisha kutunga sheria mpya ya viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilipanga kurekebisha Sheria ya Alama za Bidhaa (*The Merchandise Marks Act*, 1963) inayosimamiwa na Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission - FCC)* ili kuwezesha kupambana na bidhaa bandia na zisizokidhi viwango katika kuhakikisha kuwa ubora wa bidhaa unazingatiwa na haki za walaji nchini zinalindwa na kuepusha nchi yetu kuwa jalala la bidhaa bandia. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa marekebisho ya Sheria ya Alama za Biashara yamefanywa. Marekebisho hayo yamempa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya biashara kutengeneza Kanuni za Sheria ya Alama za Biashara. Kanuni za sheria hii zimekamilika na zimeanza kutumika tangu mwezi Juni 2008.

Aidha, marekebisho hayo yamewezesha kuwepo kwa Wakaguzi ambao sasa wanaweza kukagua bidhaa endapo wanazitilia shaka na kuchukua hatua muafaka ikiwa ni pamoja na kuziteketeza endapo itabainika kuwa bidhaa hizo ni bandia au zisizokidhi viwango. Katika zoezi hili, Tume inashirikisha vyombo vya habari ili kuelimisha umma kuhusu athari za bidhaa bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Ushindani imeendelea kusimamia ushindani wa haki kwa kudhibiti matumizi ya ukiritimba, uundaji wa magenge (*cartels*) na

muungano (*mergers and acquisition*) ambao unahatarisha uwepo wa ushindani wa haki katika biashara. Katika mwaka 2007/2008, Tume ya Ushindani imeidhinisha makubaliano saba (7) ya muungano. Aidha, Tume imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa mteja ambapo warsha nne (4) zimefanywa katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Ziwa (Mwanza). Katika mwaka wa 2008/2009 jitihada hizi zitaendelezwa ili kuhakikisha kuwa biashara inafanywa kwa misingi ya ushindani ulio wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, kupitia Wakala wa Vipimo na Mizani (*Weights and Measures Agency* - *WMA*), ililenga kudhibiti matumizi ya vipimo batili katika biashara hasa uingizaji wa mizani isiyofaa nchini; matumizi ya vipimo batili kama lumbesa; uuzaji wa mafuta pungufu katika vituo vya kuuzia mafuta na kuweka ujazo maalum katika malori ya mchanga na kokoto.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika mwaka 2007/2008 Wakala wa Vipimo na Mizani, imeendelea kuhamasisha matumizi ya vipimo sahihi katika biashara. Wakala imefanikiwa kukagua na kuhakiki vipimo 482,752 katika mwaka 2007/2008 ikilinganishwa na vipimo 445,907 mwaka 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 8. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa ni pamoja na pampu za kupimia mafuta 4,238. Wafanyabiashara 4,636 walipatikana na makosa chini ya Sheria ya Vipimo ambapo walitozwa faini ya jumla ya shilingi 102,457,350. Kati ya wafanyabiashara waliokiuka Sheria ya Vipimo, jumla ya wafanyabiashara 942 walipatikana na makosa yanayohusu ufungashaji wa *lumbesa* ambapo faini iliyotozwa kwa makosa hayo ilikuwa shilingi 60,637,000. Wakala imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti matumizi ya vipimo batili, hususan *lumbesa*.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mafanikio haya yametokana na ushirikiano mkubwa tulioupata kutoka katika taasisi na viongozi mbalimbali hasa Wakuu wa Mikoa na wananchi kwa ujumla. Ninawashukuru sana kwa kushirikiana na Wakala wa Vipimo na Mizani katika kukabiliana na changamoto hii. Ninatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana katika kupiga vita matumizi ya vipimo batili ili matumizi ya lumbesa na vipimo vingine batili yabaki kuwa historia katika muda mfupi ujao. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2007/2008, Serikali itaendelea na juhudi za kuelimisha umma kuhusu suala hili ili kuongeza ufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Wakala wa Vipimo na Mizani, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi sahihi ya vipimo katika biashara ikiwa ni pamoja na matanki makubwa ya mafuta, malori ya mchanga na kokoto, magari ya kubebea mafuta na pampu za kwenye vituo vya mafuta. Wizara inatarajia kukamilisha marekebisho ya Sheria za Vipimo na Mizani ili iendane na mahitaji mapya ya kibiashara, kiusalama na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usajili, Leseni na Hakimiliki. Wizara katika mwaka 2007/08 ililenga kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhusiana na

Sheria na Kanuni za Hakishiriki (*neighbouring rights*) na Hakimiliki (*Copyright*) kupitia Chama cha Hakimiliki cha Tanzania (*Copyright Society of Tannzania - COSOTA*). Katika kuboresha usajili wa shughuli za biashara, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*Business Registration and Licensing Authority - BRELA*) inaendelea kuboresha mfumo wa kusajili na kuweka kumbukumbu za makampuni na majina ya biashara kwa kutumia teknolojia za kisasa ikiwa ni pamoja na mitandao ya kompyuta. Katika mwaka 2007/2008, jumla ya makampuni 5,133 yalisajiliwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na makampuni 4,003 yaliyosajiliwa mwaka 2006/07. Aidha, jumla ya majina ya biashara 9,946 yalisajiliwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 13 ikilinganishwa na majina ya biashara 8,808 yaliyosajiliwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa Alama za Biashara (*Trade Marks),* ulipungua kwa asilimia 4 kutoka Alama 701 msimu wa 2006/2007 hadi Alama 672 katika mwaka 2007/2008. Usajili wa Alama za Huduma (*Service Marks*) nao ulipungua kwa asilimia 60 kutoka Alama 481 msimu wa 2006/2007 hadi Alama 192 msimu wa 2007/2008. Usajili wa Hataza (*patents*) uliongezeka kutoka 14 msimu wa 2006/2007 hadi kufikia 82 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 486 na usajili wa Leseni za Viwanda uliongezeka kwa asilimia 13 kutoka viwanda 77 mwaka 2006/2007 na kufikia leseni 87 msimu wa 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari mwaka 2008, *COSOTA* imesajili wanachama 81 na hivyo kufanya jumla ya wanachama wote waliosajiliwa na *COSOTA* kufikia 1,082. Kati ya hao wanamuziki ni 710; wazalishaji na wasambazaji 24 walisajiliwa. Vile vile, sanaa za maonyesho 154 zilisajiliwa. Jumla ya kazi nyingine 7,044 zimesajiliwa. Kati ya hizo, kazi za Muziki ni 6,349, sanaa za maonyesho 22 na kazi za maandishi 473. Aidha, katika mwaka wa fedha 2007/2008, *COSOTA* imekusanya mirabaha yenye jumla ya shilingi 113,275,500 kutokana na matumizi ya kazi za muziki na filamu katika mahoteli, kumbi za starehe na mabaa. Vile vile, *COSOTA* imesuluhisha jumla ya migogoro 25 inayohusiana na Hakimiliki. Utaratibu huu unasaidia wasanii ambao hawana uwezo wa kufungua kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia *BRELA* na COSOTA itaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhusu Sheria na Kanuni za Hakimiliki na Haki Shiriki kupitia *COSOTA* na masuala ya Miliki Ubunifu (*Intellectual Property Rights*) kupitia *BRELA* katika kuendeleza masuala ya ubunifu nchini; na kuendelea kusajili wanachama na kusuluhisha migogoro mbalimbali baina ya wadau wa *COSOTA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti na maendeleo ya teknolojia. Katika mwaka 2007/2008, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti na maendeleo ya teknolojia ilipanga kuendeleza ubunifu na kuhawilisha teknolojia ambazo zitaongeza ufanisi katika shughuli za uzalishaji, usindikaji na ufungashaji, hususan mazao ya kilimo, mifugo, misitu, samaki na madini. Aidha, Wizara ilidhamiria kujenga uwezo wa wajasiriamali kwa kuendeleza programu za viatamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza ubunifu wa teknolojia nchini, Wizara kwa kupitia *CAMARTEC* imekamilisha utengenezaji wa trekta ndogo, na imekamilisha kwa asilimia 50 uundaji wa gari la magurudumu matatu na kutengeneza mashine ya kuchambua mbegu za nyanya. Aidha, katika mwaka 2007/2008 taasisi hiyo imeshirikiana na wadau wengine kubuni na kueneza matumizi ya teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na teknolojia za kusindika matunda, mbegu na vyakula, na kueneza matumizi ya nishati mbadala zitokanazo na kinyesi cha wanyama (*biogas*). Katika mwaka 2007 wakulima na wajasiriamali 29 walishiriki katika maonesho mbalimbali ikilinganishwa na 17 walioshiriki katika mwaka 2006/2007 ili kuonyesha zana na teknolojia za kilimo kwa wakulima na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo *TEMDO*, limeendelea na majukumu yake makuu ya kubuni, kuunda na kuhamasisha utengenezaji na matumizi ya mashine na teknolojia mbalimbali katika uzalishaji mali, uongezaji thamani katika bidhaa pamoja na uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati. Teknolojia hizo ni pamoja na zile za kutengeneza mkaa unaotokana na mabaki ya mimea na hivyo kuhifadhi mazingira; usindikaji wa matunda na asali; usindikaji wa maziwa kibiashara; na uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za upepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza viatamizi vya teknolojia na biashara, *TEMDO* imewezesha wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza miradi ya kutengeneza mkaa kutokana na vumbi la mkaa, kutengeneza vifaa vya mashuleni kama chaki, kusindika matunda na vyakula, nk. Vile vile, *TEMDO* imeendelea kutoa huduma za kihandisi katika viwanda vikubwa na vidogo kwa nia ya kuongeza tija katika uzalishaji mali. *TEMDO* imetoa ushauri na mafunzo katika viwanda vya *Tanzania Breweries Limited*, *Tanganyika Planting Company Limited*, *Kilombero Sugar Company*, *Mbeya Cement Company Ltd na Sunkist Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*), limeendelea kubuni na kufanya tafiti zenye lengo la kuboresha ufanisi katika sekta za uzalishaji viwandani na pia kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo. *TIRDO* inaendelea kuimarisha maabara za chakula na bioteknolojia; nishati na mazingira; bidhaa za kilimo na kemia ya viwanda; na maabara ya uchunguzi wa vyuma ili ziweze kupata kutambulika kimataifa. Tayari maabara mbili kati ya hizo nne zimeshafanyiwa tathmini za awali na shirika linalotambulika kimataifa katika usimamizi wa viwango (*South African National Accreditation Systems* - *SANAS*).

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kutokana na mahitaji ya watumiaji wa mazao na bidhaa mbalimbali zinazouzwa katika masoko, hususan ya nchi za nje kuhitaji taarifa kuhusu mchakato mzima kutoka uzalishaji hadi inapomfikia mtumiaji (*traceability*), imekuwa ni lazima kujenga uwezo wa wazalishaji katika kufanya ufuatiliaji huo na kuweka kumbukumbu husika. Kama hatua ya mwanzo, mfumo wa ufuatiliaji wa mazao toka shambani, viwandani hadi kwa mlaji umeanzishwa na *TIRDO* kwa lengo la kuhakikisha ubora na kuweka kumbukumbu kwa mazao ya nyama na asali. Wadau wa nyama wapatao 122 huko Mpwapwa, Mvomero na Kilosa walipewa mafunzo kuhusu mfumo huu. Katika zao la asali, wajasiriamali wapatao 373 walihamasishwa na kupewa

mafunzo huko Kondoa, Handeni na katika mikoa ya Rukwa na Mbeya. Aidha, Shirika limetoa mafunzo ya mfumo huo kwa viongozi waandamizi 90 wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Vile vile, mfumo huu wa ufuatiliaji umeanza kutumika katika usindikaji wa samaki na mazao ya kahawa, chai, maua na mboga kwa ajili ya mauzo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TIRDO*, imeanza mchakato wa kuanzisha mfumo wa utambuzi wa bidhaa kwa kutumia kompyuta (*bar code system*). Utambuzi huu utawezesha bidhaa zitakazoingizwa katika mfumo wa ufuatiliaji kuuzwa katika maduka ya *super market* yaliyoko nchini na pia kuwarahisishia wafanyabiashara wa Tanzania ambao hivi sasa hulazimika kutumia mfumo wa utambuzi wa nchi nyingine wanapouza bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, iko katika hatua mbalimbali za kupitia upya sheria zilizoanzisha mashirika na taasisi za utafiti na maendeleo ya teknolojia zilizopo chini ya Wizara ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kulingana na mazingira mapya ya kiuchumi na kibiashara. Katika mwaka 2008/2009, taasisi hizi zitaendelea kufanya utafiti na kubuni teknolojia zenye lengo la kusaidia katika maendeleo ya sekta ya viwanda, biashara na masoko na sekta nyingine za uchumi kwa ujumla. Aidha, *CAMARTEC* itaendelea kuhamishia shughuli zake na kujipanga upya katika eneo la *TANADE* ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. *TIRDO* itakamilisha taratibu za kuboresha maabara zake ili ziweze kukidhi viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya rasilimali watu. Wizara ina jumla ya watumishi 219 ikilinganishwa na ikama ya watumishi 244. Kati yao, watumishi 131 ni wanaume na 88 ni wanawake. Wizara imeendelea kujaza nafasi mbalimbali hatua kwa hatua kulingana na ikama na kwa kuzingatia masuala ya jinsia. Katika mwaka 2007/08, Wizara imeajiri watumishi 29 katika fani mbalimbali. Aidha, nafasi 4 kati ya nafasi 5 za ajira katika ngazi ya uongozi zimejazwa. Wizara inatarajia kuajiri watumishi 24 katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ilipanga kusomesha watumishi katika taaluma mbalimbali kulingana na mpango wa mafunzo wa Wizara. Jumla ya watumishi 25 walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mrefu na watumishi 19 walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kukidhi matakwa na mahitaji ya wataalam kiujuzi. Wizara itaendelea kuajiri, kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa watumishi wake katika mwaka wa fedha 2008/2009 kulingana na mpango wa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza pengo lililopo katika idadi ya wataalam wa kada ya kati ambao ni kiungo muhimu kitaaluma, Wizara kwa kushirikiana na Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeanza kuandaa mpango wa kurithishana (*succession planning*) ili kuweza kubaini mahitaji ya aina ya taaluma zinazohitajika, ujuzi na aina ya sifa zinazotakiwa ili kuziba mapengo pale yanapotokea. Aidha, Wizara imeandaa mfumo wa benki ya takwimu (*data base*) ya watumishi ili kuwa na mfumo wa

taarifa za watumishi unaowezesha kupata taarifa hizo haraka (*retrievable*) kwa matumizi ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mtambuka, kudhibiti rushwa. Katika juhudi za kupambana na rushwa na kuboresha utoaji wa huduma, Wizara na Taasisi zake iliendelea kutoa elimu ya huduma kwa mteja kwa watumishi wake ili kuweza kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa. Kamati za Maadili katika ngazi za Wizara na Taasisi ziliundwa sambamba na Kamati ya Kuratibu Malalamiko na Kero za Wateja wa Ndani na Nje ya Wizara. Juhudi hizi zitaendelezwa kwa mwaka 2008/2009. Ili kufuatilia vitendo viovu vya rushwa, mifumo na utaratibu wa kazi unahimiza uadilifu, uwazi na kupunguza urasimu usio wa lazima. Rushwa inaathiri tija na ufanisi, ari ya kazi na hunyima haki. Rushwa ni gharama kubwa isiyoweza kufidiwa. Hivyo, Wizara itaendelea kupiga vita rushwa ili kudumisha maelewano na amani mahala pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, janga la UKIMWI, katika juhudi za kupambana na janga la UKIMWI, katika mwaka 2007/2008 Wizara imetoa mafunzo kwa Waelimishajirika/Waelimishajiwenza wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ili kujenga uwezo wao katika kutoa elimu kwa watumishi wenzao kulingana na rika na kuhamasisha kujitokeza kupima kwa hiari. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa Waratibu 48 wa masuala ya UKIMWI wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ili waweze kuratibu shughuli hizo kwa ufanisi zaidi katika sehemu zao za kazi. Vile vile, Wizara iliwezesha utoaji wa mafunzo nje ya nchi kwa waratibu wa masuala ya UKIMWI sehemu za kazi ili kuweza kupata uzoefu wa wadau wengine juu ya masuala ya maambukizi ya UKIMWI na hivyo kuboresha mpango wa Wizara katika kutekeleza programu ya masuala ya UKIMWI sehemu ya kazi. Pia, Wizara inatathmini Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za UKIMWI zisizohusiana na Tiba (TOMSHA) ili kuwa na mpango wa utoaji huduma ya lishe na madawa kwa wafanyakazi walioathirika. Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, virutubisho (*food supplements)* na usafiri kwa watumishi wenye virusi vya ukimwi. Wizara inaihamasisha jamii ya wenye viwanda na biashara nyingine kujali afya za wafanyakazi likiwemo suala la ukimwi mahala pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake pamoja na wadau wengine inahamasisha matumizi ya teknolojia zisizoharibu mazingira kama vile biogas, bio-latrine, nishati za mionzi ya jua na matumizi ya mkaa unaotokana na mabaki ya mimea. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kukamilisha mfumo wa uperembaji (*monitoring and evaluation system*) wa programu mbalimbali zinazotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayohusiana na hifadhi na utunzaji wa mazingira katika shughuli za uzalishaji viwandani. Wizara ilitoa elimu na kuwahamasisha wenye viwanda kutumia nishati mbadala ikiwemo gesi asilia ili kupunguza ongezeko la ukataji na utumiaji wa kuni kama nishati viwandani pamoja na utumiaji wa mafuta ambayo huzalisha gesi ya *carbon dioxide* kwa wingi na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mabadiliko ya kasi kubwa ya tabianchi. Aidha, kutokana na ongezeko la shughuli za ujenzi, Wizara imeendelea kuwahamasisha wenye viwanda

hususan viwanda vya chuma kutengeneza nguzo za chuma ambazo zinatumika katika ujenzi badala ya miti (mirunda) inayokatwa kwa wingi na hivyo kutishia hifadhi ya misitu. Hivi sasa kuna viwanda vitatu (3) vinavyotengeneza nguzo za chuma kwa ajili ya shughuli za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara ilishiriki katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda mkoani Morogoro. Shughuli hiyo inayosimamiwa na Bonde la Wami/Ruvu ambapo mkakati wa kuwa na mfumo wa pamoja wa kukusanya na kusafisha majitaka toka viwandani umeandaliwa. Utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha. Hali kadhalika, katika kipindi cha mwaka 2007/08, Wizara imeanzisha Dawati la Mratibu wa Mazingira (*Sector Environmental Coordinator* – SEC), ili kuratibu kikamilifu shughuli za mazingira katika sekta ya viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imejipanga kushughulikia uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda vya kusindika ngozi ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa sana na wananchi kuwa shughuli zao zinachafua mazingira. Wenye viwanda hivyo watahamasishwa kujenga mfumo mzuri pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa kukusanya majitaka na kuyasafisha ipasavyo ili yasiendelee kuwa kero kwa wananchi pamoja na kuleta madhara ya kimazingira. Vile vile, Wizara itaendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wadau mbalimbali katika sekta ya viwanda, biashara na masoko kuhusu Sheria ya Mazingira na Kanuni za utekelezaji wake ambao umeshaanza ili wazielewe na kuzizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto, mojawapo ya changamoto kubwa zinazoikabili nchi yetu wakati huu ni mfumko mkubwa wa bei za bidhaa mbalimbali, hususan bidhaa za ujenzi na chakula. Ongezeko hili kubwa limepelekea maisha kuwa magumu na hata kuwapelekea wananchi kulalamika mitaani, katika vyombo vya habari na hata kwa kupitia kwa wawakilishi wao hapa Bungeni, yaani Waheshimiwa Wabunge. Ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu na kupitia kwa Bunge hili kuwataarifu wananchi kuwa ongezeko hili kubwa la bei za bidhaa linatokana na kuongezeka ghafla kwa bei ya mafuta duniani. Kwa vile uzalishaji wa bidhaa muhimu hapa nchini kama saruji, mabati na sukari hutegemea nishati ya mafuta, kuongezeka kwa bei ya mafuta kumesababisha gharama za uzalishaji wa bidhaa hizi kuongezeka, na hivyo bei zake katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili linaiathiri Tanzania kwa kiwango kikubwa kwa sababu nchi yetu haizalishi mafuta, na wala haina uwezo wa kuzishawishi nchi zinazozalisha mafuta kupunguza bei hiyo. Ongezeko la bei za mafuta pia limesababisha kuongezeka kwa matumizi ya nafaka kama chanzo cha nishati duniani, hivyo kupunguza kiasi cha nafaka inayotumika kwa chakula na kusababisha bei ya chakula kwa jumla kupanda. Sababu nyingine iliyosababisha ongezeko la bei ya chakula duniani ni hulka ya wafanyabiashara wa chakula kutabiri ongezeko kubwa zaidi (*speculation*) la matumizi ya nafaka kama chanzo cha nishati, hivyo kuwa tayari kununua nafaka kwa bei kubwa zaidi ya ile ambayo ingetumika bila kuwepo utabiri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ya kupanda kwa ghafla kwa bei za bidhaa, hasa saruji na mabati, ni ongezeko la mahitaji ya ujenzi duniani, Tanzania ikiwemo. Kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizi, sambamba na kuongezeka kwa bei ya mafuta duniani, kumekuwa sababu ya bei za saruji na mabati hapa nchini kuongezeka kwa kasi. Hali hii imechangiwa pia na wazaIishaji wa bidhaa hizi kupendelea kuziuza nje ya Tanzania wanakopata bei nzuri zaidi, hivyo kusababisha uhaba nchini na kuifanya bei ipande hadi kuikaribia au kulingana na bei inayotawala katika masoko ya nchi majirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba sababu hizi kwa kiasi kikubwa ni nje ya uwezo wetu kama nchi, ningependa kuitumia fursa hii adimu kuwahimiza wananchi wote watambue kuwa njia mojawapo ya kupunguza makali ya maisha yanayotokana na ongezeko kubwa la bei hizi ni kwa sisi Watanzania kuzalisha zaidi mazao ambayo nchi yetu imejaliwa upendeleo wa kuyazalisha na ambayo hayahitaji kuzalishwa kwa kutumia nishati nyingi ya mafuta, hususan mazao ya kilimo. Tukizingatia kuwa nimeainisha katika hotuba hii kwamba bei za mazao ya chakula zimepanda na zitaendelea kupanda, ongezeko la uzalishaji wa mazao haya utalisaidia Taifa kupunguza makali ya bei za mafuta kutokana na mapato makubwa tutakayopata kwa kuuza mazao yetu ya kilimo. Vile vile, nawahimiza wananchi wote, hususan wakulima, tuimarishe ushirika ili kuepuka kugawana faida ya mazao yetu na wafanyabiashara wa kati bila ulazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia jitihada hizi za kupunguza makali ya mfumko wa bei, Wizara yangu itaendelea na jitihada za kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ili mfumo huu hatimaye uweze kutumika nchi nzima na kuwawezesha wakulima kupata malipo stahili ya mazao yao badala ya kuyauza mazao hayo kwa bei rahisi mara wanapovuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bidhaa muhimu hasa zile za ujenzi, Wizara yangu imezuia uuzaji wa bidhaa hizi nje na kutoa vibali maalum kwa wafanyabiashara kuingiza bidhaa hizo kwa upendeleo wa kusamehewa kodi ya ziada inayolipwa endapo bidhaa hizo zinaagizwa nje ya Soko la Forodha 1a Afrika Mashariki. Maamuzi haya yalilenga katika kuzifanya bidhaa hizi ziwepo kwa wingi katika soko letu na hivyo kupunguza bei zake. Wizara pia imezielekeza menejimenti za viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo hapa nchini, hususan saruji na mabati, kuuza bidhaa hizo kwa utaratibu wa kutenga maeneo maalum (*depots*) na kuyatumia kuuzia bidhaa hizo katika kanda zote nchini ili bei ya bidhaa hizo isitofautiane sana kati ya eneo moja la nchi na eneo lingine. Utaratibu huu pia utapunguza matumizi ya wafanyabiashara wa kati, ambao kimsingi huongeza bei i1i kujipatia faida kubwa huku wakiwabebesha walaji mzigo mzito wa kununua bidhaa hizo kwa bei za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia itaendelea kutumia taasisi zake za usimamizi wa ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa kuhakikisha kuwa vitendo vya ukiritimba, uundaji wa magenge ya biashara au muungano wa kibiashara unaosababisha kuongeza bei ya bidhaa kwa mlaji vinaendelea kupigwa vita hadi kutokomezwa kabisa. Ni matumaini yangu kuwa jitihada hizi zinazofanywa na Serikali zitawasaidia wananchi

kukabiliana na mfumko huu wa bei, ila nisisitize hapa kuwa ili jitihada hizi zifanikiwe zinahitaji kuungwa mkono na kila mdau na kila mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo Wizara yangu inakabiliana nayo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ambao unaifanya Wizara ishindwe kutekeleza mpango kazi na wajibu wake na hivyo kutofikia malengo ya kuwa sekta kiongozi kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2005. Changamoto nyingine ni uhaba wa utaalamu katika sekta, uhaba na upatikanaji usio wa uhakika wa nishati na maji, miundombinu duni ikiwemo ya usafiri, masoko na uhifadhi, uzalishaji bidhaa na huduma zisizokidhi viwango vya kimataifa, na vikwazo vya kibiashara hasa kuhusiana na viwango vya ubora na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia bajeti na rasilimali watu katika Wizara yangu, Wizara imejipanga kupambana na changamoto hizo kwa kutumia mikakati mbalimbali kama ilivyoanishwa katika hotuba yangu. Mikakati hii ni pamoja na Mkakati ya Kukuza Uzalishaji na Kukuza Mauzo Nje wenye kulenga matokeo ya haraka; Mkakati Unganishi wa Biashara, Mkakati Unganishi wa Kuendeleza Viwanda; na Mfumo Unganishi wa Kukusanya na Kusambaza Taarifa. Hata hivyo, mafanikio yanategemea sana juhudi za pamoja za wadau mbalimbali ili kuweza kupambana na changamoto hizi kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya viwanda  hayana budi kwenda sanjari na biashara imara ya ndani, ya kikanda na ya kimataifa. Hata hivyo, miundombinu muhimu ikiwa ni pamoja na barabara, reli, bandari, miundombinu ya masoko na miundombinu ya uhifadhi ni muhimu sana. Uendelezaji wa miundombinu hii unahitaji juhudi za pamoja kati ya Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi. Hivyo, natoa rai kwa wadau wote tushirikiane kupambana na changamoto hizi. Aidha, utayari wa sekta binafsi kuzitumia fursa zitokanazo na juhudi hizi ni muhimu sana. Hivyo, natoa rai vilevile kwa wanaviwanda na wafanyabiashara kuzitumia kikamilifu fursa zitokanazo na mikakati hii na juhudi hizi ili kwa pamoja tuweze kuendeleza viwanda, biashara na masoko. Kwa kufanya hivyo, tutaiwezesha sekta ya viwanda kuwa sekta kiongozi na kutimiza malengo ya Dira ya Mendeleo ya 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya kuiwezesha Tanzania kuongozwa na uchumi wa viwanda vya kati na mauzo nje *(semi-industrialized export led economy),* ili kuwaletea Watanzania maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia napenda kunukuu maneno ya Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifungua rasmi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Desemba 2005. Mwanzo wa kunukuu "…Uchumi wa nchi yoyote iliyoendelea ulianza na kilimo na kisha kuwa wa viwanda. Nasi hatuna budi kuelekeza nguvu na kuweka mkakati maalum katika kukuza na kuendeleza viwanda nchini. Viwanda-vikubwa, vidogo na vya kati-vina uwezo mkubwa wa kutoa nafasi za ajira, lakini vilevile vinasaidia kusindika mazao ya kilimo, kuyaongezea thamani na kuzuia yasiharibike wakati wa mavuno. Serikali ya Awamu ya Nne itatengeneza mkakati kabambe wa kutekeleza sera ya viwanda nchini. Wakati huo huo, Serikali itajitahidi kuwawezesha wazalishaji wadogo na wa kati kuongeza mitaji yao, kuingiza nchini teknolojia bora zaidi na kuwawezesha kufikisha bidhaa zao kwenye

masoko" mwisho wa kunukuu. Wakati umefika wa nchi hii kuacha kuwa *super market* ya bidhaa za nje na kuwa nchi ya viwanda yenye kujitegemea, kujitosheleza na iliyo huru kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, napenda kumalizia kwa kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa misaada kupitia Serikali yetu ambayo iliiongezea Wizara uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi. Nchi hizo ni Afrika Kusini, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, Ireland, Uswisi, India, Japan, Marekani, Sweden, Uholanzi, Uingereza na Ujerumani. Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika ya SIDA, UNIDO, DANIDA, DFID, GTZ, ILO, IFAD, NORAD, WTO, UNCTAD, OECD, USAID, UNDP, OPEC Fund, JICA, WIPO, ARIPO, SECO, IMF na ITC. Pia, napenda kuzishukuru Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na CFC kwa misaada na michango yao ya fedha na ya kitaalamu katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2008/2009. Matumizi ya Kawaida. Wizara na taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya shilingi 16,847,002,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili iweze kutekeleza majukumu niliyoelezea ya kuendeleza sekta za viwanda, biashara na masoko kwa mwaka wa fedha ujao wa 2008/2009. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,848,493,000 ni kwa matumizi ya mishahara na shilingi 7,998,509,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*OC*) ya Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Maendeleo. Wizara inaomba jumla ya shilingi 31,262,134,600 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo katika Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha majedwali mbalimbali ambayo yanatoa takwimu zitakazowawezesha Waheshimiwa Wabunge kutafakari vizuri maendeleo katika sekta za viwanda, biashara na masoko. Naomba takwimu hizo zichukuliwe kama vielelezo zaidi vya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru kwa hotuba yako, umeiba muda wa watu sasa. Kama mnavyoona, Waziri mwenyewe kapendeza, ndiyo vitenge vya Tanzania na kwa sababu hiyo, nimemuongezea dakika moja. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia hotuba hii, Mheshimiwa Mwenyekiti mwenyewe!

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na. 99(7), Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha maoni haya. Kabla sijawasilisha maoni ya Kamati, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila, kama sitaishukuru familia yangu inayonipa faraja, furaha na kila msaada katika kazi yangu ya siasa. Pia nawashukuru Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Makunduchi kwa imani waliyonayo kwangu mimi. *(Makofi)*

Kwa namna ya pekee, nitoe shukrani zangu za dhati, kwa wanakamati kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao kwa sauti moja. Nawashukuru sana kwa imani yao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mara ya kwanza kwa Kamati yangu kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati hii mpya, imepewa jukumu la kusimamia majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kabla ya marekebisho makubwa ya Kanuni za Bunge 2007, ambayo ndiyo yaliyoleta kuundwa kwa Kamati hii, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ilikuwa inasimamiwa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambayo ilifanya kazi nzuri chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu, ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hiyo, Wajumbe walielezwa kuhusu mambo yafuatayo:-

1. Dira na Mwelekeo wa Wizara;

2. Muundo wa Wizara;

3. Majukumu ya Wizara;

4. Maelezo kuhusu Taasisi zilizo chini ya Wizara;

5. Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2007/2008; na

6. Maombi ya Fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa kwa Wizara kwa mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa Fedha uliopita, Kamati ya Uwekezaji na Biashara (ya wakati huo) ilitoa Maoni, ushauri na maagizo14. Napenda kuishukuru Serikali kwa kutekeleza kwa kiasi kikubwa maagizo karibu yote. Hata hivyo, kuna maagizo machache, kwa mfano maeneo ya *General Tyre*, Taasisi za Utafiti na Maendeleo, Madini ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma na *SIDO* ambayo Kamati itaendelea kuagiza Serikali, kuongeza juhudi katika kutekeleza maagizo 20 husika, kama itakavyoshauriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa mwaka wa Fedha 2007/2008, Wizara iliidhinishiwa na Bunge, bajeti ya Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Mia Sita Ishirini na Tisa, Laki Tisa na Ishirini na Tatu Elfu (24,629,923,000/=).

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika utekelezaji wa malengo na bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008. Katika kutekeleza malengo ya mwaka wa Fedha 2007/2008, Kamati ilielezwa kuwa Wizara imekuwa ikikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Ufinyu wa Bajeti;

2. Uhaba wa wataalam katika Sekta ya biashara ili kukidhi mahitaji ya kibiashara ya Karne ya 21;

3. Uhaba na upatikanaji usio wa uhakika wa umeme na maji, ambao unasababisha gharama kuwa kubwa katika uzalishaji;

4. Miundombinu duni, na

5. Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa na utoaji huduma zisizokidhi viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na mikakati ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Wajumbe walielezwa kuwa katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Sekta ya Viwanda

(i) Kukamilisha Uundaji wa Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa kuendeleza sekta ya viwanda nchini;

(ii) Kukamilisha uwekezaji kwenye miundombinu muhimu katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuendeleza viwanda na biashara ikiwa ni pamoja na maeneo ya *EPZ* na *SEZ*;

(iii) Kuendeleza zoezi la kubainisha maeneo ya *EPZ* katika Mikoa iliyobaki na kufanya taratibu za kumiliki maeneo yaliyokwisha kubainishwa;

(iv) Kukamilisha zoezi la uwekezaji katika miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na ya Chuma ya Liganga pamoja na miundombinu;

(v) Kutekeleza mpango mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta ya Viwanda vya Ngozi;

(vi) Kukamilisha uundaji wa Sheria ya Chuma Chakavu;

(vii) Kuimarisha taasisi za Utafiti na Maendeleo;

(viii) Kufanya tathmini ya maendeleo ya viwanda na kuendelea na zoezi la kuperemba viwanda vilivyobinafsishwa;

(ix) Kuibua na kuendeleza Viwanda Mama na Mashirika makubwa ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na usindikaji wa mazao na ufufuaji wa viwanda mbalimbali.

2. Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo

(i) Kukamilisha maandalizi ya *Baseline Survey* ya viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo, ili kuandaa Benki ya Takwimu ya viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo;

(ii) Kuandaa mkakati wa kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa Wajasiriamali wadogo nchini;

(iii) Kuhamasisha uendelezaji wa ubunifu na usambazaji wa teknolojia muafaka kama vile mitambo ya uchimbaji mdogo wa madini, zana za kusindika mazao ya kilimo, vifaa vya ujenzi, teknolojia ya kupunguza matumizi ya kuni na makaa na kujengwa Vituo vya Biashara kwa ajili ya Wajasiriamali wadogo;

(iv) Kuendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo Vijijini (Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini – MUVI).

3. Sekta ya Biashara na Masoko

(i) Kuendeleza uhusiano wa kibiashara na uwekezaji na China na nchi nyingine za Asia na Mashariki ya Kati;

(ii) Kutekeleza Mpango Unganishi wa Biashara *(Tanzania Trade Integration Strategy - TTIS)*;

(iii) Kuendeleza maandalizi ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Kukuza Mauzo Nje kwa Kubainisha Maeneo Yatayoleta Matokeo ya Haraka *(Quick Wins)*;

(iv) Kuendelea kujihusisha na utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuingia katika Soko la Pamoja;

(v) Kukamilisha taratibu za kuingia Eneo Huru la Kibiashara katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC);*

(vi) Kukamilisha majadiliano ya Ubia wa Uchumi na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(Economic Partnership Agreement – EPA);*

(vii) Kuendelea kuelimisha umma katika nyanja ya biashara na masoko;

(viii) Kukamilisha Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo;

(ix) Kuandaa Mkakati wa Kutekeleza Sera ya Masoko ya Mazao, na kuisambaza kwa umma;

(x) Kuelimisha Umma juu ya fursa za masoko;

(xi) Kuendeleza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Masoko ya Kimataifa *(Integrated International Markets)* ya mazao ya kilimo;

(xii) Kujenga Mfumo wa Mawasiliano wa Ukusanyaji, Uchambuzi na Usambazaji wa Taarifa na Takwimu utakaounganisha Wadau mbalimbali ndani na nje *(Global Electronic Data Interchange Network);*

(xiii) Kuvutia wawekezaji ili kuanzisha miji/vituo vya kibiashara *(Trade Hubs)*; na

(xiv) Kuanzisha Mji wa Kisasa na Kituo cha kwanza cha Kibiashara *(Satellite Town and Trade Hub)* – Bagamoyo kitakachojumuisha Bandari ya Kisasa, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa na Mji wa Biashara wa Kisasa.

4. Udhibiti wa Ushindani, Ubora wa Bidhaa na Huduma

(i) Kukamilisha Kituo cha Ufungishaji kilichopo *TBS*;

(ii) Kuendelea kuboresha maabara za *TIRDO*;

(iii) Kutayarisha mkakati wa kukagua bidhaa kabla hazijaingia nchini *(Pre-verification of Conformity to Standards);*

(iv) Kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhusiana na Sheria na Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki na masuala ya "*Intellectual Property Rights*" katika kuendeleza masuala ya ubunifu nchini; na

(v) Kuendelea kusajili wanachama wa kusuluhisha migogoro baina ya Wadau na Chama cha Haki Miliki (*COSOTA*).

5. Utafiti na Maendeleo

Taasisi za Utafiti kama Shirika la Utafiti na Uendelezaji Viwanda (*TIRDO*), Shirika la Uendelezaji na Utafiti wa Viwanda (*TEMDO*), Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (*CARMATEC*), zitaendelea kufanya utafiti na kubuni teknolojia zenye lengo la kusaidia katika sekta ya maendeleo ya sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko na sekta nyingine za uchumi kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kurekebisha Sheria zilizoanzisha taasisi hizo za teknolojia na nyingine zilizo chini ya Wizara kama – Chuo Cha Elimu ya Biashara (*CBE*) na Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*), Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) na Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2008/2009. Baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka uliopita, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu (Mb.), Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko aliwasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Makadirio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, inaomba jumla ya Shilingi Bilioni Arobaini na Nane, Milioni Mia Moja na Tisa, Laki Moja Thelathini na Sita Elfu na Mia Sita (Tsh.48,109,136,600/=). Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Nane na Arobaini na Saba na Elfu Mbili (Tsh.16,847,002,000/=) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Bilioni Thelathini na Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Mbili, Laki Moja Thelathini na Nne Elfu na Mia Sita (Tsh.31,262,134,600/=) ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Baada ya kupokea na kujadili bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Kamati yangu inatoa ushauri na maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti. Kutokana na umuhimu na majukumu mengi ya Wizara hii, bajeti iliyotengwa ni ndogo sana ambayo haiwezi kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara na taasisi zake. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele. Kutokana na ufinyu wa bajeti iliyopangwa kwa Wizara hii, inaonekana kuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko bado haijapewa kipaumbele, kinyume na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 ambayo inaitaja Sekta ya Viwanda kuwa Sekta Kiongozi na mojawapo ya Sekta za Vipaumbele katika maendeleo ya nchi, kujenga viwanda vinavyoweza kuhimili utandawazi, kujitoa katika hali ya kuwa soko la wengine *(Super Market)*, Kujivunia bidhaa zetu na kuendeleza Sekta nyingine za uzalishaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuipa Kipaumbele Wizara hii kwa kutekeleza Ilani ya Chama Tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi za Utafiti. Taasisi za Utafiti kama Shirika la Utafiti na Uendelezaji Viwanda (*TIRDO*), Shirika la uendelezaji na Utafiti wa Viwanda (*TEMDO*), Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (*CARMATEC*), ni muhimu sana kwa nchi yoyote katika kupiga hatua za maendeleo kwa sababu zinabuni teknolojia kwa maendeleo ya Viwanda, Biashara na Sekta nyingine za Uchumi kwa ujumla, mfano zana za kilimo. Hali ya baadhi ya majengo ya taasisi hizi za Utafiti hususan *TIRDO* ni mbaya sana na hivyo kutofanana na sura ya taasisi hizi. Kutokana na hali hii ya majengo, Kamati inashauri Serikali kutumia Mifuko ya Huduma za Hifadhi ya Jamii kama *NSSF* na *PPF* kuingia mikataba ya kukamilisha ujenzi na ukarabati mkubwa wa majengo haya ili Taasisi ziweze kuboresha huduma zinazostahili kutolewa. Bila kuimarisha Taasisi hizi, hatuwezi kuendeleza viwanda vinavyozalisha zana mbalimbali *(Machine Tools)* ambazo ni muhimili mkubwa wa Viwanda vya Msingi *(Basic Industries)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Uzalishaji Matairi (*General Tyre*). Kiwanda cha uzalishaji matairi *(General Tyre)*, ni moja kati ya viwanda vya msingi *(basic industry)* ambacho hakikidhi haja iliyokusudiwa katika uzalishaji. Kwa mfano, hivi karibuni kilisitisha uzalishaji na Serikali ikatoa dhamana ya shilingi bilioni Kumi (Sh.10,000,000,000/=) ili kiweze kuendelea kuzalisha lakini hakikufanya kazi kama ilivyokusudiwa na sasa kimesimamisha uzalishaji tena. Pamoja na kusimamisha uzalishaji, *General Tyre*, wanaomba tena zaidi ya shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=) kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haijaridhika kabisa na uendeshaji wa kiwanda hiki na haielewi kiwanda hiki kinapata wapi nguvu ya kuendesha shughuli zake kama kinavyojisikia wakati hisa kubwa ya kiwanda inatoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuja na fikra *(New thinking)* na mikakati mipya ya kukinusuru Kiwanda hiki kwa njia yoyote ile na kwa hili tunaamini inawezekana.

Athari za Kiwanda hiki kuendelea kufungwa ni kubwa kwa nchi yetu kwa sababu zifuatazo:-

Nchi yetu na sera zake za uchumi na uhusiano na Wawekezaji zimesifiwa ulimwenguni kote. Mfarakano huo na Wawekezaji hawa utatupunguzia sifa na heshima, ikizingatiwa kwamba tumekuwa na uhusiano mzuri kwa kipindi cha miaka 40;

Teknolojia na ujuzi walio nao Watanzania ndani ya Kiwanda hiki itakuwa ni hasara kubwa sana kwetu sisi kama kitaendelea kufungwa;

Uwezekano wa kuendeleza Kilimo cha Mpira nchini utaathirika na kupoteza ajira kwa Wakulima wetu, hususani maeneo ya Kihuhwi, Kilombero na Zanzibar;

Kiwanda kikifungwa Mitambo yake haina soko; na

Wafanyakazi zaidi ya 400 watapoteza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti wa Madini ya Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma. Kazi ya utafiti wa madini ya Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma imechukua muda mrefu. Kamati inashauri kuwa ni muhimu utafiti huo sasa uweze kukamilika kwa haraka ili uzalishaji uanze bila kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vilivyobinafsishwa kutoendeshwa kwa mujibu wa Mkataba yaani *Memorandum of Understanding* (MoU). Kamati imesikitishwa sana na taarifa ya baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa kuendeshwa kinyume na mikataba ya makubaliano na baadhi ya Viwanda kusimamisha kabisa uzalishaji baada ya kubinafsishwa, kwa mfano, Kiwanda cha Ngozi cha Morogoro, Kiwanda cha Chuma Tanga na Kiwanda cha Mbao cha Mkata. Kamati inaishauri Serikali, kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kufanya utafiti wa viwanda vinavyoendesha uzalishaji kinyume na makubaliano na kuleta orodha hiyo Bungeni pamoja na mapendekezo ya kisheria ambayo yanastahili kuchukuliwa dhidi ya wawekezaji hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wamachinga wana mchango mkubwa sana katika uchumi wa Taifa letu, lakini bado Serikali haijawapa ushirikiano wa kutosha katika kushughulikia masuala/matatizo yao. Serikali haiwapi ushauri, haiwathamini kama inavyowathamini Wawekezaji Wakubwa wa ndani na nje, wanabomolewa vibanda vyao bila kuzingatia taratibu, hawana Baba wala Mama.

Aidha, Kamati imesikitishwa sana na watu wanaokuja kama wawekezaji kutoka nje ya nchi, lakini wakifika nchini wanafanya biashara ya umachinga badala ya kuwekeza katika viwanda. Kwa mfano ukipita Kariakoo utakuta wamejaa wamachinga wa Kichina na Kikorea, wakati vijana wetu wa Kitanzania hawana pa kufanyia biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

Umefika wakati kwa Serikali kutambua mchango wa Wamachinga katika uchumi wa nchi yetu na hivyo iweke utaratibu mzuri wa kushughulikia matatizo yao;

Iwepo Wizara mahsusi ili kushughulikia masuala yao ikiwa ni pamoja na uundaji wa Vituo vya Habari na Ushauri wa Biashara (*Business Information Centre);*

Kuanzisha Jumuiya zao za Kisheria;

Kudhibiti na kuwaondoa wamachinga waliojaa Kariakoo ambao ni wageni kutoka nje na kuwabana wafanye shughuli za uwekezaji katika viwanda na siyo umachinga; na

Kuwa makini katika utoaji wa vibali vya wageni wanaoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu sasa ina dhamira siyo tu kutembelea Taasisi na Makampuni makubwa, bali pia Wamachinga na magulio kubaini matatizo yao na jinsi ambavyo tunaweza kuwahudumia vema kupitia Bunge lako Tukufu kwa kushirikiana na Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu ni muhimu sana na una faida kubwa sana kwa Wananchi wakiutumia katika kuuza mazao yao. Mfano wakulima wa korosho Mtwara wamepata faida kubwa sana baada ya kutumia mfumo huu mwaka jana. Changamoto ya mfumo huu ni kwamba bado haujafahamika kwa wadau wengi na bajeti iliyopangwa kwa ajili ya Baraza la Mfumo huu ni ndogo sana. Kielelezo ni kwamba waliomba Shilingi Milioni Mia Tatu (Tsh.300,000,000/=) lakini wamepewa Shilingi Milioni Hamsini tu (50,000,000/=). Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Baraza la Mfumo huu wa Stakabadhi ili liweze kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wadau wote kuhusu utaratibu mzuri na faida ya mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote ile, hasa nchi zinazoendelea, unategemea sana viwanda vidogo. Lakini bado nchi yetu haijatoa kipaumbele katika kuviendeleza viwanda vidogo na hii inadhihirika kupitia bajeti ndogo iliyotengwa kwa ajili ya viwanda hivi. Mfano *SIDO* iliomba Shilingi Bilioni Tano (Tsh.5,000,000,000/=), lakini imepatiwa Bilioni Moja (Tsh.1,000,000,000/=) tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hiki cha fedha hakionyeshi nia ya dhati ya Serikali ya kutaka kujikomboa kiuchumi kupitia Viwanda hivi. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea *SIDO* bajeti kwani ndio eneo mojawapo ambalo wajasiriamali wadogo wanalitegemea ili kujikwamua na umasikini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hili limekabidhiwa majukumu mengi, likiwemo la kuibua miradi mikubwa. Inasikitisha sana kuona kuwa pamoja na kukabidhiwa majukumu hayo, *NDC* ambayo iliomba Shilingi Bilioni Mbili, Mia Tatu Milioni (Sh.2,300,000,000/=), imetengewa Shilingi Milioni Mia Moja Sabini na Tano

(Sh.175,000,000/=) katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2008/2009. Kamati haikuelewa ni kwa vipi *NDC* itatekeleza miradi hiyo mikubwa kwa mgao huo mdogo. Kamati inaishauri Serikali, kulipatia Shirika la Maendeleo la Taifa kiasi cha fedha kilichoombwa ili liweze kutekeleza jukukmu lake la kuanzisha na kusimamia miradi mikubwa. Aidha Kamati imeitaka *NDC* kupitia Wizara kufafanua majukumu yake ya kiuchumi kulingana na mazingira mapya ya kiuchumi na kuandaa sheria mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za mikopo ya Mheshimiwa Rais Kikwete. Kamati inaipongeza Serikali kwa mpango wake mzuri wa kuanzisha mikopo maarufu kwa jina la Mabilioni ya Kikwete kwa lengo la kuwezesha wananchi kiuchumi na kuboresha maisha ya Mtanzania. Hata hivyo, imeonekana kwamba mikopo hiyo haijawafikia wala kuwafaidisha walengwa wanyonge. Kinachosikitisha zaidi ni Benki zilizopewa majukumu ya kutoa mikopo kukaidi kutoa taarifa ya fedha walizotoa kwa watu au vikundi gani. Kamati inashauri Mfumo uliotumika katika kutoa mikopo hiyo ubadilishwe ili fedha hizo ziweze kuwafikia walengwa. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa *SIDO*, kutokana na uzoefu wake mkubwa wa miaka mingi, iwe miongoni mwa taasisi za kwanza ambazo zinakabidhiwa jukumu la kuhudumia katika taasisi za fedha zinazopitishiwa mikopo hii.

Mheshiwa Spika, Maonesho ya 32 ya Biashara Kimataifa Dar es Salaam *(DITF)*.Kamati yangu ilipata mwaliko wa kutembelea maonesho haya ili kuona na kujifunza shughuli mbalimbali katika sekta hii ya biashara na taasisi mbalimbali. Katika kuyatembelea mabanda yapatayo 40, Kamati ilibaini mambo mengi miongoni mwa hayo, ni uwezo walionao Watanzania katika utengenezji wa bidhaa muhimu, mfano vifaa vya maabara na mizani zenye ubora kwa mujibu wa Wakala wa Vipimo lakini, wakikwamishwa na uwezo wao mdogo kifedha. Aidha, Kamati ilipotembelea Vituo vya Biashara vya London na Dubai katika banda la Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, ilifahamishwa kuwa kuna soko kubwa sana katika nchi za Dubai na Falme za Kiarabu kwa bidhaa za kilimo na hasa matunda. Lakini kwa bahati mbaya Tanzania ina uwezo mdogo kwa maana ya kukidhi haja ya soko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wafanyabishara wa nchi hizo walituambia wako tayari kuwasaidia wakulima wetu katika sekta hii ya kilimo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kuwawezesha wafanyabiashara hao kukutana na wakulima wetu ili waweze kutekeleza azma hiyo. Aidha, ni wakati muafaka sasa kuendelea na kuzalisha bidhaa ambazo Watanzaniawenye uwezo wa kuzizalisha badala ya kuagiza kutoka nje kwa kuwawezesha watu hawa kifedha ili wazalishe bidhaa hizo na hivyo kuongeza ajira na kipato cha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kuwapongeza Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET)* ambao ndiyo walioandaa na kusimamia maonesho hayo kwa ufanisi mkubwa pamoja na tatizo la kifedha walilonalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania. Kwa muda mrefu biashara za ndani zimeonekana kutokuwa na msimamiaji hasa baada ya kuvunjwa kwa iliyokuwa Halmashauri ya Biashara ya Ndani *(BIT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefarijika na wazo la Wizara la kuandaa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania ambayo itafuta Sheria Na.5 ya mwaka 1978 iliyoanzisha *(BET)* na Sheria Na.15 ya mwaka 1973 iliyoanzisha Halmashauri ya Biashara ya Ndani *(BIT).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri *TAN-TRADE* ianzishwe haraka iwezekanavyo na kwa maana hiyo mchakato wa mabadiliko ya kisheria ufanyike mapema ili kuharakisha maendeleo ya sekta hii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuhusu majukumu ya yanayofanywa na Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, Kamati inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa kuziwezesha *SIDO*, *NDC*, Baraza la Mfumo wa Stakabadhi ya Maghala pamoja na Taasisi za Utafiti na Maendeleo zikiwemo *TIRDO, TEMDO* na *CARMATEC* ili kuweza kutekeleza vema majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru tena wewe binafsi, Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai, (Mb.), Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, (Mb.) na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, (Mb.), kwa kuendesha Vikao vya Bunge vizuri kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu, (Mb.), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, (Mb.), Katibu Mkuu, Dkt. Stargomena Tax Bamwenda, pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na taasisi zake kwa maelezo na ufafanuzi walioutoa mbele ya Kamati, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara na wakati wote wameonyesha ushirikiano mkubwa na wa karibu na Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wao katika kuchambua Bajeti ya Wizara na kutoa Maoni haya ya Kamati. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatibu, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Ame P. Ame, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Mohammed A. Chomboh, Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby na Mheshimiwa Abdallah S. Sumry.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililillah, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Aidha, niwashukuru Makatibu wetu, Ndugu Angelina Sanga na Ndugu Abdallah Hancha, kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba Bunge lako Tukufu liyapokee maoni haya na kuyajadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani anayeshughulikia Wizara hii, Mheshimiwa Lucy Owenya, anasema Waziri Kivuli anaomba aongezewe muda, anasema yeye amevaa peke yake, wenziwe wamevaa sare.

**MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii, ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa namna ya kipekee kabisa, kuwashukuru wanachama na wote wenye mapenzi mema na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kuendelea kutuunga mkono katika mapambano ya kumwendeleza Mtanzania na hasa vita dhidi ya ufisadi na rushwa, unyanyaswaji na dhuluma nyingine mbalimbali ambao ndio ukombozi wa mwananchi kwa ujumla. Naahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitaendelea kulitumikia Taifa langu kwa uadilifu siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawajibika kwa moyo wa dhati kuwashukuru viongozi wangu wakuu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, (MB), Mbunge wa Wawi na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, (Mb), Mbunge wa Karatu, kwa imani kubwa waliyo nayo kwangu mimi na hivyo kwa mara nyingine kuendelea kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, napenda kumshukuru Naibu wangu, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, (Mb) kwa ushirikiano alionipa katika kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuishukuru familia yangu hasa mwanangu Yohane na mume wangu mpenzi, Dr. Fidelis Owenya ambaye angependa kuwa hapa leo lakini kwa kuwa anapenda kulitumikia Taifa kwa moyo wote, imebidi andelee na majukumu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006, sekta ya viwanda ilichangia asilimia 20.9 kwa pato la Taifa. Mwaka 2007, sekta ya viwanda ilichangia asilimia 21.2. Ni dhahiri kwamba sekta ya viwanda bado haitoi mchango stahiki katika pato la Taifa. Ukuaji wa viwanda umekuwa ukisuasua kwa sababu nyingi na hasa ikichangiwa na sera za

utandawazi. Baadhi ya mambo yanayokwamisha ukuaji wa sekta ya viwanda ni pamoja na gharama za uzalishaji jambo linalosababisha ughali wa uchumi na bidhaa zetu za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za uzalishaji viwandani kwa mwaka 2007 zilikuwa Sh.1,712,247 milioni ikilinganishwa na Sh.1,695,292 milioni mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 27.1. Ongezeko hili la gharama za uzalishaji lilisababishwa na kuendelea kupanda kwa gharama za umeme na mafuta pamoja na urasimu mkubwa uliopo Serikalini katika kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa ciwanda unategemea pia nishati mbalimbali kwa mfano gesi asilia, umeme na kadhalika. Ni jambo la kushangaza kwani viwanda kadhaa sasa hivi vinatumia gesi asilia katika uzalishaji wake lakini bei za bidhaa zake kwa mlaji bado ni ghali. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri mwenye dhamana alitolee ufafanuzi jambo hili hasa pale gesi asilia inayozalishwa hapa kwetu, kwani haijaathirika na bei za dunia kama ilivyo kwa mafuta, ni kitu gani hasa kinafanya bei katika viwanda hivi vinavyoendeshwa kwa gesi asilia inakuwa ya juu na au inaendelea kupanda kama ilivyo kwa bei ya bidhaa katika viwanda vinavyoendeshwa kwa kutumia nishati ya umeme wa kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, miundombinu hafifu kama vile reli na barabara, ziliendelea kuchangia kupanda kwa gharama za uzalishaji. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuangalia upya sera zake ili kutoa unafuu wa gharama za umeme wa maji kwa viwanda vyetu ili viweze kuzalisha kwa ushindani.

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuwa na mpango wa pamoja utakaozihusisha sekta mbalimbali (*intergrated Sector Strategic Plan)* kwani ukuaji wa sekta ya viwanda unatakiwa kwenda sambamba na ukuaji wa sekta zingine katika uchumi mzima. Mpango huu, utasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa baadhi ya matatizo yaliyopo katika Wizara hii. Aidha, mpango huu utaweza kusukuma gurudumu la ukuaji wa Viwanda nchini na hatimaye kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa 2007, kimeainisha kuwa ajira viwandani imeongezeka toka watu 89,316 mwaka 2005 na kufikia watu 91,112 ongezeko la wafanyakazi 1,796 tu. Kambi ya Upinzani, inahoji kati ya ajira hizi ni zipi zinatoka katika sekta rasmi na zipi zinatokana na sekta isiyo rasmi? Aidha Kambi ya Upinzani, inapenda kujua ni viwanda vipi vilivyochangia katika ajira hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeeleza kuwa “Bajeti ya 2008/09 imetenga shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa *TIB*, ambao utafikia shilingi bilioni 50. Uamuzi huu wa Serikali ni wa makusudi kwa kutambua tatizo kubwa la ukosefu wa mikopo ya uzalishaji katika viwanda na kilimo.” Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuitaka Benki hii kuwekeza na kukopesha wananchi na au watu ambao wapo tayari kuwekeza kwenye sekta ya viwanda na hasa viwanda vya usindikaji “*processing industries”* na vile ambavyo vitajihusisha moja kwa moja na usindikaji wa mazao ya kilimo yapatikanayo hapa nchini kwani kufanya hivi viwanda vyetu vitaweza kukua na

sekta nzima ya kilimo kukua na hivyo kuboresha maisha ya Watanzania.Aidha Benki ijielekeze katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuzuia usafirishaji wa vito ghafi kwa kuwasaidia Watanzania ambao wamekwishaomba kuwekeza katika viwanda hivyo ila wanakwamishwa na urasimu wa Benki tu *(ATGEM LINK* ya Arusha).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana (2007), niliuliza Serikali kuhusu mchakato mzima wa ufufuaji/uimarishaji wa viwanda vilivyobinafsishwa. Tunamtaka Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko alieleze Bunge lako Tukufu hatua ambazo Serikali imeshachukua mpaka sasa katika mpango wa kufufua Viwanda vya *General Tyre* cha mjini Arusha, *Kilimanjaro Machine Tools*, Kiwanda cha Kutengeneza Magunia, Kiwanda cha Ngozi cha Mjini Moshi na Kiwanda cha Tanganyika *Packers* cha Dar es Salaam pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uzalishaji wa viwanda nilivyovitaja pamoja na viwanda vingine hairidhishi. Aidha, baadhi ya viwanda hivi havijazalisha tangu vibinafsishwe. Kambi ya Upinzani inapenda Serikali iwaeleze Watanzania juu ya Kiwanda cha *General Tyre* cha Arusha kabla ya kubinafsishwa kiwanda hiki kilikuwa kinazalisha kwa asilimia ngapi na sasa hivi hali ikoje? Kitu gani hasa kilitokea mpaka Kiwanda hiki kimefikia hatua hii na sasa inasemekana ‘kiko *ICU’* wakati ndio kilikuwa kiwanda bora katika Afrika Mashariki yote?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mbia kwenye kiwanda cha *General Tyre* ana hisa 24% na Serikali ina hisa 76%. Je, tatizo ni nini? Ni uongozi au ni mtaji? Mbia huyu ameweka mtaji kiasi gani na Serikali imeweka mtaji wa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kufahamu katika kipindi cha Miaka 10 iliyopita, Serikali imewekeza kiasi gani au kwa mkopo au mdhamana, au ruzuku katika kiwanda hiki? Kiwanda kimechukua mikopo kiasi gani kutoka kwa mashirika mengine ya umma kama *NSSF* na kama madeni hayo yamelipwa na au yanapangwa kulipwa vipi ikizingatiwa kuwa hizi ni fedha binafsi za Watanzania Wafanyakazi waliowekeza fedha zao kama bima yao ya wakati wa uzeeni? Kuna taarifa kwamba madeni yamechangia uzoroteshaji wa uzalishaji wa kiwanda hiki. Je, madeni hayo yanatokana na nini na maamuzi ya yaliyosababisha madeni hayo yamesababishwa na nani? Je, kiwanda wadaiwa hao ni kina nani hasa wanadai kiasi gani? Pia mwekezaji ameshawekeza kiasi gani ikianisha amewekeza nini na lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi ya Upinzani, inahitaji kujua ni kwa nini mbia huyu amepewa majukumu ya kuongoza kiwanda *(top management*) ambayo yanampa uwezo wa kufanya maamuzi makubwa licha ya kuwa na hisa ndogo kuliko Serikali kwa niaba ya Watanzania ambao ndio wenye kiwanda hicho? Tunamtaka Waziri atueleze wajibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya kiwanda hiki na ni kwa jinsi gani wamekubali hali ya kiwanda kufikia hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuangalia upya mkataba wa *General Tyre* na huyu mbia katika kulinusuru shirika hili. Kuangalia kama kuna mianya ya hujuma ikiwa ni pamoja na kurejesha shamba la mpira la Kihuhwi kwa

*General Tyre* au kumlazimisha mwekezaji wa shamba hilo kuuza malighafi yote kwa kiwanda cha *General Tyre* ili kuongeza uzalishaji wa matairi na kukuza ajira na uchumi kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Kilimanjaro Machine Tools* kiwanda hiki kilikuwa kinazalisha bidhaa mbalimbali ambazo zilitumiwa na wajasiriamali kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Hali hii iliweza kutengeneza ajira nyingi na kuinua hali ya maisha kwa watu wengi. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ieleza nini kilichotokea hadi kiwanda hiki kufikia hatua ya kutokuzalisha? Je, ni kweli kiwanda hiki kinadaiwa na nchi ya Bulgaria na kama ni kweli kinadaiwa kiasi gani? Je, hali hii imeathiri vipi katika mchakato mzima wa kumtafuta mwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kwa vile hiki ni kiwanda mama kuna haja ya Serikali kuwasiliana na nchi ya Bulgaria na hata ikiwezekana kukikopesha ili waweze kuendeleza teknolojia waliyokuwa wameianzisha, jambo hili likifanikiwa litakuwa ni ukombozi kwa vijana na nguvu kazi kwani wataweza kununua vitendea kazi vitakavyotengenezwa hapa nchini bila kuagizwa nje. Kuna taarifa kwamba Serikali ina majadiliano na mbia ambaye ataacha kazi za msingi (*core activities)* za kiwanda na kuwa na uzalishaji tofauti ya ule wa awali. Kambi ya Upinzani, inataka uthibitisho wa taarifa hizi kwani hii ni hujuma ya maendeleo ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda kadhaa vilivyobinafsishwa kwa lengo la kuongeza tija. Lakini kinyume na matarajio yetu, viwanda hivyo vimekuwa vikidorora siku hadi siku. Kambi ya Upinzani, inahoji sababu za udororaji huo ikizingatiwa kuwa michakato ya ubinafsishaji ilitekelezwa kwa kufanya upembuzi yakinifu kwa mbia au mnunuzi wa kiwanda husika ili kuhakikisha kuwa uzalishaji utaongezeka na ajira zitaongezeka, hili linatokeaje? Hii inatupa mashaka na wahusika katika mchakato wa ubinafsishaji kama kweli walifanyakazi kwa kuweka maslahi ya Taifa mbele au maslahi yao na wanunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyote vya ngozi vilivyobinafsishwa vinafanya kazi chini ya matarajio. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu utendaji huu mbovu wa kazi kwani Kambi ya Upinzani, inaona ni uhujumu wa uchumi katika zoezi zima la kubinafsisha viwanda kama hivi. Kambi ya Upinzani, inataka maelezo ya kina kutoka Serikalini kuhusu suala hili la viwanda vya ngozi ikiwa ni pamoja na hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Tanganyika Packers*. Kiwanda hiki kimeacha kabisa shughuli zake za awali na mpaka hivi sasa wananchi hawajaelewa mwelekeo wa kiwanda hicho. Kambi ya Upinzani inaungana na wananchi kudai maelezo ya kina kutoka Serikalini kuhusu makubaliano ya mchakato mzima wa ubinafsishaji wa kiwanda hicho. Kwani kuna taarifa kwamba eneo la kiwanda limegeuzwa kuwa eneo la maduka au shule. Jambo ambalo tunaona ni kinyume na masharti ya mkataba wa ubinafsishaji wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Sukari cha Kilombero. Kiwanda hiki kiliuzwa kwa wawekezaji wanaojulikana kama ILLOVO kwa kununua mali na madeni ya kiwanda hicho kwa Tshs.16Billion, nia ikiwa ni kuongeza uzalishaji na kuinua hali bora kwa wafanyakazi wake na pia kuwalipa wale wote watakaopunguzwa malipo yao stahiki kulingana na mkataba wa hiari kati ya wafanyakazi na uongozi wa Kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo limeishtua Kambi ya Upinzani, ni pale ilipobaini kuwa Kilombero ilikuwa na viwanda viwili vya kuzalisha sukari, yaani K1 ambacho kina eneo la 6,214.5 hekta na K2 kina eneo la hekta 3,153, vyote hivi vilihesabiwa kama kiwanda kimoja na kuuzwa kwa bei tajwa hapo juu. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe majibu sahihi, inakuwaje viwanda viwili vyenye eneo la jumla ya hekta 9,367.5 viuzwe Kwa bei sawa na kiwanda kimoja cha Mtibwa yaani kiwango kile kile cha Tshs.16billioni? Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iweke hadharani angalau katika *Library* ya Bunge ili Wabunge waweze kuchunguza mkataba huu kama uko kwa maslahi ya Taifa au la.

Aidha, Serikali inawashughulikia vipi wale watumishi ambao walikitumikia kiwanda hicho kwa muda wa zaidi ya miaka 10? Ni kwa nini Watumishi hao wamehangaika miaka yote bila kulipwa stahili zao? Kambi ya Upinzani, inahitaji maelezo ya kina kuhusu maslahi ya Watumishi hawa, ambao kumbukumbu zinaonyesha wamechoka sasa kupita ofisi hadi ofisi, ikiwemo kupitia vikao vya CCM? Hatuwezi kuwaacha Watanzania wenzetu, waliotoa jasho lao kuathirika kwa kiwango hiki kutokana na Sera ya Ubinafshaji, jambo ambalo Wabunge wengi tulikuwa tumeshauri Serikali kulitekeleza kwa umakini mkubwa na hasa kwa kuzingatia maslahi ya Wafanyikazi walioko. Katika hili, hatuhitaji majibu ya kisiasa, ni imani yetu Mheshimiwa Waziri atajibu kwa kina na hasa hatua gani zinachukuliwa ili kero hii ya Watanzania wenzetu iweze kumalizwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Viwanda vya Saruji. Mara nyingi tatizo la nchi zinazoendelea na hasa Bara la Afrika na Tanzania ikiwa mojawapo ni kutumia wasichozalisha na kuzalisha wasichokitumia. Kwa mfano, tunafahamu kwamba (*gypsum)*, ni malighafi ya kutengenezea *cement* na inapatikana nchini na hasa maeneo ya Kilwa, Manyoni na baadhi ya maeneo ya Tanga hata hivyo viwanda vya *cement*, kama vile *Twiga Cement* huagiza *gypsum* kutoka nje ya nchi. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ieleze kwa kina sababu zinazopelekea hali kama hii ambayo inaathiri ajira na uchumi wa Tanzania kwa ujumla. Kama tunaweza kuangalia upya mikataba ya madini, ni kwa nini tunashindwa kuangalia upya mikataba ya ubinafsishaji wa viwanda vya *cement* kwa mantiki ya mnyororo wa thamani (*value chain)* au mikataba ya malighafi *(sub contracting).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, tunapenda kukumbushia ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu 27-6-2008 hapa Bungeni kuhusiana na hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, (MB), Mbunge wa Karatu, kuwa kuhusiana na Kiwanda cha Mgololo

Waziri mwenye dhamana ndiye atakayetoa majibu, naikumbusha tena Serikali kuhusiana na ahadi yake hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Mgololo kilibinafsishwa kwa Kampuni ya *RAI Group Ltd* ya Kenya tarehe 16th January 2004 kama inavyoonekana kwenye *Assets Sale Agreement* kati ya *United Republic of Tanzania* na *RAI Group Ltd* inayomilikiwa na Wakenya wawili, Bwana Jaswant Singh Rai na Bwana Sarbjit Singh Rai, kila moja akiwa na hisa 0.006% kwa bei ya Dolla za Marekani 26 Millioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Waziri wa Viwanda na Biashara aliyotoa ndani ya Bunge lako Tukufu, tarehe 07 August, 2008, imezidi kuzua utata kuliko kutoa majibu. Mkataba huu wa mauziano, unatisha na una mapungufu mengi, hivyo, Kambi ya Upinzani, inataka ufafanuzi wa kina katika maeneo yafuatayo:-

Kifungu cha 3.1 cha Mkataba wa Mauziano, unatamka kuwa Bei ya mauzo ni Dolla za Marekani 26 millioni. Cha kushangaza ni kuwa mkataba huo huo unaeleza Serikali italipwa Dolla za Marekani 1 Million siku ya kuwekeana saini na Dolla za Marekani 3,000,000 zitawekwa kwenye *Escrow Account* ambazo Mwekezaji atazichukua atakapokuwa ametimiza masharti fulani fulani kwa ukarabati wa kiwanda "chake". Maana yake ni hela zake na si malipo ya ununuzi wa kiwanda. Mambo haya, yanahitaji ufafanuzi na Kauli ya Waziri haikutoa ufafanuzi kabisa kuhusu hali hii tata. Fedha zingine Dolla za Marekani 22 Millioni atazitumia Mwekezaji kwa kufanyia kiwanda ukarabati, nazo zinabaki kwake. Kama lengo lilikuwa kuhakikisha kiwanda kinaendelea kwa nini Serikali haikusema hivyo wazi katika mkataba? Ni nini basi maana na Tafsiri ya "*Purchase Price*" kwa mujibu wa Waziri? Mheshimiwa Naibu Spika, hivi anadanganywa nani? Kama Bei ni $ 1 Millioni kwa nini isielezwe hivyo wazi wazi? Tatizo ni nini?

Kukosekana kwa mnunuzi kama Serikali inavyotaka kueleza kwa nini hakikuuzwa kwa Shs '1' yaani '*nominal value'* katika mauzo ya viwanda na Makampuni ambayo kweli yamedhihirika yako hoi kabisa na ikajulikana hivyo kuliko kutumia mkataba ambao kwa dhahiri una sura ya udanganyifu? Hili fumbo maana yake ni nini? Isitoshe hata kodi ya Serikali imekwepwa kwani mkataba unasema dhahiri kuwa kwa kutimiza matakwa ya ushuru wa *Stamp Duty,* kiwango kitakachotumika ni Dolla za Marekani 1 Millioni? Hii maana yake ni nini kama si kutoa sadaka rasilimali za Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kujua hivi hawa wawekezaji wenye Hisa 0.006% kila mmoja ni kweli wawekezaji? Wanaweza kukifufua kiwanda kama kweli kiko kwenye hali mbaya kama Serikali inavyosema? Utafiti wetu umeonyesha kuwa kumbe mwenye mali halisi wala siyo *Rai Brothers* kama walivyo kwenye *Sale Agreement*, bali ni *Angel Hurst Industries* ya Uingereza yenye hisa 99.988%

kama ilivyosajiliwa kwenye Kituo cha Uwekezaji kama inavyoonekana kwenye *Certificate of Incentives* No. 00021049 iliyotolewa *TIC* tarehe 19 April, 2004 kwa *Mufindi Paper Mills Ltd* ambayo ndiyo Kampuni iliyosajiliwa baada ya kununua Kampuni ya *Southern Paper Mills (SPM)* ambayo ilikuwa asilimia 100% mali ya Serikali na hivyo mali ya Watanzania wote na kusimamiwa na *NDC* ikiwa na Hati ya *Industrial Licence No. 0907*. Isitoshe, kiwango cha Fedha kilichotajwa kwa *TIC* ni Dola za Marekani 52 Millioni *(Foreign*) na Tshs billion 9.251 fedha za ndani yenye jumla ya Dola za Marekani 61.251 na siyo 25.Millioni walioyotaja kwenye Nyaraka mbalimbali za *Sale Agreement.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kuwe na udanganyifu huu mkubwa? Hata kama Serikali itajitetea kuwa *Angel Hurst Industries* ni ya hao hao, Serikali itamke ndani ya Bunge hili kama jambo hilo kisheria ni sahihi na hao wenye hisa zaidi ya 99% wanaonekana wapi? Kama mkataba wa mauzo hauwataji, kukitokea tatizo, wao watawajibikaje na mkataba ambao wao si washiriki? Kwa nini kuwa na mikataba kama kunaweza kuwa na watu waliojificha nyuma na mkataba kusainiwa na watu wasio na kitu? Je, ni kweli *Rai Group* iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania, ni wamiliki wa *MPL Ltd*. wakati kwa pamoja wakati wa kuuziana wanamiliki tu asilimia chini ya 0.01? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri aeleze kwa kina fumbo hili maana yake nini kwa Watanzania na ni nani hasa anayedanganywa hapa? Iwapo hatutapata maelezo ya kina, Kambi ya Upinzani itaangalia uwezekano wa kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kufumbua fumbo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Kazi katika hukumu yake ya Uchunguzi wa Mgogoro wa Kazi, Na. 80/2006 ya *TUICO vs PSRC* na wenzake ilitamka wazi kuwa:-

*"si rahisi kuamini kuwa mali zote za Southern Paper Mills Ltd, za thamani ya soko la mabilioni, si chini ya 500 Billioni kwa makisio yangu na si ile thamani ya Tshs 85 Billioni iliyotumika kuuzia, tunaona hii ni "token/book price value" tu ambayo mathalan flat rate ya Trailer Scania linalofanya kazi lilithaminiwa kwa Tshs.300,000/- kwa kila Traillor ambayo ni chini ya bei halisi hata ya tairi lake moja tu…"*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hali ya kutisha kwani hata kama tatizo ni kuwa na mnunuzi wa *SPM Ltd.* basi wangeliuza vifaa hivyo kimoja kimoja wangelipata mara kadhaa ya bei waliyopata. Rasilimali zilizouzwa ni pamoja na nyumba zikiwemo za *Grade A,* Kijiji kizima cha Wafanyakazi kama ilivyorikodiwa kwenye Mkutano wa Mashauriano wa Kamati ya *Fast Track* ya Baraza la Mawaziri la tarehe 4 August, 2003 inayosomeka:-

*"…kinachouzwa ni kiwanda, kijiji na eneo la ardhi ambalo bado kuendelezwa la hekta 28,000".*

Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni kwa nini mwekezaji huyu kauziwa mali ya Watanzania kwa bei ya kutupa? Haiwezekani gari la tani 60 tena '*heavy duty'* likauzwa kwa Sh.600,000/= bei inayofanana na bei ya tairi moja tu la gari hilo! Hapa kunahitajika maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa si makini katika ubinafsishaji huu, kama ilivyo kwa mengine mengi. Watumishi zaidi ya 760 bado wanadai haki zao pamoja na hukumu iliyotolewa na Mahakama, wanadai zaidi ya TShs.2,647,255,816. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali isimamie utaratibu unaoeleweka wa kulipwa Watanzania hawa maskini ambao wamejikuta wao na familia zao katika maisha magumu kutokana na maamuzi yasiyo makini ya Serikali. Kambi ya Upinzani, inafahamu kuwa *SPM* imeomba *Review* ya Tuzo iliyotolewa na Jaji Mwipopo, lakini kwa vile Serikali yenyewe haijakata Rufaa wala haijaomba *Review* basi ionyeshe njia kwa kuanza kulipa sehemu yake ya Tuzo kama ilivyotolewa uamuzi na Mahakama ya Kazi, ama sivyo Waziri alieleze Bunge hili Rufaa hiyo ni namba ngapi na au *Review* hiyo ni namba ngapi. Hata Hati ya Marejeo (*Review)*, NA.42A iliyowasilishwa na *MPM Ltd*. dhidi ya *TUICO* kwa niaba ya Bwana Thomas Mashaka na wenzake 760, ilimtaka Wakili Amour wa *MPM* Ltd. awasilishe Kiapo Kinzani hadi tarehe 18/07/2008 jambo ambalo halijafanyika hadi leo na Hati Kiapo ya Majibu iliyotakiwa iwasilishwe tarehe 29/07 2008 nayo isingewezekana kuwasilishwa kwa kuwa Hati Kinzani haikuwa imewasilishwa jambo ambalo linaashiria kuwa hawakuwa na nia ya kuendelea na Marejeo hayo. Kambi ya Upinzani, inaamini, hii ni mbinu tu ya kuchelewesha haki za Watanzania ambao tayari familia zao zimeteseka vya kutosha kwa kunyimwa haki zao ambazo tayari zimekwisha kutolewa TUZO.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali yafuatayo:-

(i) Bunge hili lielezwe *Angel Hurst Industries* ni nani hasa na kwa nini hawako popote kwenye Mkataba rasmi? Uchunguzi wa kina uliofanyika na Kambi ya Upinzani, umeshindwa kuonyesha hata usajili wa awali wa Kampuni hii katika kisiwa cha *British Virgin Islands,* kama Waziri anao basi awasilishe ni Hati namba ngapi na ya tarehe ngapi!;

(ii) Kama Waziri anavyotaka kulieleza Bunge hili, ni kwa nini Kampuni haikutajwa katika wasifu wa *RAI Group* kama walivyofanya kwa Makampuni tanzu ya *Nilepty* (Uganda) *Ltd, Raiply* Kenya *Ltd, Timsales Ltd, Raiply* (Malawi Ltd), TSRAI Ltd, *Comply Ltd* ambayo hayakushirikishwa kabisa katika kuwekeza kwenye Kampuni ya Mufindi *Paper Mills*. Kuna nini hapa? Mheshimiwa Waziri ni lazima alieleze Bunge hili Tukufu, *Angel Hurst* ilisajiliwa lini *BVI*, kwa hati namba ngapi, mtaji wa kiasi gani, majina ya Wakurugenzi, shughuli za msingi ni zipi, Wakaguzi wake ni kina nani? *Physical Address* yao ni ipi na atoe maelezo ya wazi bila kutafuta visingizio ambavyo

havimfikishi mahali. Kama nilivyosema, iwapo Kambi ya Upinzani haitapata taarifa kamili, nitawasilisha kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ili kupata ukweli kamili juu ya ubinafsishaji huu wa *SPM Mgololo*; *(Makofi)*

(iii) Mkataba kati ya Serikali na *RAI Group*, utazamwe upya kuondoa utata huu wa mali ya Watanzania, ikiwemo vifaa vya kiwanda, nyumba, kijiji cha Wananchi Watanzania na eneo la Hekta 28,000 ambazo hazikulipiwa kitu kabisa, ikiwa lazima tathmini ifanyike upya kuangalia bei halisi ya yote hayo na au Mkataba uvunjwe;

(iv) Hii *NGO* inayoitwa *ICOMET*, iliyopewa Hekta 2,000 lakini ikapewa Hatimiliki ya Hekta zote 28,000 ni ya nani na je, imekwishakulipa 15 Millioni ilizokuwa inaidai Serikali ili iweze kurudisha Hatimiliki. Kulikuwa na mchezo gani hapa?; na

(v) Kambi ya Upinzani inataka Bunge hili lielezwe, ni kwa nini Serikali na Watendaji Wakuu Serikalini hawakulinda maslahi ya nchi yetu, badala yake waliegemea kwa mwekezaji ikiwa ni pamoja na kuweka Jeshi la Polisi kulinda kiwanda hicho kwa miaka yote kwa kodi ya Watanzania, wakati Polisi hao wangeweza kufanya kazi ya ulinzi na usalama wa raia. Kuegemea huku kunaonekana hasa katika barua ya Waziri wa wakati huo wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Juma Ngasongwa yenye Kumb CCD/111/450/01 ya 14 August, 2005 na tena Barua yanye Kumb. Na CCD/111/450/01/33 ya tarehe 8 September, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Maonyesho ya Biashara Sabasaba, Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kuboresha miundombinu iliyopo kwa kuweka *floor pavement* kupunguza vumbi, hata hivyo tunashauri viwanja hivyo viboreshwe viweze kutumika kwa maonyesho tofauti kwa kipindi kizima cha mwaka kama zifanyavyo nchi nyingine. Aidha, Wizara inashauriwa kuweka mkakati na mpangilio mpya wa maonyesho haya ili yawe ni sehemu ya kuwakutanisha wenye viwanda na wanunuzi kwa mantinki ya mikataba (*buying and selling contracting)* na siyo kama ilivyo sasa ambako viwanja vinatumika kama gulio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inashauriwa kuwa na viwanja vidogo vya biashara vya kikanda. Kwani itawapunguzia wenye viwanda gharama za usafirishaji na kutoa fursa nyingi zaidi kwa wao kuweza kujitangaza. Pamoja na suala hili la Kanda, Serikali iweke mchakato wa kuweka mazingira mazuri katika maeneo mbalimbali kikanda ili kuweza kuanzisha viwanda ambavyo vinauhusiano na mazao yapatikanayo kutokana na sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mkutano wa *Sullivan*, Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina juu ya gharama zilizotumika kwa ajili ya

kuandaa Mkutano huo, je, ni manufaa gani halisi na siyo ya kinadharia tu ambayo sisi kama Taifa tumepata kwa kuwa na Mkutano huo? Je, tumeweza kupata masoko wapi na ni kwa ajili ya bidhaa gani? Tumeweza kupata wawekezaji wangapi ambao wapo tayari kuja kuwekeza hapa nchini kwenye ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa? Huu ni utaratibu wa kawaida unapokuwa na mikutano na maonyesho makubwa, unatakiwa kufanya tathmini ya kina ili kubaini faida zinazotokana na hatua mbalimbali zinazotumia kodi za wananchi. Iwapo faida hizo zipo, je, wawekezaji wakija tumejitayarisha kiasi gani? Katika mkutano ule, tuliomba pia wataalam kama Walimu na Madaktari, kama wakija katika Halmashauri zetu miundombinu kama nyumba na kadhalika imeandaliwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo wataalamu wetu hawathaminiwi kama wataalamu wanaotoka nje katika taasisi mbalimbali na kupelekea kutumia wataalamu kutoka nje. Inasikitisha kuona kwamba *NDC* inakodisha wataalamu (*consultants*) wakati baadhi ya wataalam wake kama Mheshimiwa Simbakalia anateuliwa kwenye wadhifa wa kisiasa, kweli kwa hali hii tutafika katika kuleta mapinduzi ya viwanda *(Industrial revolution)?*

Hali ya mashirika yetu kwa mfano *TIRDO*, *SIDO*, *CARMATEC* yanafanya kazi kwa kiwango cha chini kwani hawawezeshwi kwa kupewa fedha za kutosha ikiwa ni pamoja na vitendea kazi ili kutekeleza majukumu yao. Kwa mantiki hii, tunakuwa na wataalamu ambao hatuwatumii ipasavyo na badala yake kutumia wataalamu kutoka nje ya mashirika husika jambo ambalo huigharimu sana Taifa na walipa kodi bila hata wao kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizopo zinazonyesha kuwa Serikali bado haijathamini mchango wa asasi hizo. Taasisi hizo ikiwa ni pamoja na *NDC*, *TIRDO* na *SIDO* katika mpangokazi wao waliomba TShs.7 billion,5 billion na 11 billion kwa mfuatano lakini Serikali imewatengea Tshs.75million,150million na 1 billion kwa mfuatano. Je, ni kweli tumekusudia *NDC* ishirikiane na wawekezaji kwenye miradi mikubwa wakati hata fedha za kufanyia utafiti hawapewi? Hii ni kuonesha kiasi gani taasisi zetu na wataalamu wetu tusivyowathamini kweli na kuwakatisha tamaa na matokeo yake wanakimbilia kwenye siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kutenga maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo ya nje (*Export Processing Zone – EPZ)* katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje. Kambi ya Upinzani, ina wasiwasi na mafanikio ya mpango mzima kufikia malengo yake kwani hadi leo maeneo yaliyotengwa mengi hayana miundombinu ya kuridhisha kama kivutio kwa wawekezaji. Tukumbuke kuwa Duniani kote, miundombinu ya kumvutia mwekezaji ni kazi ya Serikali na siyo ya mwekezaji, vinginevyo ndiyo sababu kubwa ya sisi kupata mkia na wawekezaji kuchukua ng'ombe mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni vivutio gani *(incetives*) wawekezaji katika *EPZ* wanapata na nchi imenufaika kwa vipi? Je, hadi leo ni maeneo mangapi yaliyotengwa kwa *EPZ* na kwa shughuli gani? Tukijua matatizo ya uvamizi wa ardhi nchini, je, maeneo yaliyotengwa ni mangapi yameshapata hatimiliki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, pia inaitaka Serikali kutoa elimu kwa wananchi kama njia ya kuwahamasisha waweze kuelewa na kutumia fursa kama hizi. Serikali haiipi umuhimu unaostahili *EPZ* hii imejidhihirisha kutokana na maombi yao ya bajeti ya TSh.Billion 3 na kupewa billion 1.9. Hivi kweli kwa kiasi hicho wataweza kufanikisha mipango ya shughuli zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuleta mapinduzi au mageuzi ya kweli ya viwanda *(industrial revolution*), lazima mageuzi haya yaendane na mapinduzi ya kilimo *(green revolution*). Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na kutoa kipaumbele katika viwanda vya nguo na (*textile industries*) na usindikaji wa vyakula (*agro processing industries*). Matunda ya mchakato huu, yanaweza kuonekana zaidi ikiwa Serikali itaweka pia mazingira mazuri ya masoko hasa katika kuimarisha na kufufua vyama vya ushirika na kuweka msukumo zaidi wa soko kwa kutumia stakabadhi za maghala kama njia ya kuwalinda wakulima wadogo kwa nchi nzima na kwa mazao yote makubwa yanayozalishwa na wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato mzima wa kuboresha au kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika viwanda (*private public partnership*), Serikali inatakiwa kuandaa sera nzuri ikiwa ni pamoja na sheria ili kuwepo na usimamizi madhubuti wa mapinduzi katika viwanda. Sera na sheria madhubuti zitaweza kusaidia msukumo wa ukuaji wa viwanda kwa njia ya mnyororo wa thamani (*value chain*) mikataba midogo (*subcontracting)* na uhusiano (*linkage).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwekezaji anayetaka kuja kuwekeza kwenye kiwanda cha kutengeza *juice*, ni vizuri kuwepo na utaratibu ambao utamlazimu aidha alime mazao yeye mwenyewe au awe na mkataba na wakulima kuzalisha matunda husika ili aweze kutengeneza *juice* na siyo kuagiza malighafi nje. Aidha, wawekezaji wakubwa wa vyakula wangewekewa sheria za kuwalazimu kuingia mikataba na wakulima ili waweze kulimiwa vitu ambavyo vinakidhi mahitaji ya maduka yao na siyo kuwa na ma-*supermakert* makubwa na kujaza bidhaa za kilimo kutoka nje kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira kama haya yakiwepo yanaweza kuisaidia nchi kuwa na viwanda vikubwa, vya kati na vidogo kwa mtizamo wa *Private Public Partnership*. Hali kama hii inaweza ikaiweka Tanzania katika soko la dunia ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zenye ubora hafifu. Tanzania imeendelea kuwa jalala *(dumping*) la bidhaa zenye ubora usiokidhi kiwango cha Kimataifa.  Hali kama hii ni hatari kwa viwanda vyetu, afya zetu pamoja na uchumi kwa ujumla. Katika hotuba yangu ya mwaka jana niliitaka Serikali ihakikishe kwamba mitumba ya nguo za ndani isiingizwe au kuuzwa nchini kama njia ya kulinda afya ya wananchi kama ambavyo Serikali ilikwisha kuahidi ndani ya Bunge hili.  Kinachonisikitisha nguo hizo bado zipo na zinauzwa waziwazi wakati vyombo husika vikishuhudia licha ya tamko la *TBS* kwamba zimepigwa marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze tatizo ni nini kushindwa kuzuia uingizaji na uuzaji wa nguo hizo.  Sambamba na hilo vifaa hafifu vya umeme vimeendelea kuingia nchini bila udhibiti madhubuti hali ambayo imechangia majanga ya moto katika sehemu mbalimbali nchini.  Pamoja na jitihada nzuri za Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission*) za kukamata na kuharibu bidhaa hizi feki bado tatizo ni kubwa.  Kuna haja ya kuiwezesha Tume ya Ushindani, ili iweze kuwa katika kila Mkoa ikiwa ni pamoja na mipakani na kupitia sheria iliyoianzisha Tume husika kuangalia mapungufu yaliyomo ili kuweza kudhibiti uhalifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wa bidhaa kama hizi kama wahujumu uchumi.  Aidha, chombo kama *TBS*, nacho kinapaswa kiwezeshwe ili kudhibiti hizi bidhaa zisizokidhi viwango.  Tunaitaka Serikali kushirikiana na makampuni yanayotengeneza bidhaa zinazoingia Tanzania kuweka nembo ambayo inayokidhi viwango vya Tanzania aidha Serikali inashauriwa kutuma maofisa wao katika viwanda husika kama njia za kuhakiki bidhaa ziingiazo nchini. Hata hivyo, ni muhimu kuwepo na utaratibu wa kuandikisha bidhaa na viwanda husika ambavyo vitaruhusiwa kuingizwa nchini. Kwa vile bidhaa nyingi zinazouzwa na wamachinga hazikidhi viwango kuna haja ya kutunga sheria ya kuwabana wauzaji na wanunuzi wa bidhaa barabarani. Jambo hili litaongeza pato kwa Serikali kwani wengi hutumiwa na watu wanaotaka kukwepa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu, Serikali kupitia fungu na 260700, *Rental Expenses*, imetenga kiasi cha TShs. 744,900,000/= (milioni mia saba na arobaini na nne na laki tisa ) kwa ajili ya pango (*Rental Expenses*) na kati ya hizo Tshs.726,000,000/= fungu na 260703 ni kwa ajili ya pango la ofisi kwenye jengo la *NSSF Water Front*. Kambi ya Upinzani, inaziona gharama za pango kuwa ni kubwa mno hasa ukizingatia kwamba Wizara inashindwa kutenga fedha za kutosha kwa masuala ya maendeleo. Kwa njia hii ni kuwa kwa kipindi cha miaka mitano (2005-2010) Wizara itakuwa imetumia kiasi cha shilingi 3,630,000,000 kwa ajili ya kulipia pango la Makao Makuu ya Wizara fedha ambazo ni nyingi kupindukia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe tamko rasmi ni kwa nini isitenge fedha kwa ajili ya kujenga jengo lake yenyewe kama inavyofanyika

kwa Wizara zingine. Wizara kuwa na jengo lake yenyewe ni faida kwa siku za mbele na tunashauri Serikali itenge kiwanja cha kujenga jengo la Wizara haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kipindi hiki cha 2008/2009 imetenga pia TSh.500,000,000/= kupitia fungu na 310600 *Plant And Equipment* kwa ajili ya kununulia magari mawili ya Ofisi na gari la zimamoto katika eneo la *BWM – SEZ.*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo ni nyingi mno kwa ajili ya kununulia magari ya Kifahari, Kambi ya Upinzani inataka fedha hizo ziongezwa kwenye taasisi za utafiti na maendeleo hususani *CAMARTEC*, *TEMDO* na *TIRDO* ili zikasaidie kuimarisha taasisi hizo kwa masilahi ya taifa na Ofisi inunuliwe magari ya kawaida yatakayokidhi hadhi ya barabara zetu. Tunataka maelezo ya kina kuwa magari haya ni kwa ajili ya ofisa gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumejitokeza tabia ya viongozi na watumishi wa umma kupenda kutumia magari ya kifahari hasa *Toyota Landcruiser Vx*, *Nissan Patrol* wakati ambapo watumishi wa umma wangeweza kutumia magari ya kawaida kwa bajeti ndogo kuliko mamilioni yanayotumika sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kutenga bajeti kwa ajili ya kununua gari la Zimamoto halina maana. Nashauri Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Ndani ili suala la Zimamoto lishughulikiwe na kikosi cha Zimamoto kwenye maeneo yote yanayohitaji ulinzi na zimamoto. Kwani utaratibu kama huu ukiachwa wa kila Wizara kujinunulia gari lake la zimamoto utakuwa ni usumbufu kwani hapatakuwa na usimamizi (*coordination)* na hatimaye fedha nyingi kutumika bila usimamizi na bila tija kama ilivyokwisha kutokea kwenye eneo Halmashauri zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha *CBE* kipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, cha kusikitisha chuo hiki kina matatizo mengi lakini fedha walizoomba wamepewa pungufu sana. Waliomba bill 5.4 na kupewa million 100. Je, fedha hizi zitatosha baadhi ya matatizo yafuatayo? Chuo hiki kinakabiliwa na matatizo ya mabweni ya wasichana, Chuo cha Dodoma na cha Dar Es Salaam, madarasa yanatakiwa kuongezwa, hivi tunategemea wanafunzi hawa watasomaje wakati hamna *Library?* Jengo la *CBE* lililopo hapa Dodoma linahitaji kukarabatiwa sababu limechakaa sana. Kwa sasa hivi wanafunzi wengi Tanzania nzima wanategemea vyuo hivi viwili. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itafute kiwanja mjini Mwanza wajenge chuo ili kuwawezesha wanafunzi wa Kanda hiyo kusoma kulekule badala ya kusafiri mbali ukizingatia gharama za usafiri ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiritimba wa kuingiza vileo nchini. Sheria ya Ushindani (*Fair Competition Act, 2003*), ndiyo sheria inayosimamia masuala yote

yanayohusu ushindani wa kibiashara inayofanya kazi kupitia Tume ya Ushindani. Kuna kampuni inayoitwa *Baraka Store* ambayo ilifanikiwa kuwa wakala wa kuingiza bia aina ya *Heineken* toka Uholanzi. Kwa makusudi mazima, kuna kampuni nyingine imehodhi soko la bia hizo hapa Tanzania na inafanya kila mbinu kuhakikisha kuwa hakuna Kampuni yoyote itakayoingiza bia hizo hapa Tanzania. Hii ni kinyume na sheria na dhana nzima ya ushindani kwenye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Commissioner* wa Kodi kwa kushirikiana na Mabibo *Wine & Spirits Ltd.* kwa makusudi mazima waliisababishia hasara Kampuni Mshindani ambayo tayari ilikwishalipia gharama zote zinahusika katika uingizaji wa bidhaa kutoka nje, kwa tangazo la *Commissioner* wa Kodi kuwa Mabibo ndiyo Kampuni pekee inayoweza kuagiza bia hizo hapa nchini. Kambi ya Upinzani, inataka maelezo, je, ni *Commissioner* wa Kodi ndiye anayetoa kibali cha *exclusive right* kwa muingizaji bidhaa au ni mzalishaji wa bidhaa hizo? Ni kwa nini *TRA* itumiwe katika ugomvi wa kibiashara kati ya *Baraka Store* na *Mabibo Wine & Spirit Ltd.* wakati Tume ya Ushindani ipo?

Haya ni masuala yanayoonyesha wazi kuwa yamefanywa kwa maslahi binafsi (UFISADI). Kambi ya Upinzani, inataka ufafanuzi wa kina na hasa kujua kama utaratibu huo ni sahihi ama la na iwapo siyo sahihi, Serikali inachukua hatua gani kwa Afisa wake huyo aliyeruhusu ukiritimba kinyume na Sheria za nchi na kuliingizia Shirika lilipata ushindi wa kuwa Wakala kukataliwa na *Commissioner? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa hotuba, wala hukuhitaji muda wa ziada. Sasa watakaoweza kuchangia asubuhi hii ni Mheshimiwa Abdallah Sumry, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Janeth Massaburi. Hawa ndiyo wanatosha mpaka saa saba. Halafu mchana tukiingia atakuwepo Mheshimiwa Ndesamburo, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Aloyce Kimaro na wengine atataja Mwenyekiti kwa jioni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu ya shughuli nyingine, ninamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti anipokee kazi na ataendelea mpaka jioni.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa namwita mchangiaji wa mwanzo Mheshimiwa Abdallah Sumry atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kufika siku ya leo, niweze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Pia, namshukuru kwa kuweza kunipa nafasi kuwa mtu wa kwanza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo Wizara mtaji na tunashukuru tunao viongozi mahiri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami na dada yangu Katibu Mkuu wa Wizara, viongozi wote wa Wizara pamoja na wataalam kutoka taasisi zote zinazoshiriki katika Wizara hii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara na napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina maeneo matatu. Eneo moja ni wakulima ambao ni asilimia 80. Eneo la pili ni wafanyakazi na eneo la tatu ni wafanyabiashara. Wizara hii ndiyo kitovu kikubwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na hatuwezi kufikia malengo yetu ya kukuza uchumi kikweli kweli bila viwanda. Tumeona mtiririko wa kodi mbalimbali zinazotufikia ni kutokana na kuwa na viwanda ambavyo tayari vitakuza thamani ya mazao yetu kutoka shambani kwa mkulima na pia thamani ya matunda yetu yatokanayo na ardhi nzuri tuliyonayo badala ya kutumia matunda kutoka Dubai nchi ambayo tayari inatengeneza ardhi na umwagiliaji wa maji kwa kutegemea mvua ya miaka mitano mara moja katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee pia kwenye sehemu kuu muhimu juu ya vitendea kazi vya Jumuiya zetu tulizoteua ndani ya Wizara hii. Wizara hii ina Shirika la *CARMATECH*, Shirika la *TIRDO* na *SIDO*. Maeneo yote haya ni muhimu sana kwetu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Wizara yetu imepewa pesa kiasi kidogo sana ukilinganishwa na majukumu makubwa iliyonayo. Kwa upande wangu naweza kusema, kiuchumi, Wizara hii ni uti wetuwa mgongo. Kwa sababu hakuna mkulima atakayenufaika na mazao yake katika enzi na nyakati hizi ambazo zina shida ya chakula ikiwa mazao yake hayataboreshwa vyema.

Mfano mzuri ni wa mazao yetu yaliyopo mashambani. Wakati huu ni wakati wa shida ya chakula katika dunia nzima. Mungu ametujalia, tuna mvua ya kutosha, tuna ardhi, tuna watu wa kutosha na tuna siasa safi. Wizara hii ilipaswa itazamwe na Serikali kwa namna ya pekee kabisa ili vitendea kazi vyote vya Jumuiya hizi nilizozitaja viweze kufanya kazi zake za utafiti na *SIDO* kwa ajili ya kuimarisha vijana wetu waweze kuwa na ajira na baadaye tufikie lengo la maisha bora kwa kila Mtanzania ambayo tunayatarajia kadri ya ahadi ya Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba, taratibu na mpangilio mzuri ulioletwa kwetu na Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dr. Nagu, nina matumaini mazuri. Lakini ninaiomba Serikali kwa kipindi kijacho cha mwaka 2009/2010 tuweze kuongezewa fedha za kutosha ili taasisi hizi zifanye kazi kikweli. Zabuni mashine mbalimbali kwa ajili ya kilimo chetu, zabuni karakana mbalimbali kwa ajili ya Wilaya na Vijiji vyetu. Tushuke hadi huko chini ambako kuna uzalishaji mwingi kwa kuimarishwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea maonyesho ya Nane Nane hapa Dodoma na nilifika katika Banda la Wizara ya Viwanda na Biashara, nimekuta wajasiliamali wanajitahidi sana kubuni mashine mbalimbali ambazo zina bei nafuu kwa ajili ya wakulima wetu, hata nimekuta wajasiliamali wengine wameweza kuunganisha *wheelchair* moja ya walemavu wakaunga wao wenyewe kuifanya baiskeli ya miguu mitatu. Maeneo mengine kuna watu wanamudu kutengeneza hata aina mbalimbali za

mashine. Mimi nilishauri Wizara hii iongezewe mtaji kwa kuwapa fedha za kutosha hawa watafiti wetu na iwajengee kijiji cha utafiti, maana yake ni kwamba yule muhuzi wa vyuma tangu miaka ya enzi za zamani huko Rukwa aliyesababisha jembe la Chapa ya Mamba likaundwa Uingereza, mfumo wa jembe lile halikutengenezwa na Muingereza; alilikuta tayari limetengenezwa kutoka Ufipa Mkoani Rukwa na yeye akapata soko na jembe lile likawa linauzwa na lina thamani kwenye Bara zima la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watu wengi wenye hekima na elimu tena elimu ya asili ya kutumia vijiti kama vipimo, ya kutumia nyuzi kama vipimo lakini wakaweza kutengeneza *thread* na *nut* na *bolt* kwa viwango kwa cha kupima na kijiti tu bila kutumia zana yoyote ya kutoka nje. Naishauri Wizara ingejenga taratibu maalum na kwa makusudi kuwakusanya hawa wajasiliamali kutoka popote pale ili elimu hii ya asili na ya zamani iweze kukusanywa na kuwekwa katika kijiji kimoja. Kwa maana huyu wa Manyara, mwenye elimu yake aweze kushiriki kuchangia elimu iliyotoka Rukwa. Kwa maana hii tutakuwa tumewaenzi wazazi wetu huko nyuma waliokuwa na teknolojia duni waweze kufikia teknolojia mpya na kuleta maendeleo kwa ajili yetu na kwa ajili ya maeneo mengine yote na wakati huo huo tukawa wabunifu, wenye viwango bora na wazalishaji wazuri wa mitambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Rukwa ni Mkoa uliojitenga sana na upo pembezoni. Sisi ndiyo wazalishaji wakuu wa mazao ya chakula. Ni kati ya Mikoa ile minne *the big four* tunayoizungumzia. Lakini mbolea inatufikia kwa wakati duni, wakati tuna mbolea ya kutosha. Utafiti ulitazamiwa tangu mwaka 1938 kwa ajili ya mbolea tuna hazina ya kuendesha kiwanda kwa miaka 300. Nimezungumza katika Bunge hili mara kadhaa. Nashukuru Wizara sasa kwa kufungua lile blanketi na kuliondoa, nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuonyesha mfano wa kuweza kubuni taratibu na kujenga kiwanda kwa ajili ya Minjingu. Sisi tuna Minjingu kubwa Mkoa wa Rukwa *(Phosphate).* Tafiti zile zilifanywa tangu mwaka 1938, 1952 na zikafanywa mwaka 1956 na watu waliotembea kwa miguu hawa Wakoloni waliotoka Uingereza wakivaa kaptula na patisi. Patisi ni magamba ya ngozi yanayozuia *fellow* lisiweze kuchunwa na miba. Wakati umefika sasa wa kutumia mbolea hiyo, kwa manufaa ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii tunaiomba Serikali sasa ifike kwenye maeneo yetu yanayohusika ili watu waweze kumudu ule utajili wa mbolea. Naona kengele ya kwanza imelia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda nizungumzie barabara iliyopo kutoka Karema kwenda Mpanda na huku ndiko kuna hazina ya madini mengi na huko ndiko kuna hazina ya siri nyingi tu Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Tuna Ziwa Tanganyika ambalo lina samaki aina 54 wa Bahari ya Hindi wamo katika ziwa lile. Nilisema katika kipindi cha nyuma kwamba labda pengine katika maajabu ya dunia kuwa wale samaki walitambaa wakapita Dodoma na wakafika kule Ziwa Tanganyika.

Lakini pengine ni maana ile ile ya dunia kuwa maji na baadaye ikatokea Maziwa na Bahari vikatengana. Tuna hazina kubwa ya samaki, tuna wavuvi kando ya Ziwa

Tanganyika ambao hawana namna ya kuvua mali ile. Tunahitaji miundombinu ya barabara na zana za uvuvi. Ziwa lile ambalo linatutenganisha na Zambia pamoja na Congo na Burundi. Tunasema kwamba taratibu za Wizara kadri zinavyosema Wizara iachiwe nafasi, ibuni ramani maalum kwa ajili ya maendeleo yetu. Kiwanda kiwekwe Karema kwa ajili ya usindikaji wa samaki. Leo Mwanza imetushinda kwa sababu ya samaki wa Sangara aliyetoka Ziwa Tanganyika akapelekwa Ziwa Victoria. Sisi tuna Mabilioni ya tani hayajaguswa bado. Wenzetu wa Burundi wanaingia kwetu na Wazambia wanaingia wanachukua neema zetu wakiwa na maeneo madogo. Naomba sasa kwa makusudi kabisa Mheshimiwa Waziri aweke taratibu ya kubuni ramani maalum kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu.

Mhesimiwa Mwenyekiti, kule Mpanda tuna kilimo cha jetrofa na kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiniona wanasema Mzee wa Jetrofa. Tuna hekta 10,000 tayari, lakini sisi hatujauza ardhi. Kiwanda cha Wajerumani tumekiambia kiweze kununua kutoka kwa wakulima wetu. Kampuni ina mikataba na wakulima wetu. Ardhi tuliyotumia ni ardhi iliyoharibiwa na wakulima wa tumbaku. Maeneo ya ardhi yalitengwa vizuri na vijiji vyetu, tuna misitu ya asili kwa ajili ya mvua na kadhalika. Kiwanda kile kina uwezo wa kukamua tani 40,000 za mafuta kwa mwaka, kitakamilika mwezi Desemba mwaka huu 2008. Kitaajiri wananchi wa Tanzania 100 mafuta yale tayari tumeshakamua kwa kutumia mashine za mkono na wananchi wetu wanatumia kwa taa, wanatumia kwa trekta ndogo. Kwa vurugu hii ya uchumi duniani kutokana na bei ya mafuta, tuna hakika Mkoa wa Rukwa utakuwa na zao la biashara. Mbono unalinda mazingira, mti wake unadumu mika 50, unahimili ukame, mavuno mara tatu. Hekta inazalisha tani nne na bei ni Sh. 500/= kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii, tunaomba utaratibu uliozungumzwa leo asubuhi na Mheshimiwa Makwetta kuhusu kufungua uchumi na kuweka viwanda Reli ijengwe kutoka Mpanda hadi Karema na ni kilomita 120, kuiunga na reli hii ili iwe na uchumi mkubwa kwa kutumia lile Ziwa Tanganyika kwa mazao na biashara kutoka nchi jirani ambayo pia ina utajili na inatutegemea sana sisi huku kwa uchumi wao. Ujenzi wa gati kule Karema, utaleta tija kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru wananchi wa Mpanda Magharibi na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, nawahimiza waendelee na zao letu hili kwa ajili ya uchumi wetu maana ya resi moja ya gari, mafuta yanalika maana yake mafuta yanahitajika. Tuweze kuongoza katika soko hili na wakati huo huo tuna uhakika tutakuwa wazalishaji wazuri wa chakula na tutaendelea kulisha Mikoa mingine ya Tanzania na hata kuweza kuvusha nchi za jirani kama tulivyofanya wakati wa vita kule Congo, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo. Kipekee namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai. Kabla sijaendelea, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda,

Biashara na Masoko aliyewasilisha hapa hotuba nzuri yenye kutupa matumaini na kuona kwamba sasa tunakwenda vizuri. Pia, nampongeza sana Naibu Waziri na Katibu Mkuu na vile vile Mwenyekiti wa Kamati aliyowasilisha hotuba hapa ambayo kwa kweli mengi yaliyozungumzwa ndiyo ambayo tunatarajia yatakuwa majibu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mimi nikianza kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ninaomba twende kwenye ukurasa wa 105 ambapo Waziri alipohitimisha kunukuu ile hotuba ya Rais ya kufungua Bunge letu yeye mwenyewe alituhakikishia kwa msisitizo kabisa anasema: "Wakati umefika wa nchi hii kuacha kuwa *Super Market* ya bidhaa za nje na kuwa nchi ya viwanda yenye kujitegemea, kujitosholeza na iliyo huru kiuchumi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanzia hapo kwa sababu mimi naona nchi yetu imekuwa *super market* ya bidhaa za wengine na hapa ninasisitiza kwamba sio siri tumekuwa tukinunua bidhaa kutoka nje ikiwemo China, bidhaa kama samani za ofisi, samani za majumbani na samani nyinginezo. Wakati huo huo unakuta kwamba sisi Watanzania tuna-*export* mbao na wakati mwingine magogo kwa wingi. Sasa mimi najiuliza kama malighafi ya kutengeneza mali hizo yanatoka hapa Tanzania, halafu sisi tunapeleka nje na sisi tunaletewa bidhaa zao: Je, nini hasa kinachopelekea kufanya hivyo? Lakini baada ya uchunguzi nikaona kwamba ni ule ubora wa matengenezo ya samani hizo na ule mvuto wa macho. Kwa sababu utakuta kwamba kwa ndani sio kweli samani zile zina hali nzuri au zina ubora sana kuliko samani zetu, ila tu wao, katika kutengeneza wanajua kunakshi vizuri na *finishing* nzuri. Sasa nikajiuliza: Je, Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko itatusaidiaje kutatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta hapa nchini una mafundi ambao wangeweza kufanya hivyo, lakini hawajawezeshwa au kuwa na mashine ambazo zinafaa au watu hao hao waweze kusomeshwa vizuri kwenye vyuo vyetu vya *VETA* au vingine na watengeneze samani ambazo zina ubora. Huenda pia kama wakiwezeshwa hivyo lakini hawawezi kutengeneza kwa wingi au hawawezi kuwa na haraka pale mtu atakapotoa *order* yake mara moja inatengenezwa na kupata kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitatoa mfano mmoja. Unakuta umependa kitu labda kinatengenezwa Magereza au kinatengenezwa *VETA*, lakini muda utakaotoa *order* mpaka utakapokuja kupata, hata hamu ya kile kitu au ile thamani imekwisha. Hapa ndani tunao mfano mzuri tu wa hiyo meza ambayo Siwa imewekwa. Meza hiyo, mimi nina uhakika na niliona ilitengenezwa Magereza. Mwezi wa nne mwaka jana mimi nilipopita Magereza wakiwa na mnada, niliikuta hiyo meza, nikavutiwa sana, nika-*order* na mimi vifaa vyangu. Lakini, huu ni mwaka mzima sijaweza kupata vifaa vile. Sasa mimi niseme tu, huenda hakuna uharaka wa kutengenezwa hivyo vitu au hao mafundi hawajawezeshwa na hivyo basi inafanya hata watu wapende vile vya haraka haraka kutoka madukani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiomba Wizara hii iwape kipaumbele wale mafundi wetu wa hapa nchini ambao ni watengenezaji wazuri wa samani wakiwemo hawa wa *JKT*, Magereza, wakiwemo *VETA* au mafundi seremala walio wenyewe katika

vikundi, wawezeshwe ili waweze kufanya haraka matangenezo na kuweza kutoa bidhaa ambazo wananchi wetu wanaweza kupatiwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi pia ninaomba Serikali yenyewe kwenye Maofisi, kwenye Mashirika ya Umma labda au kwenye mahospitali wao wawe ndio soko la kwanza. Sasa hivi ukienda ofisi zote za Serikali ni samani kutoka China. Sasa iweje nyie mnatuambia sisi wananchi tununue vitu vya hapa nyumbani? Leo Mheshimiwa Waziri ametuonyesha kweli amevaa kitenge cha hapa nyumbani, lakini, twende mbali basi zaidi ya nguo, pia zile samani za maofisini zote ichukuliwe kama hatua muhimu, kufa na kupona, zinunuliwe kutoka kwa watengenezaji wa hapa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala la bidhaa zetu hapa nchini kutokuheshimika na kuwekwa kwenye maduka makubwa. Ukienda *Shoprite*, vitu vingi vimetoka nchi za nje. Hapa nyumbani utakuta sisi tuna matunda hayo hayo, utakuta ng'ombe wetu wana maziwa na pia tunayo ambayo yamesindikwa. Lakini pale *Shoprite* huwezi kukuta maziwa kutoka huku nyumbani, utakuta maziwa yote yametoka nje. Ukienda kwenye kuku, utakuta kuku wao wametoka nje, unaambiwa tatizo ni kwamba ubora wa vitu vyetu na *size* yenyewe haiko *uniform.* Kwa hiyo, *Shoprite* hawawezi kuwa na vitu kama hivyo. Sasa mimi niiombe tu hii Wizara iwasaidie basi wale ambao wanaandaa bidhaa hizo waweze kuzifikisha katika ubora unaotakiwa kwenye maduka ambayo ni makubwa ili pia yafungue soko kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba sasa niende katika eneo langu ninakotokea ambako ni katika Mkoa wa Kilimanjaro. Pale Kilimanjaro viwanda vingi viliingia ubia kikiwemo Kiwanda cha Magunia, *KILTIMBER*, kikiwemo pia kile kiwanda cha kutengeneza ngozi. Mpaka sasa kile kiwanda cha magunia hakijazalisha na siyo kweli kwamba kiwanda cha magunia kimekosa soko. Pale tuna zao la kahawa ambalo haliwekwi kwenye aina nyingine yoyote ya *packing* zaidi ya magunia yale ya hewa, magunia ya katani. Sasa magunia hayo kwa sasa yanatoka Morogoro na yanapofikia wakulima pamoja na kile kiwanda au hao wanaokoboa kahawa, yanakuwa ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeyote anayekuja Kiongozi wa Serikali pale Mkoani, kilio cha watu pale, kilio cha wananchi, kilio cha viongozi kupitia kwenye mikutano yetu mingi ya viongozi, *RCC* na mingineyo, unakuta kilio chetu kikubwa ni viwanda. Viwanda vile vimefungwa, sasa hivi hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba mbia kama yule aliyechukua kiwanda cha magunia, endapo haendelezi kile kiwanda kabisa, wananchi waelezwe kwamba hiki kiwanda kimefungwa na hakiendelezwi tena, kwa sababu kuona lile jengo pale kama gofu, sisi kwetu linatuletea hasara na pia linatupa uchungu. Basi litolewe kwa watu wenye biashara nyingine ili mambo mengine yafanyike. Hivi majuzi tu tuliona lile jengo la bia ambalo lilikuwa ni Kibo *Breweries* limetolewa na wenzetu kwenda kwenye taasisi ya dini na hiyo sasa imekuwa ni jambo jema kwa sababu itakuwa ni Chuo Kikuu cha Mambo ya Tekinolojia. Endapo hicho cha magunia basi hakitafanyika tena kuendelezwa, tunaomba tuambiwe hatima yake na tujue ni nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viwanda hivyo ambavyo haviendelezwi, lakini pia tungependa tujue kilichokwamisha ni nini, kikiwepo kile kiwanda cha ngozi. Kuna mfanyabiashara mmoja ambaye yeye anaendesha kiwanda *private*, *Shaha Industries*, amekuwa akifanya shughuli hiyo kidogo kidogo na hajakwama na ametoa ajira nyingi tu na hasa kwa walemavu. Mfanyabiashara huyu ametuhamasisha sana pale Mkoani. Yeye ameweza kubuni na anaendeleza. Sasa hicho cha ngozi kwa nini kisiweze kushamiri kama ilivyokuwa? Endapo wakati ule kikiwa *SU* kiliweza, sasa hivi hawa waliokuja kuwekeza inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda kama hivyo ndivyo vinavyotoa ajira pale Mkoani. Pale Mkoani Kilimanjaro sasa hivi hakuna viwanda vingi pamoja na kwamba kuna kimoja ambacho naomba hapa nikipongeze, ni kile kiwanda cha Sukari cha *TPC*. Hicho ndiyo kiwanda peke yake ambacho sasa hivi kinakwenda vizuri baada ya kubinafsishwa na kinatoa ajira takriban 4,000 kwa watu wetu kutoka nje ya Mkoa na ndani ya Mkoa. Hicho ni kiwanda pekee cha mfano ambacho kiliweza kubinafsishwa na bado kinakenda vizuri. Sasa tungeomba basi wengine wote waweze kuiga viwanda kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi hizo kwa *TPC*, ninaomba, wako wajasiriamali au wako wawekezaji binafsi walijituma na kuweka viwanda vyao kikiwepo kile kiwanda pale Himo, kiwanda cha kusindika matunda na mboga mboga. Mwanzoni tulielezwa kwamba ni kmiwanda cha kusindika nyanya. Kiwanda hicho ni kizuri, jengo hilo ni zuri, lakini nadhani imefikia mahali yule mwekezaji naye pia nguvu zikamwishia au hakupata *support* ya Benki na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na akina mama wa Kilimanjaro tunaomba, kwa vile kiwanda hicho kingekuwa mkombozi wa akina mama kuuza nyanya zao na kuona kwamba wanapata kipato, mwekezaji kama huyo afuatiliwe ili ifahamike amekwama nini, nini anaweza kusaidiwa ili amalizie jengo lake na shughuli hiyo iweze kuanza. Tukiona tu kwamba mtu kama huyo amekwama na sisi tukamwachia tukijua kwamba aha, hii ni shughuli yake mwenyewe, ikishafikia hapo, Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwi tena shughuli ya mtu ila inakuwa ni shughuli ya sisi wote.

Ninatoa rai hii kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko iweze kufuatilia wawekezaji kama hao wenye upendo na nchi yao, walioweza kupata mtaji nje, wakaja labda kuwekeza nyumbani na sasa labda wamekwama kidogo, tuweze kujua tutawasaidiaje watu hao ili waweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kengele ya pili haijagonga, ninaomba pia wakati wanajumuisha, Wizara iweze kunieleza ni jinsi gani uhusiano wa *SIDO* na shule za *VETA*, yaani *SIDO* iweze ku-*sponsor* watu waende kusoma *VETA*. Utakuta kwamba *SIDO* ni katika Viwanda vidogo vidogo na inapata msaada kutoka Serikalini au inapata fungu kutoka Serikalini, lakini sasa *VETA*, watu wengi wangependa kujiunga na *VETA*, lakini wengi inabidi wajilipie wenyewe na wao hawawezi, siyo wote wanaoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe basi uwepo utaratibu rasmi wa watu ambao wanapenda kujiunga na *VETA* ambao wana shughuli zao wenyewe, *SIDO* iweze kuwadhamini watu hao waweze kujiunga na *VETA* ili watakapotoka sasa wawe wamehitimu wakiwemo hao wa kuweza kuendeleza bidhaa za mbao, wakiwemo hao wengine wa shughuli mbali mbali, lakini, *SIDO* isimamie mafunzo hayo na iweze kuwalipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa tu nisisitize kwamba endapo tuna ule Msitu pale Rongai na sisi tunatoa mbao na mbao hizo kiwanda chetu cha Kilimanjaro *Timber Utilization* kimefungwa na sasa hivi hatuna ambako vijana wetu watafanya kazi na pia tunapata shida sana. Ninaomba kwa dhati kabisa kwa kilio kilicho katika Mkoa wangu, Wizara hii, nikisisitiza tena na nikiomba kwa vile imekuwa ni kilio cha wengi na ni kilio cha Mkoa mzima, iweze kuona ni jinsi gani mbao zile badala ya kusafirishwa au kupelekwa nje au kwingineko na sisi wenyewe pale Kilimanjaro tuweze kuona tena uhai wa kiwanda kile ambacho miaka ya nyuma kilikuwa kinaongoza na maeneo mengi yalikuwa yananunua samani.

Jambo moja zuri tu ni kwamba, kuna soko ambalo ni la kudumu kutoka kiwandani pale, yakiwemo makanisa, kwa sababu siyo rahisi ukute makanisa yanakwenda kununua samani zao, yaani mabenchi yale kutoka nje. Kwa hiyo, hapo ni soko la uhakika. Siyo kanisa tu, shule, vyuo, siyo rahisi sana uone mabenchi wanayokalia vijana wetu yanatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nikiamini kwamba Wizara hii ina nguvu, inao viongozi waliobobea, wote ni madaktari, inao pia wengine watendaji ambao wana uwezo mzuri, ikiisha bajeti hii tuweze kupata sasa mwanga, tujue vile viwanda vilivyofungwa au vile viwanda vilivyobinafsishwa na havizalishi, badala ya watu kuja kufungua zile mashine na kupeleka kwingine, iweze sasa kufanyika shughuli pale pale Mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja tena! *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ambayo ni muhimu katika kuendeleza uchumi wa nchi hii. Mimi ninayo machache sana ya kuzungumza, lakini nadhani ni muhimu kama elimu ili tuweze kuelewa. Nazungumzia *from practical experience* na siyo kama mwanasiasa ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza uchumi wa nchi, tunahitaji kitu kimoja ambacho Tanzania tulikuwa nacho lakini tumekiacha, nacho ni *Venture Capital*. Tunahitaji *Venture Capital* katika kila Mkoa ili tuweze kufufua uchumi. Labda kama ninapozungumzia *Venture Capital*, sisi Waafrika au sisi Watanzania kwa ujumla wetu tuna mapungufu yetu. Unapokwenda Benki kukopa kwa ajili ya kutimiza mradi fulani, badala ya kufanya ule mradi, wengi wetu tunakwenda kuoa wake wa pili, tunakwenda kujenga nyumba nyingine, tunakwenda kufanya miradi mingine na inatufanya pesa

tulizokopa haziwezi kufanya kile tulichotaka kufanya cha maendeleo kama ni kiwanda au kama ni kitu kingine cha namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa na *Venture Capital,* wale wanaotoa zile pesa wanakuwa *more or less* kama *partner* katika ile kampuni, wana-*sit on the Board*, wanahakikisha pesa zilizochukuliwa ambazo ndio wamekopesha, zinatumika kwa mradi ule na hazitumiki kwa ajili ya jambo lingine. Watanzania wengi tumeshindwa kufanya biashara kwa sababu ya kutokufuata maadili ya biashara. Unakopa pesa za kujenga kiwanda, badala ya kujenga kiwanda, unaoa mke wa pili katika pesa zile zile, badala ya kiwanda, unakwenda kujenga nyumba maana ulikuwa huna nyumba, baada ya hapo, unakwenda kumsomesha mtoto pesa zile zile, una mtoto wa mjomba, una nani, pesa zile zile; ni kwamba kile kiwanda hutakaa ukijenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapokuwa katika *Venture Capital*, *Board* haitakuruhusu kutumia pesa zile kwa matumizi mengine. Wale wenye pesa kwa kuwa watakuwa kwenye *Board*, watahakikisha pesa zile zinatumika kwenye mradi ule na wanakaa kwenye *Board* mpaka wakati wakishaona kweli kitu hiki kinasimama imara, wanaweza kuwauzieni zile *share* zao au wakaondoka wakaona kweli hii kazi tumefanya ni nzuri. Hilo ni jambo ambalo ni lazima Watanzania tujifunze na Serikali ianze ku-*create Venture Capital*, Mabenki yanayotukopesha yajue *what is Venture Capital*, wajue namna ya kutuendeleza kwa sababu *interest rate* za Benki kama utalipa ile *interest*, ni vigumu sana uweze kutimiza masharti ya Benki na uweze kumaliza kama ni kiwanda au ni chochote kile unataka kufanya na ndiyo kinachotulemaza na kinatupa taabu, tunashindwa kuendelea katika viwanda katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vimekuwa ni vya watu wa nje na Serikali imekuwa inalinda hiyo. Lakini, *through Venture Capital*, nina hakika Serikali itaweza kusaidia wazawa wa nchi hii waweze tena kufufuka na kuweza kufanya biashara. Nitakupeni mfano. *Precision Air* inaendelea vizuri na inatoa huduma, inashindana hata na *Air Tanzania*, ilianza na *Venture Capital*. *Precision Air* ilianza na *Venture Capital* na ndio maana iko inaendedelea, nina hakika. Sina hakika sana, nadhani hata *TATEPA* ile ya kule Iringa ambayo inafanya vizuri sana, imeanza na *Venture Capital* ambazo ndiyo tulitakiwa tu-*create* katika kila Mkoa, tuweze kufufua uchumi, tuweze kufufua makampuni ambayo ni ya wazawa ambayo yatawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, nawaambia Serikali, tunapochukua pesa, tukatawanya kama karanga Tanzania ati tunatoa kwenye *SACCOS* na tunatoa Kwa Machinga, hii nchi tunaiharibu. Serikali inaangalia *top layer* - wawekezaji, halafu inakwenda chini kwa Machinga, inasahau hapa katikati ambapo ndio kuna wafanyabiashara ambao ndio wana-*create employment* ya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pesa zote zilizokuwa zinaitwa za Mheshimiwa Kikwete, hazitarudi. Anayeniambia zitarudi, ninamshangaa. Watu wanasema ilikuwa ni zawadi ya uchaguzi. Hakuna mtu anarudisha na siyo kosa lao, tabia ya Watanzania yenyewe pamoja na Serikali yake haina tabia ya kulipa madeni mpaka tunasamehewa. Sasa unataka kuniambia Machinga atakopa, alipe kwa sababu gani?

Kama Serikali hailipi madeni, Serikali ikikopa hailipi, mimi mtu mmoja wa Kitanzania unaniambia nikope, nilipe kwa sababu gani? Ndio sababu hawalipi! Ndivyo tulivyojijengea sisi Serikali yetu! Kama Serikali ingekuwa na maadili ya kulipa madeni na watu wake wangekuwa na maadili ya kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pesa tunazopeleka, unampa mtu shilingi 50,000 au 100,000, unamwambia akaanze mradi, ni mradi gani na *interest* anayolipa katika zile pesa? Ni mradi gani atakaoanza na pesa zile? Mimi ni mfanyabiashara, lakini nataka kujua tu, unampa mama shilingi 50,000, nenda kaanze biashara ya kuuza karanga. Mimi wanakuja kwangu, kwa kuwa mimi ni Mbunge, wanashindwa, wanakwenda kuchukuliwa vitanda nyumbani, *SACCOS* hizi! Watachukuliwa, maana yake ni kuwauza kabisa. Ni hatari hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema na nimesema kwenye Bunge hili mara nyingi, Serikali, tutafute namna ya kuwafanya watu wachache wawe matajiri, waweze ku-*create employment*. Watanzania wanataka chakula! Kuondoa umaskini ni watu wapate *employment*, siyo kufanya kila Mtanzania mfanyabiashara, hiyo ni uwongo, *it's a wrong philosophy, very wrong!* Kila Mtanzania afanye biashara! Haiwezekani! Lazima tuwe na wachache ambao watakuwa na viwanda, watakuwa ndio wafanyabiashara na wata-*create employment*, wengine wafanye kazi waweze kuwasaidia wale wengine. Nadhani kwa *Venture Capital* hilo nimezungumza vya kutosha. Labda nirudi katika Jimbo langu la Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Moshi mwaka jana katika bajeti wakati ule Mheshimiwa Basil Mramba akiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, nilitamka kwenye Bunge hili, viwanda vya Moshi ambavyo vimeshindwa kufufuliwa au haviendeshwi, nipeni mimi Ndesamburo. Nikawaambieni nina kiburi, hiyo na nina uwezo wa kuweza kuvifufua na vikafaa na wananchi wa Moshi wakapata kazi. Mimi nashangaa mpaka leo hakuna mtu amenipa hata kimoja. Hivi Serikali ilifikiri ninasema uwongo Bungeni? Mimi sisemi uwongo! Kama Serikali imeshindwa, nipeni mimi nitavifufua, nataka watu wangu wa Moshi wapate kazi! Nataka watu wa Moshi wapate kazi na uchumi wa nchi hii uendelee. Watu wote wakishapata, vurugu nchini hakuna na pesa zetu ni halali tunafanya kazi kwa jasho, siyo za ufisadi jamani! Naomba tuelewe hili. Tuna matajiri Tanzania ambao wanasema ni matajiri, lakini wote wezi. Wengi wa hawa watu ni wezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameanza kufumka mambo machache hapa Bungeni, tumeanza kusikia jinsi watu walivyokuwa wanaiba katika Serikali na tunawaona ni matajiri, tunawaheshimu. Sasa siwaheshimu tena! Kumbe siyo watu waliokuwa wanafanya kazi ya kusaidia nchi, wao walikuwa wanafilisi nchi. Unapofilisi nchi halafu ukasema unasaidia nchi, sio kweli ni uwongo! Kwa hiyo, hawa watu tunaowalinda hao, tunaosema ni wawekezaji ambao ni mafisadi, wananyonya nchi hii, wanatuharibia nchi, wanatumaliza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, kama mmeshindwa viwanda vya Moshi, Serikali, nipeni Ndesamburo, mimi nitaleta wawekezaji, tutavifufua vyote. Ni mwaka

mzima nimesema na huu narudia tena kauli yangu mwaka wa pili. Sisemi kwa ajili ya siasa wala kwa ajili ya kutaka kujitakasa au kujifanya *famous*, hapana, nataka watu wa Moshi wapate kazi. Moshi imekuwa Mji wa mwisho kwa kuendelezwa, viwanda vyote vimefungwa. Nashukuru Mungu *KKKT* imeona heri ichukue hata kile kiwanda cha bia, ifanye *University* ya kuleta watu wasome waendelee. Lakini, sidhani kama ile *Council* ya Moshi au tuseme Serikali inaona uchungu wa Moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza katika Bunge hili, nikasema tunataka kufufua biashara, Kenya imeendelea katika biashara, Kenya iko mbele na mali nyingi zinazotumika Tanzania zinatoka Kenya. Nikasema kwa nini hatufungui reli ya kutoka Mombasa kuja Moshi tuka-*create inland depot* pale Moshi ambayo inge-*create employment* na kuleta biashara kubwa? Hakuna mtu amenijibu na ile reli tumefunga, wanakuja nayo mpaka pale mpakani kwetu Tanzania ambayo ni kilomita 15 tu imebakia tufike Moshi. Tumefunga ile reli, tumeifunga kwa manufaa ya nani? Kwa nini hatuwatakii mema wananchi wetu? Au Moshi ina dhambi gani? Kwa nini tusiiendeleze ile reli itoke Mombasa ili mali yote ya Tanzania ikatoka na reli kwa bei rahisi, ikija Moshi tukachukua hapa kwa urahisi? Hata Burundi wangekuja kuchukulia pale Moshi hata mpaka Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hiyo ipo, lakini tunaiacha inaoza. Hivi tumepungukiwa akili au tumepungukiwa maarifa? Nazungumza haya kwa uchungu kwa sababu mimi natoka Moshi, naona watu wa Moshi wanavyoteseka, naona jinsi Moshi inavyokufa na inauawa kwa makusudi kwa ajili ya itikadi. Ni itikadi tu! Lakini watu wa Moshi ni watu wazuri sana, wanaopenda kufanya kazi na uwezo wanao na biashara wanajua, lakini hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana! Inasikitisha ninapofikiria mambo haya, yananipa taabu sana. Inanipa taabu kubwa! Kweli kama tunataka viwanda na tunataka kusaidia Watanzania kwenye biashara, Serikali ifikirie upya namna ya kuinua wafanyabiashara wa Tanzania, namna ya kuwasaidia Watanzania ili waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna pesa, siyo za kutupa, pesa tulizonazo Tanzania ni nyingi, tunaambiwa tuna pesa nyingi, lakini tunakosa *management*, tunakosa *thinking capacity* ya kuweza kufanya watu wetu washibe. Kwa nini tunakosa *thinking capacity*? Tuna wasomi wazuri, tuna watu wengi ambao wanajua, lakini ni nini kinatufanya tunafikia kiwango hiki? Tunakuwa Taifa la kuomba omba, tunakuwa Taifa tunajiita maskini badala ya kuwa na kiburi cha kujiita matajiri sisi, tunajiita sisi ni maskini kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *psychologically* ukishajua wewe ni maskini, utakufa maskini tu. Lakini lazima tu-*create environment*, mawazo ya watu wa Tanzania wajivune waone wao siyo maskini. Lakini hii kuwabeza kila siku, nyie ni maskini na ndio maana kila siku wanasema sisi omba omba. Tutafute njia ya kubadilisha *mentality* ya Watanzania, tutafute namna ya kuwafanya wawe na fikra tofauti za kutokufikiria sisi ni maskini wa kubebwa. Hii tabia ya Serikali kugawa pesa kama korosho, kama karanga,

iachwe, ni mbaya, inalemaza watu. Hata mtoto wako kama unambembeleza bembeleza, siku moja atakuja kukurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Serikali inalemaza watu! Badala ya kufanya uchumi ukue, inalemaza uchumi wa nchi hii. Sitasema mengi zaidi ya hayo, naomba nimalize hapo. Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana! Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao haumtoshi mchangiaji anayefuata kuweza kuchangia. Lakini nitapenda niwatangaze wachangiaji watano watakaochangia jioni: Kwanza kabisa, nitamwita Mheshimiwa Janeth Massaburi, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum na pia atafuatia Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro pamoja na Mheshimiwa Benito William Malangalila.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo, napenda nisitishe shughuli za asubuhi leo mpaka saa 11.00.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa ruhusa ya kuweza ya kuwa mtu wa kwanza kuongea katika kikao chetu cha Bunge jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye ananipa kibali cha kuweza kuzungumza kwa kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu rafiki yangu sana, Watendaji wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ingawaje wanaifanya katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie yafuatayo. Nitachangia kuhusu viwanda vya kubangua korosho, viwanda vya ngozi, viwanda vya kusindika alizeti na viwanda vya kusindika maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na korosho, mwaka 2007/2008 Tanzania ilizalisha tani zipatazo 98,272 za korosho ghafi, asilimia 20 kati ya hizo ndizo zilizouzwa nje ambazo zilikuwa zimebanguliwa na asilimia 80 ghafi, hali hii inasaidia sana kuzorotesha hali za wakulima wa korosho na mazao mengine kutokana na ubora kuwa mdogo, thamani kuwa ndogo, yote hii ni kwa kutozitilia maanani umuhimu wa viwanda vyetu na hasa viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika mazao ya ngozi, mwaka 2006 mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi ilikuwa ni tani 8,998 sawa sawa na vipande 750,000 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 7.84 na ngozi iliyosindikwa kwa mwaka 2006 ambayo imeuzwa nje ya nchi ilikuwa tani 3,178, thamani yake ilikuwa shilingi bilioni 5.352.

Mwaka 2007 ngozi iliyouzwa nje ya nchi iliyosindikwa ilikuwa tani 5,566 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 16.035. Wastani wa ngozi inayosindikwa kwa nchi yetu inauza kati ya asilimia 35 mpaka 40. Sasa hapo angalia tofauti ilivyo kubwa ambayo tunapoteza kiasi kingi sana cha fedha ambayo inaathiri pia wakulima na wafugaji wa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hali hii tutaendelea nayo mpaka lini? Katika mipango, wataalamu wetu wameandika mipango mizuri sana na hotuba ni nzuri sana sasa utekelezaji ni lini? Ukizingatia, mara nyingi tunahimiza kwamba tunahitaji wawekezaji, lakini hawa wawekezaji wa ndani tunawaangalia vipi kwa haya mazao ambayo nimeyaongelea machache tu. Kwa nini tusiongeze bidii katika kuwawezesha wenye viwanda vya kati ili waweze kuboresha bidhaa zao? eneo hili ndilo linalotoa ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nitoe mfano, wiki tatu zilizopita tulikuwa kwenye mkutano Nairobi, katika vitu vilivyotumika kama *folder* na *briefcase* zilikuwa zimetumika ngozi za wanyama kama ng'ombe na ngozi hizo walikuwa wametengeneza vijana wa pale Nairobi. Sasa utaangalia nchi ile jinsi inavyowapa umuhimu vijana wao, lakini sisi tukiwa na mikutano ya ndani na nje, kuna mikutano mingi ya kimataifa hapa nchini na ya ndani sana sana utakuta tunaagiza bidhaa kutoka China. Mimi sielewi tunapiga kelele uzalendo, kwa nini tunapenda kung'ang'ania vitu vya nje? Kwa nini hatujali bidhaa za ndani? Tukiwawezesha vijana hawa na viwanda vyetu uzalishaji utakuwa mkubwa na bei itakuwa ndogo. Maana yake hapa tutakuwa tunasingizia kwamba bei zetu ni ghali, hawana uwezo, uzalishaji ni mdogo na ndiyo maana gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tuache muda wa kuongea mikakati, mipango Mikakati muda huo umekwisha, tunaomba vitendo tuwezeshe viwanda vyetu vya ndani vya kati. Tunakaribisha wawekezaji, sawa, lakini hawa watu wa ndani, wenzetu China walijali sana soko lao la ndani, sisi tunawaza nini? Tununue bidhaa nje zije ndani, badala kutilia nguvu tutengeneze bidhaa za ndani ili tuuze nje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupe mfano kidogo, naomba mnivumilie. (*Hapa alionyesha vielelezo*) Mkoba huu ni ngozi ya pundamilia, inatengenezwa na viwanda vyetu vya ndani na bei yake ni kati ya Sh. 40,000/= mpaka Sh. 90,000/=, huu hapa unatoka nje ya nchi bei yake ni Sh. 300,000/=, ni ngozi ya Chui, hakuna tofauti. Sasa tutasema ni usindikaji! Basi tuwaite ndugu zetu ambao tupo karibu nao Wachina waje kuwekeza au waingie ubia na wenye viwanda vyetu waweze kutengeneza bidhaa ili waweze kuuza nje. Tuna wanyama wengi sana nchi hii, hatuna umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema kwamba sisi tuna umaskini wa kufikiri, lakini tuna viwanda, watu wapo na rasilimali zipo za wanyama, kuna wanyama wa aina mbalimbali na ni wazuri sana, kuna viatu vya ngozi za sangara, mamba, chatu na wanyama wengine wa kila aina, lakini hawa majangili wanaiba wanakwenda kuuza kisha wanarudisha, tunanunua sisi wenyewe, wanyama wetu wenyewe halafu tunawanunua. Kwa kweli hali hii inabidi tuiache tuwe wazalendo, tuipende nchi yetu. Mikoba sijui ya kitu gani imetoka wapi! Tuwape nguvu wenye viwanda vyetu ili waweze kutengeneza tutumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani kila siku tunakwenda kwenye semina Jumamosi, tunapewa ile mikoba. Kwa nini ile mikoba isitengenezwe na vijana wetu? Naomba kwa kweli suala hili litiliwe maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, nilitembelea hizi kampuni za kutengeneza bidhaa za ngozi, kuna kiwanda kinaitwa *Himo Tenary*, *J.A Tanzania Ltd, P.M Titos, Italy Shoe Limited, Urono Leather, Shah Indusries, Open Summits,* Magereza, kuna Mwanza, Moshi, Dar es Salaam, Kibaha na Moshi Magereza, viwanda hivi vyote vinatengeneza viatu, mikoba, mikanda, *Jackets*, ukiiona huwezi kuamini kama hii ni kweli imetengenezwa Tanzania. Kwa kasumba yetu, huwezi amini kama imetengenezwa Tanzania, lakini wanatengeneza hawa watu! Ni nani atawasemea na nani atawasikiliza? Tunaomba Mheshimiwa Waziri waangalie hawa watu waweke kwenye *umbrella* moja waweze kutusaidia na kuweza kuinua uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee viwanda vya kusindika alizeti. Katika ukanda wa Singida, Dodoma ardhi inakubali sana na linastawi sana hili zao la alizeti. Alizeti ni mafuta ambayo ni bora yanayotumiwa na matajiri duniani, kwa nini tusiyape nguvu mazao haya? Kwa nini tusiwawezeshe tuamue tu Dodoma, Singida peleka nguvu kwa wakulima walime alizeti wapelekee viwanda vidogo vidogo, akina mama na vijana wapate ajira? Hii nayo tunahitaji mwekezaji? Kwa kuwa sisi hatuwezi kuwekeza, kwanini tunategemea wawekezaji kutoka nje? Tunaomba wawekezaji waje wajiunge na vikundi vyetu huku tuingie nao ubia, lakini vilevile sisi pia tunaweza, hii ni teknolojia ndogo sana na ni rahisi, haihitaji maarifa makubwa sana, lakini *SIDO* inafundisha kuhusu usindikaji na utengenezaji wa mafuta. Naomba sana Mheshimiwa Waziri au naiomba Serikali iangalie eneo hili. Siyo lazima Tanzania nzima tulime alizeti, twende maeneo machache tu tupeleke nguvu tutaona matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee viwanda vya kusindika maziwa. Sisi Tanzania tuna bahati, tuna viwanda kwa mfano, Tanga *Fresh*, Iringa kuna kiwanda cha maziwa, Arusha, Mara maziwa mazuri sana nimesikia sasa hivi wanauza Kenya, kuna viwanda vingi katika kila Mkoa, Mwanza, Shinyanga lakini tunaviangaliaje hivi viwanda vyetu? Kwa nini hivi viwanda tumeviacha kama kuku wa kienyeji, vinajichunga vyenyewe? Uwezeshaji maana yake nini? Uwezeshaji ni mgeni kutoka nje ambaye anasamehewa kodi, lakini hawa tunawaangaliaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwajengee mazingira ambayo yanafanana na zile kodi ambazo tunawapunguzia wawekezaji wa nje ili hawa watu wenye viwanda vya maziwa

waweze kufanya vizuri na soko lao la ndani na nje liweze kupatikana. Mimi nafikiri tuna kasumba tu. Maziwa ni mazuri nafikiri labda ile *packaging*, basi tuwaite watu waje kuwekeza watengeneze kiwanda kwa ajili ya vifungashio. *Supermarkets* zimejaa maziwa ya Afrika Kusini, maziwa yanatoka Arabuni, Arabuni wanafuga ng’ombe, lakini wale wame-*pack* tu, hawana mashamba. Sasa hivi vitu vidogo navyo vinakuwa ni taabu! Mimi sielewi tatizo ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ajira hakuna. Ajira ipo, mazao tunayo, watu tunao, mipango iko kwenye makaratasi; utekelezaji, watu hawana maamuzi, tunangojea Rais ndiyo atoe maamuzi. Si tutamuua? kazi anayofanya ni kubwa sana. Anategemewa na dunia, lakini ana wasaidizi wake, tufike mahali tuwe na maamuzi, kama ni mabaya mwanadamu hajakamilika kama ikitokea bahati mbaya ni mabaya basi tunarekebishana. Mimi nafikiri pale kila mtu akitimiza wajibu wake nafikiri tutakwenda, lakini mimi naona kosa ni kutokuwa na maamuzi, tunaogopa lawama. Una dhambi gani unaogopa lawama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia naomba nichukue fursa hii niishukuru *SIDO* na *TIRDO*. Hizi Taasisi kwanza hazina hela, kuna watu wanasema tunataka *SIDO* sijui itupe nini, hela, hawana ni maskini wa kutupwa, wanapiga kelele tu hawana kitu *SIDO*. Mimi ni kiguu na njia kwenye *SIDO* naongoza, wanahitaji msaada ili waweze kufanya kazi na hao ndiyo mkombozi, itasaidia *VETA*, kuna wale wa *VETA* watakwenda kusoma kule lakini *SIDO* yenyewe itakwenda kule kwenye *grassroot* na tumsifie Mwalimu Nyerere kwamba wazo lake lilikuwa ni jema Mungu amrehemu, alikuwa na wazo takatifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* imekaa kama mtoto yatima. Waheshimiwa siku moja mfanye ziara mkatembelee *SIDO* na *TIRDO* ndiyo mtajua mawazo ya Mwalimu Nyerere alikuwa anawaza wapi? Mwalimu Nyerere alikuwa na mawazo ya miaka 200 ijayo, lakini ukienda pale inasuasua tu, *SIDO* wanaweza wa kufunza watu kutengeneza bidhaa za aina zote. Kule *supermarket* ambako zimejaa bidhaa za nje, *SIDO* wana uwezo navyo vyote. Lakini sisi kwenye *supermarkets* zetu kuna bidhaa za kutoka Uarabuni ama Afrika Kusini; hivi kuna nini? Mimi nashindwa kupata jibu, sielewi kwa nini tunang’ang’ania bidhaa za nje, mbona sisi tukienda *South Africa* hatukuti bidhaa za Tanzania madukani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi ya kuzungumza mchana huu. Nilikuwa nimeshachangia kwa maandishi, kwa hiyo, nimeshawapongeza Mawaziri na Watendaji wote. Sasa niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Halmashauri yangu ya Wilaya ya Same. Nilikuwa sijapata nafasi ya kuipongeza Halmashauri yangu ya Wilaya ya Same na kwa kipekee kabisa nampongeze Mkurugenzi wangu ambaye baada ya malalamiko mengi ya wananchi wa Same kuhusu zao letu la

Tangawizi aliweza kuhangaika mpaka sasa ninapozungumza wananchi wa Tarafa ya Mambavunta wanajenga kiwanda chao wenyewe cha kusindika Tangawizi ili waweze kuiuza Tangawizi ikiwa imeongezwa thamani.

Naomba kupitia Bunge hili niwaambie wananchi wangu wa Tarafa ya Mambavunta kwamba wafanye bidii sana katika ujenzi wa kiwanda hiki kwa sababu ni mali yao na ndiyo itakuwa mkombozi wao, wasijisikie kwamba wapo peke yao, lakini wawe na uhakika kwamba wapo na Mbunge wao pamoja na hayo wapo pamoja na Serikali Kuu kwa sababu nina uhakika wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha Dada yangu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu atazungumza neno zuri la kuwatia moyo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya kiuchumi humu duniani yalianzia Ulaya. Kama ukisoma histortia ya uchumi na ilikuwa ni karne ya 14 mpaka karne ya 17. Wenzetu Ulaya walikwenda mwendo tunaokwenda sisi wa kuuza mazao yakiwa ghafi, wakagundua kwamba wanazidi kuwa maskini, wakaondoka kwenye kuuza mazao ghafi wakaingia kwenye viwanda ndipo maendeleo ya kiuchumi yalipoanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameanza Ulaya, wakaja Marekani ya Kusini, wakaja Marekani ya Kaskazini, Australia, Asia mpaka sasa hivi ni kitu ambacho kipo mwenye mwendelezo, lakini sisi Tanzania tuzungumze kwa ukweli kwamba tumejikita mno kwenye kuuza mazao ghafi na hapo ndipo umaskini wa Mtanzania ulipolalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania hatakaa akombolewe na Serikali kama ataendelea kuachwa akilima na auze mazao yakiwa ghafi. Naiomba Serikali ifike mahali ikubali mabadiliko na mabadiliko ni magumu na yana misukosuko, lakini unapotaka kuleta mabadiliko, ukiweka nia kamilifu na ukiamua kuthubutu na ukifanya kazi kwa bidii hakuna kisichowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama imeamua kweli kumkomboa Mtanzania maskini, mkulima, ihakikishe inaingia kwenye mfumo wa viwanda ili wananchi wake wauze mazao ambayo yameongezwa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mazao mengi, tuna kahawa, chai, katani, mbuga, matunda na tangawizi. Same inaongoza kwa tangawizi, lakini tukimwachia Mtanzania akiendelea kuuza mazao ghafi zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima tutawafanya waendelee kuwa maskini mpaka mwisho wa dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze na Serikali Kuu kwa sauti kidogo tofauti, tuanze operesheni ya pamoja, operesheni ya kuingia kwenye mabadiliko ya uchumi wa Tanzania, Serikali Kuu siyo kwamba ifanye mabadiliko haya peke yeke, tuungane na *Local Government* na sisi wenyewe Wabunge pamoja na wananchi wetu, tuamue kwamba sasa tunabadilisha mfumo wa uchumi, tunatoka kuuza mali ghafi tunakwenda kwenye viwanda vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la viwanda, naomba nizungumze ukweli, hatuwezi kumkwepa *SIDO!* Hatuwezi kumtenga *SIDO*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sido ilianzishwa kisheria na ilipoanzishwa nakumbuka sina uhakika, lakini nadhani aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara alikuwa ni Mheshimiwa Cleopa Msuya na madhumuni ya kuanzisha *SIDO* ilikuwa ni kwamba *SIDO* ifanye kazi ya kusindika mazao ili iongeze thamani mazao ya Mtanzania, imwondoe kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nailaumu Serikali Kuu kwa sababu madhumuni ya *SIDO* ambayo sisi wenyewe tulisema, hayatawezekana hata kidogo kama *SIDO* wakiomba shilingi bilioni tano tunampa shilingi bilioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa nguvu zangu zote kwamba naishukuru sana *SIDO*. Mimi sasa hivi nipo kwenye harakati za kujenga pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Same na wananchi wangu kupitia ushirika wao tunajenga kiwanda cha kusindika Tangawizi, tumepata soko nchi za nje lakini mitambo yote tunaitoa *SIDO*. Hivi mnavyoona tunavyohangaika mimi na wananchi kila siku naondoka Jimboni nipo na *SIDO* ndiyo watakao-*supply* mitambo yote ya kiwanda hicho leo tunamweka *SIDO* kando, anaomba shilingi bilioni tano tunampa shilingi bilioni moja na wakati yeye ndiye atakayenipa mimi Anne Kilango mitambo ya kuweka kwenye kiwanda cha wananchi wangu Same Mashariki, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Mheshimiwa Waziri inabidi arudi kwenye Baraza la Mawaziri ili *SIDO* waongezewe hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Wilaya zote zina uwezo mkubwa wa kushirikiana na wananchi wa kuhamasisha wananchi kuunda usharika na kujenga viwanda vya kati vya kusindika mazao kule ambako kuna mazao ambayo yanahitaji kusindikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumze hivi kwa sababu nimeona manufaa yake, kile kiwanda ambacho kinajengwa pale Tarafa ya Mambavunta kimetokana na Halmashauri yangu ya Wilaya ya Same na mimi Mbunge nikaingia pale kwa nguvu zangu zote na wananchi wakaunda ushirika, *SIDO* akaja akatuonyesha kila kitu, mafunzo yote tumepata kutoka *SIDO (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* kama wapo hapa watajua tumeingia mkataba wa kuleta mitambo kwenye kiwanda kile. Ni kitu kimoja tu ambacho *SIDO* wamesema hawataleta, lakini watachukua kutoka Uholanzi lakini ni wao ndiyo watafanya hivyo. Ninaiomba Serikali ione kwamba ni muhimu sana kuiwezesha *SIDO* ili iwakomboe wakulima maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo sina ugomvi na wawekezaji lakini naomba nizungumze ukweli. Tunazungumzia sana utandawazi, wawekezaji, sisi ni Taifa dogo, wananchi wetu ni wakulima, nakubali. Ukienda Tanga ama kama unapita njia ya Tanga, machungwa mengi yanaoza. Ukienda Geita mananasi mengi yanaoza, lakini mimi naomba nitoe mawazo yangu kama yangu maana hatuna sare katika kufikiri, kwamba ni vyema tukaenda kwenye viwanda vya kati vya wananchi wenyewe, wajiunge katika

shirika, Serikali Kuu nayo iweke mkono wake, Halmashauri nazo ziweke mikono yao. Waheshimiwa Wabunge, tuhamasishe wananchi kuliko sisi kuwaita wawekezaji wao ndiyo waje wasindike mazao yetu. Kwanini nakataa? Mwekezaji anapokuja, nia yake kubwa anayokuja nayo ni kutafuta faida. Hana nia nyingine mwekezaji hata siku moja! Anakwenda Tanzania kwa wananchi maskini kwenda kusindika mazao, lakini apate faida yeye. Hana *interest* ya kwamba yule mkulima atapata faida au lah!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tukasimama imara kuanza pole pole kwa sababu sisi ni Taifa dogo. Wenzetu Japan walianzaje? Ukisoma vitabu vya Japan walianza kidogo kidogo. Walipoanza kutengeneza saa, kikundi fulani wanatengeneza kioo, hawa huku wanatengeneza kile cha kurekebishia, wengine mkanda halafu wanakuja kwenye *assembly*, lakini walikwenda kwenye viwanda vyao wenyewe pole pole wakakua ndiyo wakafikia kuwa na wawekezaji na viwanda vikubwa.

Sisi leo Taifa dogo kama hili, tuna *SIDO*, tuliyoianzisha ndani ya Bunge Tukufu kisheria kwamba ije kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya Watanzania. Tukisema tumwite Mwekezaji, anakuja kuchuma, ni lazima atamega faida ambayo angepata mkulima. Kwa hiyo, tunarudi pale pale kwenye sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize hilo kwamba tuwe na operesheni maalum yenye *timeframe* siyo haya mambo ya kuandika kila wakati mimi nimechoka mikakati iliyopo kwenye vitabu vyenu, mimi nataka mikakati ninayoiona kwa macho. Naomba Serikali itupe mikakati inayoonekana kwa macho lakini ya kusomewa kila siku kwamba tuna mkakati huu, Wabunge hatutaki tena. Twende kwenye kutekeleza, twende kwenye kuwakomboa Watanzania kimatendo. Watanzania wakihamasishwa, wataweza kabisa kushirikiana na *SIDO* na wakaanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao yao.

Hii ndiyo sababu ninaomba na ninarudia, Mheshimiwa Waziri uniwie radhi wewe ni dada yangu, lakini upande wa *SIDO* ile shilingi bilioni moja nitasimama wakati wa vifungu. Shilingi bilioni moja kwa *SIDO*, hapana! Tukimpa *SIDO* shilingi bilioni moja tumewaumiza wakulima wa Tanzania wakomboke. Atakayewakomboa ni *SIDO* na *SIDO* anategemea Serikali Kuu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali Kuu mjue kwamba sisi tunayemtegemea ni *SIDO*. Ninasema hivyo kwa sababu kiwanda kinachojengwa na wananchi wangu mitambo yote mimi ninatoa *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ina uwezo wa kusindika matunda, mboga mboga, nafaka na ina uwezo wa kuelimisha. Kwa nini tunamwacha mtoto wetu tuliyemzaa wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa katika hili la viwanda na biashara nasimamia viwanda vidogo na viwanda vya kati na hili ningependa lijengwe kule mazao yalipo. Machungwa yalipo kikajengwe kiwanda cha juisi kule machungwa yalipo. Mananasi yapo Geita kiwanda kijengwe kule kule Geita, kuna njia nzuri sana, wananchi wakielimishwa watаunda ushirika, Serikali Kuu na nyie muongeze kidogo. Halmashauri iwekwe kidogo lakini tusianze kukimbilia wawekezaji sasa hivi, tuanze pole pole kama wenzetu Japan alivyoanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ghafi yote bei yake ni ndogo sana. Ukizungumzia mchele, ukija ukazungumzia tangawizi, ukizungumza machungwa, bei wanayouza wananchi kule Geita, kule Tanga ni bei ya bure, hailingani na kazi wanayoifanya. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikaona kwamba hii operesheni ianze sasa kama ambavyo amezungumza Mheshimiwa Rais. Rais alizungumza mwaka Desemba, 2005. Sasa hivi ni Agosti, 2008 je, tumejenga viwanda vingapi? Ni vyema hapo kidogo wakati Waziri anahitimisha atueleze kwamba ni viwanda vingapi ambavyo tumejenga tangu kauli imetoka mpaka sasa hivi. Kwa sababu Rais alipozungumza nia yake ilikuwa ni kwamba tutoke kwenye kuuza mazao ghafi, tuende kwenye kuuza mazao yaliyosindikwa. Kwa namna hiyo tutaweza kuuza ndani ya nchi na nje ya nchi na tutaongeza thamani mazao yetu na tutamkomboa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi la kwangu lilikuwa hilo. Lakini kilio changu kikubwa ni kwamba tumwezeshe *SIDO* kwa sababu *SIDO* ilianzishwa kisheria. Madhumuni yake wote tunayajua na mkombozi wa Mtanzania ni *SIDO* siyo mwekezaji. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa mchango mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Aloyce Kimaro, atafuatiwa na Mheshimiwa Benito Malangalila na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ajiandaye.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hotuba hii ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kumpongeza pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri pia niwapongeze Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii ambayo naiona ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wana uwezo sana wa kufanya kazi, wana uwezo wa kubuni, Watanzania wako tayari kufanya kazi na Watanzania wakisimamiwa watafanya kazi ambayo italeta maendeleo kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema tunaanzisha viwanda kwa nadharia tu. Tunachozungumza hapa miaka yote ni nadharia. Ili Taifa liweze kuendelea lazima liwe na viwanda. Tunasema, tunasema, sasa viwanda viko wapi? Ili tuweze kufikia katika malengo hayo lazima mipango iwepo, sera iwepo, mipango hiyo iweze kusimamiwa, lazima Baraza la Mawaziri liamue kama tunataka kuwa na viwanda tuwe na viwanda vya namna gani, viwanda vya kati, viwanda vikubwa na viwanda vikubwa sana. Kwa hiyo, tukishapanga ndani ya Baraza lazima tuweze kusimamia kwa ukamilifu ili malengo hayo yafikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua. Tulipanga tutajenga Chuo Kikuu Dodoma, Chuo Kikuu kinajengwa, tukipanga tutatengeneza viwanda na

tukasimamia inawezekana. Serikali ipange viwanda vitakavyotengenezwa watasimamiwa na watu gani? Watakaojenga hivyo viwanda ni watu gani? Watanzania hao watakaokuwa na hivyo viwanda pesa watapata wapi? Serikali iweze kupanga mikakati na mipango mizuri ya kuwawezesha Watanzania ambao wanaweza kuanzisha viwanda. Viwanda vidogo na viwanda vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuja hapa *World Bank*, wakatushauri tuuze viwanda, wakasema Serikali haiwezi kufanya biashara. Lakini Serikali ni nani? Serikali ni sisi wenyewe. Kwa hiyo, Serikali kazi yake ni kuwasimamia Watanzania waanzishe viwanda kwa kuwadhamini wakope katika mabenki na kutayarisha mipango yenyewe, kama Serikali inataka viwanda vijengwe je, viwanda vijengwe vya aina gani na wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malighafi ya viwanda hivyo yako wapi kama yako Kigoma, kiwanda kijengwe Kigoma, kama yapo Tabora kiwanda kijengwe Tabora, kama yako Mwanza kiwanda kijengwe Mwanza, kama yako Kilimanjaro viwanda vijengwe Kilimanjaro. Inashangaza mpaka sasa hivi hatuna kiwanda chochote cha juisi wakati tunazalisha matunda mpaka yanaoza. Hatuna kiwanda chochote kinachosindika matunda. Kwa hiyo, wakulima wanalima lakini wanapouza yale mengi yanayobakia yanaoza. Kwa hiyo, tunawakatisha tamaa. Viwanda vyetu vya ngozi, tulishauriwa na *World Bank* tukaviuza. Wamenunua wajanja, wamevifunga. Sasa ngozi wanauza nje na watu wetu hawana ajira. Viwanda vya baiskeli kilikuwepo, kimefungwa, kiwanda cha *Bulb* kilikuwepo kimefungwa. Viwanda vya Nguo vilikuwepo vikubwa sana, sasa hivi viwanda vya nguo ni vichache na ni vidogo na vinazalisha kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakati huo ikiongozwa na Mwalimu Julius Nyerere, ilikuwa imepanga kwamba tuanzishe viwanda ili tuweze kuendelea. Baada ya ule uamuzi wa kuuza, mimi nasema ulikuwa sio uamuzi wa busara, kitu ambacho tungefanya, tungeongeza mkazo wa kusimamia, kama wewe ni Meneja wa Kiwanda, tumekupa mali ya Watanzania wewe unaharibu, unauwa. Wewe ni muhujumu uchumi, upelekwe Mahakamani na ufungwe. Hatuwezi kukukabidhi mali wewe ukafuja na sisi tukakaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuuza vile viwanda, wale walionunua ndiyo wanaokwenda nje, wanaokwenda China wanakwenda wanaleta bidhaa hafifu na dhaifu. Mpaka sasa hivi bidhaa hafifu na dhaifu zimejaa madukani. Zimejaa kwenye ma-*godown* ya Watanzania ambao hawana nia nzuri na Watanzania wenzao, wanataka kuharibu uchumi wa nchi kwa kuleta bidhaa dhaifu. Matokeo ya bidhaa dhaifu ni kwamba hata wale Watanzania ambao wanataka kujenga viwanda vizuri vya kuzalisha bidhaa bora kwa ajili hata na *export* hawawezi kuthubuti kuzalisha kwa sababu zile bidhaa dhaifu zinaletwa kwa bei ya chini kama bidhaa nzuri inazalishwa na inauzwa kwa shilingi 20,000/= analeta bidhaa inayofanana na ile lakini ni feki anauza shilingi 10,000/= anasambaza Tanzania nzima. Kwa yule mwenye kiwanda ambacho anakiendesha vizuri bei yake shilingi 20,000/= kiwanda chake kinakufa. Baada ya kiwanda kile kufa hawa Watanzania wenzetu ambao sio wazalendo sasa wanapandisha hata zile bidhaa feki sasa zinakuwa ni shilingi 20,000/=.

Kwa hiyo, unakuta uchumi wa nchi unavurugika, mwananchi badala ya kununua *bulb* ambayo itamaliza mwaka mzima, ananunua *bulb* ambayo inawaka kwa mwezi mmoja. Kwa hiyo, kila mwezi lazima anunue *bulb.* Ile pesa angetumia kwa shughuli zingine. Ndiyo maana wananchi wetu wanazidi kuwa maskini kila kukicha. Lakini mimi nasema ndugu zangu Serikali kazi yake ni kusimamia watu hawa na kuwapa adhabu kali. Haitoshi tu kuchoma hizi bidhaa zao. Lazima watajwe kwa majina hawa ambao wanatuhujumu ni hawa na wapelekwe Mahakamani. Ile Sheria ya Uhujumu Uchumi iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kujenga Taifa kwa huruma huruma tu, wanatuhujumu tunawaona, tunanyamaza. Mheshimiwa Waziri kama unataka nikupeleke kwenye hayo ma-*godown* nitakupeleka na utayaona. Hawa watu wanakwenda China. China wanazalisha bidhaa nzuri na za kati na bidhaa dhaifu kama unavyotaka wewe. Hawa wa kwetu wanakwenda pale Wachina wanauliza wewe unataka aina gani? Anasema anataka ile ya chini kabisa. Kwa hiyo, anakuzalishia unaleta unakuja kuwaumiza Watanzania hapa na wewe ni Mtanzania vile vile, tamaa ya pesa. Hivi ukiwa na mapesa mengi na mwenzio hana, inasaidia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakuwa na mapesa mengi mpaka sasa wanaona njia nzuri ya kupeleka hizi pesa ni kupeleka kwenye mpira, kumbe angewapelekea Watanzania wale maskini akaenda akawaanzishia viwanda wakazalisha, wakapata kipato kizuri. Wanaona njia eti ya kuwa Watanzania kuwasikia ni kupeleka pesa kwenye mpira, siyo kuwasaidia Watanzania. Nenda kule Singida kawaanzishie viwanda vidogo vidogo vya kukamua alizeti, njoo huku Dodoma njoo uwaanzishie mashamba madogo madogo ya kuzalisha zabibu ili waweze kupata kipato. Kwa hiyo, utakuwa umesaidia watakuwa wanapata kila siku. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye vipimo. Watanzania tumegeuka watu wa kuibiana, ukienda kununua sukari badala ya kilo moja ile mizani mibovu unanunua robo tatu. Watanzania wakipeleka mazao kwenye Ushirika zile mizani wameshaharibu, badala ya kilo 10 unaandikiwa kilo tisa. Magunia haya yanayoitwa lumbesa, kosovo, gunia la mahindi *standard* ni kilo 100, inakuwaje mtu anakuambia nipe gunia la mahindi anapima yeye mwenyewe anaweka ile inaitwa kosovo mpaka inakuwa kilo 130. Huku ni kuibia Watanzania. Lakini tunazo idara, tunao watu wa kufanya kazi hizo. Leo kwenda sokoni utakuta haya malumbesa yamejaa kule, lakini hawachukuliwi hatua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye mifuko ya *cement*, mifuko ya *cement standard* ni kilo 50, ya sukari kilo 50, leo hii wanasema unatia bomba. Nenda pita kwenye maduka chukua ile mifuko ile ya *cement* utakuta ni kilo 45, kilo 40. Lakini wewe mwananchi hujui unaambiwa mfuko wa *cement* mfuko wa sukari, unachukua. Kumbe umepunjwa. Lakini Serikali tunayo, tunataka Serikali isimamie, tusiogopane hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Watanzania ambao wapo hapa kwa kuibia wenzao hatuwataki, lazima tushikamane, twende pamoja ili tuweze kujenga Taifa hili. Hatuwezi tukasema sisi ni Taifa lile ambalo Mataifa 25 ambayo hayajaendelea. Miaka 40 iliyopita China ilikuwa kama sisi, Singapore walikuwa kama sisi na Malaysia walikuwa kama sisi. Leo hii wako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Kenya kuna viwanda chungu mzima na sisi Watanzania sijui tunapatwa na nini? Leo sisi Watanzania tunapeleka magendo Kenya, lakini huwezi kukuta mtu wa Kenya anahujumu nchi yake analeta magendo Tanzania. Lakini sisi ndiyo tunajiua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba wafanyabiashara tuwe na uzalendo. Tuweke uzalendo mbele, kile kidogo ambacho tunapata tushukuru Mungu na tufanye kazi. Ukifanya kazi ukiwa tajiri Mungu anakubariki. Nakuambia wale matajiri ambao tunawajua wanafanya kazi vizuri ni kama ni Mungu anapitishia pesa kwao ili wagawe kwa wengine. Ili waajiri watu kwa maelfu wawasimamie vizuri na wawagawie mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye fanicha. Mimi nasikitika sana wakati nchi ya Tanzania tuna miti ya kila aina. Tunaweza tukaanzisha viwanda vya samani. Tuna ngozi, leo Serikali ndiyo inaongoza katika kuondoa samani za mininga kwenye ofisi wanakwenda kununua samani takataka, feki, kutoka Malaysia kutoka China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko tunaweza tukaanzisha viwanda vya samani sisi ndiyo tukawa tuna-*export* samani kwenda China na kwenda huko huko Malaysia inakotoka. Kwa sababu tuna mbao nzuri, tuna vijana wazuri, tunaanzisha viwanda vya kutosha angalia magereza angalia JKT, nenda kule Keko Dar es Salaam, vijana wetu wanatoka *VETA* na wanafanya biashara nzuri ya samani. Lakini leo tunawapiga chenga, Serikali ndiyo inaongoza katika kuagiza samani feki kutoka nje, ni aibu kubwa. Sasa naomba Serikali wote muone aibu kwamba si vizuri kuagiza samani, tutoe *order* kwa vijana wetu, tutoe *order* magereza, tuode JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Dar es Salaam, viko viwanda vya uani vya Wachina wanatembeza viatu barabarani shilingi 5,000/=, shilingi 6,000/=. Hivi viwanda ndio viwanda tunaita feki. Haiwezekani wewe mtu sawa sawa Mtanzania ukaanzisha sasa kiwanda cha ngozi, kiwanda cha viatu ili uuze kiatu bora ambacho mtoto wa shule ukimnunulia atamaliza mwaka mzima na kile kiatu, ukaweza kushindana na hawa watu wanaotengeneza viatu uani, Wachina wamejaa kule Dar es Salaam sasa hivi wanauza shilingi 5,000/=, 6,000/=. Sisi tunawaangalia, hivi hawa ndiyo wawekezaji? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, lazima tufike mahali tuseme *no! Enough is enough.* Sasa tushirikiane wote Watanzania wote wanaopenda nchi yao kuhakikisha kwamba tunawatambua hawa watu kama Serikali haijawaona, tutaieleza Serikali wako hapa wadhibitiwe ili tuweze sasa kupata Watanzania ambao wataanzisha viwanda vizuri na

vya kuzalisha bidhaa nzuri tuweze kuuza nje. Hakuna Taifa linaweza kuendelea kama halina viwanda vizuri vya kuzalisha kwa ajili ya soko lake na kwa ajili ya soko la nje. Tukifikia hapo basi tutatoka kwenye mkia, kila siku tunasema sisi ni maskini, sisi ni maskini. Si maskini, kule Jaypul, India wanaajiri watu 280,000 kuchambua tu *Tanzanite*, lakini *Tanzanite* inatoka hapa Mererani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Kimaro, mchango wako ulikuwa mzuri. Sasa nimwite Mheshimiwa Benito Malangalila, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Basil Mramba ajiandae.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii na pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mimi mwenyewe kunipa uhai mpaka dakika hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kusini. *(Makofi)*

Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa hotuba yake nzuri sana aliyoiwasilisha asubuhi ya leo. Binafsi naiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nianze kwa viwanda vidogo vya mbao kule Mufindi. Sisi Wilaya ya Mufindi, miaka ya zamani miaka ya nyuma kama miwili tulikuwa tunazalisha asilimia 60 ya *soft wood* yote ya Tanzania. Lakini hivi sasa naamini uzalishaji umepungua. Zipo sababu kwa nini uzalishaji wa mbao laini umepungua. Sababu kubwa ni kwamba malighafi ya mbao, ambao ni msitu wa *Sao Hill* imepanda mno bei na jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba wale waliokuwa wanavuna pale *Sao Hill* hivi sasa wanavuna huko Malawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa athari ya mambo haya iko wapi? Ni kwamba vita ambavyo Rais wetu anatuambia tunapigana dhidi ya umaskini inashindikana. Sasa kama wananchi wa Mufindi ndiyo waliopanda ile miti na sasa hivi inaanguka kwa sababu imeshazeeka, nataka niulize Serikali inapata faida gani juu ya jambo hilo? Lakini pia hasara nyingine ya pili ni kwamba pato la Serikali linapungua pia. Maana yake pesa zile ambazo zilikuwa zilipe *Sao Hill* wananchi wanunue msitu pale sasa hivi pesa hizo zinaingia nchi ya Malawi.

Mheshimiwa Aloyce Kimaro amesema vizuri sana, amesema kwamba yapo mambo mengine viongozi wetu wa Serikali ni lazima waone aibu. Mimi namuunga mkono sana Mheshimiwa Aloyce Kimaro kwa hotuba yake yote na pia Mheshimiwa Anne Kilango kwa hotuba zao nzuri sana. Lakini nimshukuru sana Mungu kwa sababu Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete alitembelea Wilaya ya Mufindi nadhani wiki iliyopita, mimi nilipewa nafasi ya kuwasalimia wananchi pale. Liko neno nililisema, lilikuwa neno la Kikristo. Sisi Wakristo tunasema kwamba, "Eee Mwenyezi Mungu sema neno moja tu na roho yangu ipone." Nilimwambia Rais Jakaya Kikwete kwa sababu uko hapa, sema neno moja na bei ya msitu wa *Sao Hill* ipungue. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba nchi hii ni yetu sisi sote, tunaitwa Watanzania, tunawajibu wa kuipenda nchi yetu, tuna wajibu wa kuuchukia umaskini wa Watanzania hasa sisi kama viongozi, tuna wajibu wa kuchukua kila hatua kuwasaidia kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Very good!*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Baba yangu mkubwa alikuwa *Sub-Chief* kule Tarafa Mlolo alikuwa anasema kwa Kihehe, *ukubufu unufu.* Maana yake umaskini unanuka. Sasa hilo neno pamoja na maneno mengi lilikaa katika kichwa changu mpaka sasa. Hebu tembea hapa Dodoma hawa ndugu zangu wa Dodoma wanavyoishi kwa kuomba omba. Lakini ardhi yao inazalisha zabibu kwa wingi sana. Kwa hivi ningeomba kuzungumza mambo machache kuhusu soko la mbao laini.

Mheshimiwa Aloyce Kimaro pale amezungumza juu ya Serikali kuagiza samani kutoka nje, ukiangalia kwa kweli zile samani ni nzuri tu kwa sura na rangi. Lakini samani dhaifu sana. Ule ubao wa pale *Sao Hill* ni ubao mgumu sana kutoka hizo mbao za *soft wood* kutoka nje. Ni vema sisi kama Taifa kama viongozi wa nchi ya Tanzania tutumie akili zaidi. Mheshimiwa Aloyce Kimaro anasema yenyewe ikajipigia marufuku katika Wizara zake kwamba ni marufuku kuagiza samani katika ofisi yoyote ya Serikali katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana gani, maana ya kauli hiyo ni kwamba mbao toka Mufindi, zitanunuliwa mbao mninga kutoka Tabora na zitanunuliwa kila aina ya mbao kutoka kule Mtwara, tunatengeneza soko la ndani kwanza kabla hatujaangalia soko la nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu, nataka kuzungumzia juu ya kiwanda cha Pareto pale Mafinga. Kama sikosei pale Mafinga kilijengwa kiwanda cha Pareto mwishoni mwa miaka ya 1970, kiwanda kile kilikuwa kinanunua maua ya Pareto *then* wanatengeneza *crude*, hiyo *crude* ilikuwa inapelekwa Marekani. Kule wanakwenda kutengeneza dawa.

Sisi tulikuwa dawa kutoka Marekani. Nadhani utaratibu huo uko mpaka sasa miaka 46 baada ya nchi hii kuwa huru. Kiwanda kile kwa kweli kilipata mgogoro kilikuwa kinayumbayumba, kikawa kimeshindwa kujiendesha, Serikali ikaamua kukiuza. Lakini mimi sijui kiliuzwa kwa nani na nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atuambie Serikali iliuza kiwanda kile cha Pareto kwa akina nani na anipe kwa majina ili tuwajue, kwa sababu gani, kwa sababu inasemekana kile kiwanda kiko kwa Wamarekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nalisema kwa uchungu sana ni kwamba *PSRC* iliyokuwa na mamlaka ya kuuza kiwanda kile wakati inawalipa mafao wafanyakazi iliandika cheki ikaenda na yenyewe benki ikachukua *cash*, ikachukua *cash* ile ikasafirisha mpaka Mafinga, sasa kama zilifika zote, kama zilifika nusu, kama zilifika

robo, kama zilifika asilimia kumi, hakuna anayejua. Lakini hivi sasa yapo malalamiko makubwa sana ya wafanyakazi waliokuwa wanafanyakazi kiwanda cha Pareto kwamba walipewa hela kidogo, mtu amefanya kazi miaka 20, analipwa laki moja na nusu. Ni mafao ya wapi hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wafanyakazi wa pale wanaamini kwamba wameibiwa pesa nyingi, wametoa jasho pale, wamehangaika, wake zao wamewapikia chai asubuhi na chakula cha jioni. Lakini miaka 20 shilingi laki na moja na nusu, hii si haki. Si haki hata kidogo. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha anipe jibu. La kwanza nataka jibu liseme ni lini watawamalizia mafao wafanyakazi wa kiwanda cha Pareto, Mafinga. Akinijibu vizuri nitaunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO*, Mheshimiwa Anne Kilango amezungumza mambo mazuri sana kuhusu *SIDO*. Mimi nawakaribisha Mufindi Kusini, pale Mpanga tunazalisha peasi nyingi sana na peasi hizo huanguka na zinaoza tu. Waje watutengenezee kiwanda kidogo cha kusindika ili tupate juisi kutoka kijiji kile cha Mpanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kuhusu Kiwanda cha *MPM Mgololo* zamani kilikuwa kinajulikana kama *SPM Mgololo.* Kiwanda kile kwa sasa kinazalisha karatasi nyingi sana na kila miti ya karatasi inayozalishwa *MPM Mgololo* inauzika na ni ya hali ya juu sana karatasi kutoka Mgololo. Siku moja nilikwenda kutembelea kiwanda cha ma-*box* kule Mwanza. Walikuwa wanatoa machozi wanasema jamani kama *SPM* haizalishi, utapata wapi karatasi nzuri kama *SPM.* Nikawauliza zile karatasi kutoka Ulaya? Wakasema zile ni karatasi feki tu, wanaokota mikaratasi ya mitaani wanakuja ku-*process* inatoka karatasi, hilo *box* ukiligusa tu linapasuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini karatasi kutoka Mgololo inatoka kwenye *virgin tree*, mti halisi na ningependa kuwapongeza sana wafanyakazi wa Mgololo, sasa hivi inaitwa *MPM Mgololo* kwa kazi nzuri wanayoifanya pale kiwandani. Lakini pia nimpongeze sana yule muwekezaji yule *RAI*, anafanya kazi nzuri, kwanza aliwalipa wafanyakazi mishahara mwaka mzima wakati yuko kwenye *process* ya kukiandaa vizuri kile kiwanda kwa sababu kwa kweli kilikwishafikia hali isiyo nzuri. Ndugu zangu hapa wa Upinzani wamekitupia tupia madongo juzi lakini mimi nasema tupieni madongo kwa kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka mimi nilikuwa Mbunge toka mwaka 1995, kile kiwanda kilikuwa kinachechemea, kilikuwa kinatembelea mguu mmoja. Mpaka kinafikia kubinafsishwa mimi nimeomba Mungu, nikamwambia Mungu wangu nimechukua kiwanda kikubwa katika Afrika, ndio kifie mkononi mwangu? Mungu akasema hapana mwanangu, nitakupa muwekezaji. Tukapata mwekezaji pale na kwa kweli anafanya kazi hiyo isipokuwa tatizo kubwa pale ni wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mwekezaji alipofika pale hakuwapenda kabisa viongozi wa kisiasa, hasa wa Chama Tawala na viongozi wa vyama vya wafanyakazi. Wale ndio walikuwa wa kwanza kabisa kuwatimua, kuwafukuza kazi. Sasa wale

wafanyakazi wako pale wanakaa karibu miaka miwili hawana mshahara, lakini wanakaa katika nyumba za kampuni na Serikali inatakiwa ilipe na yule mwekezaji anatakiwa alipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi namuomba sana Waziri, anayehusika na Wizara hii aende. Tulikuwa tunaongea hapa amesema atakwenda Mgololo, napenda nimsisitizie kwa dhati kabisa kwamba anawajibika kwenda Mgololo, akaongee na wale wafanyakazi waliofukuzwa kazi pale ambao wengine sasa hivi wanafariki kwa sababu mbalimbali, sijui njaa? Akawape majibu ya kueleweka, kwamba kwanza wataondokaje pale kwenda huko makwao, kwa sababu wale wafanyakazi sio wenyeji wa asili ya pale ni watu waliotoka sehemu mbalimbali za Tanzania na Mheshimiwa Waziri, anajua kulikuwa na wafanyakazi 760 wanaishitaki Serikali na hukumu imeshatolewa, mimi sielewi Serikali inatafuta nini juu ya jambo hili. Lakini kwa sababu Chama cha Mapinduzi kilipata ridhaa ya kuchaguliwa na Watanzania wakiwemo na wale wafanyakazi na Chama cha Mapinduzi kilipata 94% ya kura katika Wilaya ya Mufindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono mia kwa mia hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, na vile vile kuwapongeza kwa hotuba hiyo ambayo ilikuwa nzuri na yenye mawazo mengi na mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo kwamba kwa sababu ni jana tu nimetoka huko naweza nisieleweke sasa unamwambia nani? Si ulikuwepo? Na mimi ninasema kama niliyekuwepo nisiposema, nani anajua kuliko mimi? Kwa hiyo, ni bora niyaseme kwa sababu ni ya umma na kwa sababu ndio jukumu la Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na waliosema kwamba kwa kasi hii, kwa mwendo huu, nchi yetu itachukua muda mrefu sana kuwa nchi ya viwanda. Viwanda tulivyonavyo ni vile ambavyo alianzisha Mwalimu Nyerere, tukavikarabati, tukavipiga rangi, tukaweka mitambo mipya hapa na pale na utaalamu mpya na mitaji mipya, ndivyo leo tunavyoita viwanda vya Tanzania na ndivyo vinavyotupa ile asilimia ya kukua kwa viwanda ambayo iko kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Mwalimu Nyerere, ilikuwa inaitwa *Basic Industry Strategy,* haijatekelezwa tena toka Awamu ya Tatu, nafurahi kuona kwamba sasa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, inarejea sera ile na kuileta katika hali ambayo tunaweza tukaitekeleza kwa mazingira ya leo. Kazi hiyo niliianza, natumaini kwamba haitachukua muda mrefu kuja kwa sababu kwa kweli bila hiyo, tunaweza tukasahau habari ya viwanda katika Tanzania na la msingi litakalojitokeza kwenye sera hiyo ni Serikali kurudia kuwa kichocheo cha uanzishwaji wa viwanda kwa kuweka fedha zake yenyewe. Serikali isiporudia kuwa kichocheo cha kuanzisha viwanda, tunaweza tukasahau habari ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda, kwa Kiingereza tunaita *catalytic role*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri uko hapa Dodoma, Wizara ya Mifugo kwa hali isiyo ya kawaida ilianzisha kiwanda cha kusindika nyama kwa fedha zake, ingawa ilikopa nje. Kiwanda sasa kinafanya kazi na juzi tulisoma kwenye hotuba ya

Waziri wa Mifugo kwamba kiwanda kile sasa kimekwishabinafsishwa 51% na waliokinunua ni wenzetu akina *NICO.* Hebu fikiria kama toka Awamu ya Tatu tungekuwa tunafanya mambo ya namna hiyo, leo ni nyama, kesho ni kahawa, kesho ni pamba, kesho ni tumbaku, kesho ni mazao yote haya, ungekuta tuko mbali kabisa na mimi nataka nitoe angalizo kwamba ingawa tumeweka mazingira mazuri mno kwa uwekezaji katika viwanda, hawa wanaokuja wapya kuanzisha viwanda hawaji, ni lazima sisi tuanze halafu watukute na watuunge mkono. Sisi ni lazima tuanze. Mengine yamesemwa sitaki kuendelea zaidi, lakini nililotaka kusisitiza hapa ni Serikali kuwekeza kama mchochezi ili wengine waweze kununua na wengine hao wanaweza wakawa Watanzania, sio wanaweza wakawa, hasa Watanzania na kwa njia hiyo tutaweza vile vile kuwawezesha Watanzania kuanzisha viwanda kwa utaratibu wowote ule wa *Private Public Partinership (PPP),* wowote ule utakaokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hasa lililonifanya nikasimama leo ni suala la viwanda vidogo. Viwanda vya Watanzania ni viwanda vidogo kwa sababu ndivyo vilivyo ndani ya uwezo wetu kifedha, yaani kimtaji na kiutaalamu, viko ndani ya uwezo wetu sisi Watanzania wa kawaida. Hatuwezi kuanzisha viwanda vikubwa kama cha bia au cha sigara au cha saruji, sisi Watanzania tuliomo humu ndani wote sisi hapa hakuna hata mmoja mwenye uwezo wa kuanzisha kiwanda hata kununua huko hisa 10% tu hatuna, lakini hivi vidogo tunaviweza. Kwa bahati mbaya simuoni Mheshimiwa Yusuf Makamba hapa, Katibu wetu wa Chama cha Mapinduzi, lakini naona wajumbe wa *NEC* wako wengi hapa ndani na mimi nauliza swali, je, Chama cha Mapinduzi bado kina sera ya kuendeleza viwanda vidogo vidogo? Je, Chama cha Mapinduzi, bado kina hiyo sera? Sera ile ni ya mwaka 1972, ilikuwa sera ya *TANU* ndiyo iliyoanzisha viwanda hivi vidogo na ilikuwa na nafasi kwenye sera ile ya *Basic Industry Strategy,* ile sera ya viwanda vya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa, siku hizo mimi nilikuwa Mkurugenzi Mkuu Muanzilishi wa *SIDO,* siku hizo ilikuwa Rais hawezi kwenda kwenye Mkoa asitembelee kiwanda kidogo, Waziri Mkuu, hawezi kwenda kwenye Mkoa asitembelee kiwanda kidogo na wewe Mkuu wa Mkoa, ukipanga ratiba usipoweka kiwanda kidogo upo hatiani, lazima mkubwa aende akaangalie. Leo ni Mwenyekiti yupi wa Halmashauri ya Wilaya, ni Meya yupi wa miji yetu anayejua kuna viwanda vingapi vidogo katika mji wake au katika Wilaya yake? Mimi naweza nikasema hamna, ni Halmashauri ipi yenye Bajeti ya kuendeleza viwanda vidogo katika Wilaya yake? Hamna. Sasa hivi viwanda vidogo ni mali ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana wamachinga wanaongezeka kwa sababu machinga ni mtu huria anajiendesha mwenyewe na hategemei mtu yeyote na hakuna mtu anayemsaidia. Sera ile ya *TANU* ilisema mambo ya kufanya na jambo hili nimeona kwenye hotuba kwamba wanaangalia upya namna ya kurejesha baadhi ya sera hizi na kubadilisha sheria ya viwanda vidogo. *(Makofi)*

Mimi nashauri, kila kitu kinachotakiwa kusemwa juu ya viwanda vidogo kipo, kipo wapi? Kipo kwenye agizo la *TANU* juu ya viwanda vidogo vidogo na liko kwenye maktaba ya *CCM* bila ya shaka, agizo la *TANU* juu ya viwanda vidogo vidogo lilisema nini? Lilisema ni marufuku idara yoyote ya Serikali kununua vitu nje ya pale Wilayani, kama unataka *furniture* utanunua *furniture* ya pale Wilayani, unataka kujenga jengo utatumia fundi wa pale Wilayani, chochote kile kinachohusiana na manunuzi kwanza

viwanda vidogo halafu viwanda vikubwa vya humu ndani, yaani uzalendo ule aliokuwa anazungumza ndugu yangu Mheshimiwa Aloyce Kimaro, uzalendo. Hii habari ya kununua kila aina ya kitu na tena siku hizi baada ya ile sheria ya manunuzi ndio tumezidi kulemaa kabisa. Sheria ya manunuzi nyie mko Rombo, mnaenda kuleta vitu kutoka Moshi, na mafundi wenu hapa wanakosa kazi, halafu mnasema mnaendesha viwanda vidogo vidogo, mtaendesha wapi? Kwa hiyo, manunuzi ya Serikali, yatokane na viwanda vidogo na viwanda vya humu nchini, kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, viwanda vidogo visamehewe kodi. Kama tunaweza tukasamehe kodi wale wakubwa kwa muda mrefu, kwa nini usisamehe kiwanda chako kidogo kwa miaka mitano, kwa miaka kumi mpaka kijiimarishe. Ya tatu, viwanda vidogo vipate njia rahisi za mikopo katika benki, hapa tumechelewa kupata ile sheria ya *hire purchase*, ile ya kumuwezesha mtu kukopeshwa mashine ndogo ndogo, vifaa vidogo vidogo vya kuzalishia halafu akarejesha. *SIDO* ya kwanza ilikuwa inafanya jambo hili sasa tumekuja kusikia kuna matatizo na kuna sheria inayokuja, ile ije haraka, itawawezesha watu wadogo hawa kukopeshwa mashine badala ya pesa taslimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya tatu, nchi zenye sera sawa sawa ya viwanda vidogo, benki zinalazimishwa kisheria kukopesha asilimia fulani ya mikopo yao yote ya mwaka kwenye viwanda vidogo yaani kama wewe unakopesha shilingi bilioni 10 asilimia fulani ya ile shilingi bilioni 10 ni lazima iwe imeenda kwenye viwanda vidogo. Tusibembeleze hawa maana yake ukisoma *balance sheets* za haya mabenki kila mwaka kila benki hata ndogo mabilioni ya faida wanagawana, lakini mtu mdogo anakuwa mtazamaji tu. Sisi tunasema kwenye nchi zenye sera za dhati mabenki yanalazimishwa ku-*set aside*, kutenga asilimia fulani ya fedha zao za mikopo kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati na hapa ni lazima hiyo ije kama tunataka kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya nne, wale walioendelea zaidi kama India, wameanzisha benki ya viwanda vidogo. Hapa nimesikia tunazungumza habari za benki ya kilimo, benki ya viwanda vidogo pia ni muhimu sana kwa sababu hii ndio sekta ya Watanzania. India wana benki ya viwanda vidogo. Hapa kama hatuwezi basi tuziambie hizo benki zi-*set aside* hizo pesa hiyo asilimia kwa kuanzia lakini tulenge kuanzisha benki ya viwanda vidogo. Mmeona maombi ya *SIDO* ya kuendesha *SIDO* tu hapa tumeambiwa kwenye hotuba hii, walitaka shilingi bilioni tano wamepewa shilingi bilioni moja, tutafika, tutafika lini kwa *speed* hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kasi hiyo hatufiki. Katika nchi zenye sera ya sawa sawa, leo kwenye kipindi cha Maswali na Majibu kuna Mbunge mmoja alisema, sijui maswali sijui ilikuwa kuchangia mwanzoni, je, haiwezekani mimi nikiwa na kiwanda kidogo nikampeleka fundi wangu kusomea kule *VETA* na Serikali ikamlipia kupitia *SIDO?* Nchi zenye sera ya kweli zinalipia watu wa viwanda vidogo kusoma, kupata ujuzi ili wakirudi waendeleze viwanda vyao na hela hizi zingepitia *SIDO*. Sasa hivi wala hatuna na wala hatuizungumzi na katika vyuo vyetu, vyuo vyetu vingefundisha wasomi wetu mambo ya viwanda vidogo, jinsi ya kuendesha viwanda, jinsi ya kusimamia viwanda vidogo na mwisho kabisa, hatuwezi kuendeleza viwanda vidogo bila wataalamu, wahudumu hawa wa *SIDO*, wale wangetakiwa wawe ni watu wenye elimu ya juu, waliobobea na wanaolipwa vizuri. Narudia, wanaolipwa vizuri sana na tena hawa wasibaki pale mkoani, miaka 30 *SIDO* iko pale mkoani, sasa waende Wilayani kila

Halmshauri iwe na mtaalamu wa *SIDO* wa kushughulikia viwanda vyao pale kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kweli tunataka kuendeleza viwanda vidogo hayo ndio mambo ya kufanya jana, sio leo, jana na kwa kuwa sasa Wizara inafanya marejeo ya sera iliyokuwepo na sheria yake, mimi nashauri kwa dhati, hiyo ndiyo njia, hakuna njia mkato katika jambo hili. Lakini tunahitaji *political will* (utashi wa kisiasa), huu utashi mimi siuoni, kwamba kweli tunataka kwa dhati kuendeleza Watanzania kwa njia ya viwanda vidogo? Huu utashi mimi siuoni maana utashi ni lazima uendane na vitendo na hivyo vitendo sivioni. Hatupendelei viwanda vidogo wala hatutumii mafundi wetu, wala hatushughulikii, kama ilivyoelezwa hapa na Wabunge wengi na kama kuna watu waliofanya makosa hayo hata mimi ni mmojawapo lakini sasa ni lazima tujirekebishe. Utashi wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba kama tunataka nchi yetu iendelee kiuchumi, ikue kuchumi, sekta ya kilimo ni kama sasa tumefika mahali tunazungumza mpaka habari za mapinduzi ya kijani. Sekta ya kilimo yaani uzalishaji katika kilimo na sekta zinazoendana na kilimo ni muhimu lakini la pili, uzalishaji wa viwanda vikubwa, vya kati, vidogo, ni muhimu. Ukiangalia Bajeti ya Wizara hii, hela zile kuna watu wengi walionazo mfukoni, shilingi bilioni 16, na 31 Wizara nzima na madaktari wengi namna hii? Pale umesikia wale madaktari wale? Waziri Daktari, Katibu Mkuu Daktari, Naibu Katibu Mkuu Daktari, madaktari daktari wengi namna hii, wana daktari nini? *Nothing,* kwa sababu hawana pesa, wapeni pesa tutumie madaktari hawa kutusaidia tuendelee katika sekta ya viwanda, shilingi bilioni 16 watu wengi wanazo mfukoni, ni aibu kabisa, na fedha za mwaka huu ni kidogo kuliko za mwaka jana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nashangaa kwamba kama kweli tuna nia ya kuendeleza uchumi na kukuza uchumi ni lazima tuione Wizara hii ya Viwanda kama Wizara mama na Wizara muhimu ya kupendelewa. Ukishamaliza kufanya hivyo vitu vingine bila fedha zaidi, maana yake hela ni lazima izae hela zaidi, hela inazaliwa kwenye viwanda na hela inazaliwa kwenye kilimo, tusipotoa hela humo tumekwisha. Kwa hiyo, naomba kuunga hoja mkono na ninashukuru sana kwa nafasi uliyonipa, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa siku ya leo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa kazi nzuri na mwelekeo mzuri ambao wanaanza kuuonyesha, kuweka mazingira mazuri ya kibiashara na ujenzi wa viwanda hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa nukuu ya nukuu, ndani ya kitabu hiki, Mheshimiwa Waziri, amemnukuu Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, sasa yeye amemnukuu na mimi nanukuu, nukuu ya Mheshimiwa Waziri, hapo ndio mahali pa kuanzia. Inasema; “Uchumi wa nchi yoyote iliyoendelea, ulianza na kilimo na kisha kuwa na viwanda,” na sisi Watanzania hilo ni la kwangu nimeongeza, hatuna budi kuelekeza nguvu na kuweka mkakati maalum katika kukuza na kuendeleza viwanda nchini. Viwanda vikubwa, viwanda vidogo na vya kati, vina uwezo mkubwa wa kutoa

nafasi za ajira na vile vile vinasaidia kusindika mazao ya kilimo, mimi naomba niishie hapo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sisi kama Watanzania tutafakari maneno hayo na leo hii tujiulize je, mwelekeo wetu ni nini kwa kauli hii ambayo mimi nimemnukuu Mheshimiwa Waziri, ambaye yeye pia amemnukuu Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Je, ni kweli Tanzania kama nchi hapa tulipo tunakuza viwanda? Kwasababu imetamkwa kwamba nchi zinazoendelea zilianzia huko kwenye kilimo hatimaye zikaenda kwenye viwanda. Je, tunakuza kilimo? Je, Tanzania hapa tulipo tunakuza viwanda? Kama hivyo sivyo na kwa kweli kwa kuzingatia Bajeti zilizopita na kwa mfumo ambao nimeuona kwa muda mrefu, kilimo hakijakua, viwanda havikui, ukitizama huko tulikotoka tulikuwa tunajaribu kutaka kukuza kilimo, tulijaribu kwa kiasi fulani kukuza viwanda tukafika mahali kilimo kikaanguka na viwanda vikaanguka na ni mahututi na sioni mkakati mkubwa unaonipa matumaini kwamba viwanda vitafufuka. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba njia yetu kuelekea kukuza uchumi kwa kutegemea kilimo na kutegemea viwanda tutafika mahali tutasema tumekwama Watanzania. Lazima tusimame imara tuanze upya, tukuze kilimo basi na tukuze viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatua ya kwanza ya ushuru wa forodha inakaribia kufika ukomo wake mwisho wake wa kuendeleza. Maana yake ni kwamba tutakwenda katika hatua ya pili na mimi nafahamu kwa sababu nimekuwa nikishiriki katika baadhi ya mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nafahamu kinachoendelea. Tunakwenda kwa kasi kuanza utekelezaji wa hatua ya pili ambayo ni kuwa na soko la pamoja. Sasa tunakwenda Watanzania tunakaribia hatua hiyo ya pili, tutakwenda hatua ya tatu ambayo ni ya sarafu na baadaye umoja. Lakini tunafika hatua hiyo ya soko la pamoja Watanzania hatuna kitu tutakachoingiza katika soko hilo la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko maana yake ni nini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? Maana yake mnakuwa na eneo kubwa zaidi ambalo mnaweza mkauza bidhaa zenu. Soko limepanuka, sasa nchi ni tano kweli soko ni kubwa lakini tuna nini tutakachopeleka katika soko letu? Kenya wanajivunia viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wana bidhaa ambazo watazipeleka katika soko hilo la Jumuiya ya Afrika Mashariki linalokuwa sisi hatuna. Tunafanya nini sasa ili kujenga uwezo wa viwanda vyetu? Wenzangu wamezungumza sana, tumekuwa tukiitegemea sana *SIDO* na ni lazima tukiri *SIDO* wamefanya kazi nzuri. Lakini wanafika mahali wafanye nini zaidi ya hapo kufuatana na uwezo tuliowajengea? Hawana cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Muheza wamejitahidi sana, wamesaidia akinamama katika kiwanda cha kusindika matunda, lakini nilitoa mapendekezo miaka mitatu iliyopita kwamba sasa *SIDO* mkae chini muwasaidie akinamama hawa katika mambo yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza muwasaidie kuwaandikia andiko ili liwawezeshe kuanzisha viwanda. Jambo ambalo namsifu sana Mheshimiwa Anne Kilango, kwamba kule kwao Same wamefanikiwa katika hilo. Muwasaidie kwa sababu hawana hata uwezo wa kuandika hilo andiko. Lakini muwasaidie vile vile namna ya kuanzisha viwanda, muwasaidie namna ya kupata mashine, lakini msaidie pia namna ya

kuwafundisha kusimamia viwanda hivyo, lakini muwasaidie namna ya kutengeneza ule mchanganuo wa hisa ili kuweza kusaidia kuanzisha kampuni. Hili kule Same wamelianza kwa jitihada kubwa, naomba sasa huo ndio uwe mfumo wa *SIDO* kusaidia viwanda vidogo vidogo lakini hawatataweza kufanya hilo kama hatuwapi fedha. Kwa hiyo, tutizame mahitaji ya *SIDO* kama kweli tunataka viwanda vidogo vianzishwe ili hatimaye vikue na viwe viwanda vikubwa. Siku zote viwanda vinaanza taratibu kwa uzalishaji wa kiwango fulani, lakini kutokana na mafanikio ya mwaka wa kwanza wanaendeleza uzalishaji mwaka wa pili na mwaka wa tatu na hatimaye vile viwanda vidogo vinakuwa viwanda vikubwa na vinajijengea uwezo wa kuviwezesha kuwa viwanda vikubwa, tunafanya nini kuwasaidia *SIDO?* Tumeona maonyesho, tangu Saba Saba imeanza sijui huu mwaka wa ishirini na ngapi sasa? Kila siku ukiingia katika maonyesho yale utawakuta wabunifu wazuri wamebuni mitambo mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho nilipokwenda mwaka jana kwenye maonyesho tuliona wabunifu hawa lakini tulisema hivi mnawasaidiaje hawa *SIDO?* Wamebuni mashine hii, ina uwezo huu ambao sasa tunauona na tunaufurahia ndani ya maonyesho ya Saba Saba, kinachofuatia ni nini? Ni uzalishaji wa mashine zaidi kutokana na ubunifu ambao hawa wabunifu wadogo wadogo wajasiriamali wameweza kufanikiwa kuufanya. Hawana mtaji maskini ya Mungu, kwa hiyo, wanaishia na maonyesho wanayoleta mashine moja pale kwenye maonyesho ya Saba Saba na mwaka unaofuatia watakuja nayo hiyo hiyo, baada ya miaka mitatu hiyo hiyo. Hatuwasaidii kitu, mfumo wetu wa kuweza kupata mikopo hauridhishi wala haupo, ndio tunataka kuanza kuujenga kwa kuanzisha sheria hizi ambazo tumeziona zinaanzishwa sasa. Tuziimarishe sheria hizi ili tujenge uwezo na fursa ya kuwezesha hawa wanaoanzisha viwanda vidogo waweze kuvianzisha, wabunifu wanaotengeneza mashine, waweze kutengeneza mashine za kutosha ziweze kuuzwa katika masoko ili mashine hizo zisaidie katika usindikaji wa mazao na katika uzalishaji wa umeme na vifaa vingine muhimu katika uendeshaji wa viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niikumbushe Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwamba mnawajibika kama Wizara na hii mmeiandika katika ukurasa ule wa 49 sehemu ya "E" ya kitabu hiki cha hotuba. *(Makofi)*

Moja ya wajibu wenu ni kutoa elimu ya kanuni na taratibu za masoko na biashara na nchi za nje, hili mnalitekeleza vipi? Hakuna mwaka ambao nitasismama kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, bila kusema hali ya machungwa katika Wilaya ya Muheza, biashara ya machungwa. Nimesema hapa nimewaomba viongozi wa Wizara hii waje, wameahidi mara chungu mzima, hakuna hata siku moja wamefika Muheza, kwamba biashara ya machungwa Muheza inaendeshwa na watu wa Kenya, wanakuja kununua machungwa kwa kutumia fedha za Tanzania. Hivi ndiyo biashara hii? Ndiyo kanuni ya utendaji wa biashara kati ya nchi na nchi? Ni kweli tunaelekea kwenye Jumuiya, tupo kwenye Jumuiya, sawa, lakini bado Kenya na Tanzania ni nchi, zipo kanuni zinazosimamia uendeshaji wa biashara pale mmetusaidia vipi? Mara kumi nawaita hamji, hamlisaidii Taifa hili kwa sababu kama mngekuja mkasimamia inawezekana machungwa yale yangenunuliwa kwa fedha za nje, ingesaidia nchi hii. Lakini kanuni wananchi hawazijui na ninyi hamji kutusaidia kuzisimamia. Mheshimiwa Rais ametoa ahadi mara kadhaa ya kusaidia Wilaya ya Muheza kupata kiwanda cha usindikaji, nimejaribu kuzungumza na Wajerumani wamefika Muheza wamejaribu

kuangalia lakini wakaona kiwango cha machungwa yanayozalishwa hakitoshi kiwango cha kiwanda wanachotaka, wanataka kiwanda kinachofanya kazi saa 24 kwa zaidi ya siku 300 kwa mwaka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunahitaji kuwa na kiwanda cha kati na ninafurahi kusema kwamba katika semina tuliyohudhuria juzi nimeona mwelekeo kwamba inawezekana, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri akumbuke hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais, asaidie na mimi nitakuja tushirikiane ili tuweze kuhakikisha kwamba Muheza wanafanikiwa kupata kiwanda cha usindikaji wa matunda kwani tuna machungwa mengi sana, maembe, mananasi, ndizi na kadhalika ambazo zinatosheleza usindikaji katika viwanda. Niikumbushe tena Wizara kwamba hebu malizeni taratibu za kuandaa Kanuni na tumesikia mnataka kufanya marekebisho katika Sheria ile ya uandikishaji wa biashara, fanyeni hizo kwa sababu sasa sheria ipo lakini haitumiki, huu sasa unakaribia mwaka mmoja na nusu bado katika Halmashauri zetu kuna mivutano ya ada za leseni. Lakini tulisema pengine sheria hii itaondoa hilo tatizo, nini kinawakwamisha kuandaa taratibu na kufanya marekebisho hayo ya sheria hiyo ili wananchi waweze kufahamu na kuanza uandikishaji wa biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mfumo wa kodi tuliyokuwa tumeomba na ukawa unasimamiwa umeanza kuleta sura mpya sana, katika miji yote nenda Muheza, Tanga, Dodoma, Dar es Salaam katika kila nyumba utakuta wanajenga madirisha kwa ajili ya biashara, nani wanakodisha madirisha haya ya biashara ambayo ni mengi sana? Ni hawa wamachinga waliokuwa wanatembea barabarani sasa wanakuja katika vibanda tunavyojenga, vipo vingi sana. *(Makofi)*

Nnenda Dar es Salaam kila nyumba imegeuka ina madirisha matatu, matano au hata kumi ya biashara, hata mimi pia ninayo na wamachinga ndiyo wanakuja wanataka kukaa kule. Tumewajengea jengo zuri sana pale Dar es Salaam nina imani kabisa kwamba majengo ya namna hiyo yataendelea kujengwa katika Mikoa na katika Wilaya nyingine. Machinga wanataka kuondoka barabarani warudi, lakini ukienda katika utekelezaji wa haya utakuta jinsi wanavyohangaishwa Wamachinga hao wanaokuja kufanya biashara katika vibanda hivyo ambavyo wawezeshaji wameweza kuvijenga. Tuondoe kasumba hizi za kuwakatisha tamaa hawa ambao wanataka kufanya biashara katika maeneo sasa yatakuwa yanatambulika rasmi. *(Makofi)*

Lakini la mwisho niseme bidhaa bandia zinatuletea matatizo, chombo hiki tulichounda, sheria tuliyoiweka ifanye kazi vizuri, kwenye semina juzi tuliambiwa bado kuna kasoro, hitilafu na mambo yanahitajika kufanyika ili kuboresha sheria hizo na kanuni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Herbert Mntangi na sasa nitamuita Mheshimiwa Yono Kevela, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Margreth Mkanga ajiandae.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi ya kipekee kukushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. *(Makofi)*

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, kwa hiyo, ninahusika moja kwa moja na hii Wizara. Lakini sasa hivi kabla sijaanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwamba Waziri amejitahidi sana sana kueleza vizuri na kutoa hotuba vizuri. Lakini pia niwapongeze wote ambao wako kwenye Wizara hiyo akiwemo Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

Lakini kabla sijazungumza labda nijikite katika suala la hawa Wamachinga. Hawa Wamachinga mwenzangu amezungumza hivi karibuni ni kama watoto yatima, wanasumbuliwa sana na ni vijana wenzetu wale, wanahangaika biashara na mitaji ya kukopa lakini wanasumbuliwa sana. Sasa kwa vile mimi ni mdau na ni mfanyabishara naona kwa kweli hawa watu wanatakiwa wawezeshwe, wapewe mitaji na masoko. Ningekuwa ni Waziri ningefanya juu, chini niwatengenezee hata *scholarship* waende kule India kusoma au niwapeleke pale Ngurdoto wasome na wapewe semina kwa sababu mpaka sasa hivi wanajihangaikia wenyewe na hawana mtu wa kuwasaidia. Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Waziri atengeneze semina ya kutosha kwa ajili ya hawa vijana wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nizungumzie hapo hapo kuhusu suala la hawa Wamachinga ni hili tatizo la hawa wageni wanaofanyabiashara za vijana wetu. Nimesikia kwamba kuna Wakorea na Wachina na kweli huwa wanaonekana pale, sasa sielewi hawa Wachina umachinga wafanye kule kwao China ili hawa vijana wetu waachiwe wafanye hizo biashara kwa sababu ndiyo ajira zao.

Tukianza kuwabanabana maana yake wanataka waingie msituni waanze kuiba, kwa hiyo, nashauri hawa wafanyabishara wadogo wadogo wasisumbuliwe na ninaposema Wamachinga hatumaanishi kwamba ni wale wanaoishi pale Dar es Salaam, lakini wapo Wamachinga pale Makambako, Ilembula, Mtwara na sehemu mbalimbali kwa hiyo, wale watu wawezeshwe wapewe semina, nani atafanya semina siyo kazi Waziri peke yake hata Wakurugenzi wa Wilaya walitakiwa wahakikishe wanatafuta mbinu zozote za kuwakusanya vijana wetu hawa na kuwapa elimu ya kutosha yaani elimu ya ujasiriamali *(entrepreneurship)* ili waweze kufanya biashara kwa faida, siyo wafanye kwa hasara hasara na wasisumbuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Baraza la mfumo wa stakabadhi ya mazao. Wenzetu wanaeleza habari za korosho, mpunga na maendeleo mbalimbali wanafaidika sana kuhusu huu mfumo wa stakabadhi ya mazao. Sasa najiuliza kwenye Jimbo langu la Njombe Magharibi, mimi natoka kijiji cha Kamalenga pale wanalima alizeti, tarafa za Mdandwi, Malinyi wanalima alizeti lakini hasa hasa tarafa ya Wanging'ombe ndiyo alizeti ipo ya kutosha sana. Sasa hii alizeti imeshasahaulika, haina stakabadhi ya mazao wananyonywa wananchi na hiyo alizeti ina *grade* ya aina mbalimbali na ninaposema alizeti ina maana hata wenzetu wa Singida na Dodoma wanalima alizeti na Mikoa mingine pia siyo Mkoa wa Iringa tu. Kwa hiyo, hawa watu huo mfumo wa stakabadhi ya mazao hata alizeti wangeliingiza. Halafu alizeti yenyewe

iwe na bodi yaani bodi ya kumtetea mkulima, kuna mafuta mazuri sana ya kupikia hayana athari kabisa kwa mtumiaji. Sasa nilikuwa nafikiria kwamba hii alizeti nayo iingizwe kwenye stakabadhi ya mazao ili mkulima asinyonywe aweze kuweka kwenye ghala akapewa ile hati akachukulia mkopo na wakati bei ya alizeti inapopanda inakuwa ni rahisi kuiuza kwa bei ya juu siyo kama ilivyo sasa hivi tunaibiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niruke hilo, nitazungumza vile vile kuhusu suala la kiwanda nitakapofika kwenye upande wa *SIDO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije upande wa mikopo, hizi *microfinance.* Hizi *SACCOS* wenzangu wanasema zinasaidia, ni kweli zinasaidia lakini wale watu wanapewa visenti vidogo sana sasa mtu unamkopesha shilingi 50,000/= unasema akafanye biashara, unamkopesha shilingi 100,000/= sasa hapo labda ni kama unamsaidia tu. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nafikiria kwamba unaposema *SACCOS* unataka kumkopesha mkulima au mfanyabishara mpe hela inayotosha na hili nazungumza hata upande wa *Price, Thinker*. Kule wanakokwenda kuchukua hela wanapewa riba kubwa sana kwa hiyo, ile riba kubwa wanayopewa watu wa *Thinker* au *Prider* ina *affect* sana huyu mkopaji wa chini yaani huyu mfanyabishara mdogo mdogo huyu kwa hiyo, ina maana asilimia inazidi sasa wananchi wanashindwa kurudisha mikopo. *(Makofi)*

Mimi nafahamu kabisa adha wanayoipata hawa wafanyabiashara, wanauziwa mali na kwa sababu hawana jinsi na sisi kama kampuni yangu inahusika na suala la kuuza mali za watu inasikitisha lakini hatuna jinsi ni sawa sawa na biashara ya majeneza kwa sababu hata ukikataa kwamba usiuze mali kwa huyu bwana ina maana atauziwa na mtu mwingine. Kwa hiyo, nilichokuwa nafikiria hapa kwa kweli suala la elimu itolewe na wapewe mitaji ambayo inaendana, kuwe na *specialisation,* siyo lazima wote wafanye biashara, wengine ni wakulima wapewe mikopo ya kilimo, wengine ni wafugaji basi wapewe mikopo ya ufugaji. Lakini hawa wafanyabiashara ndogo ndogo wawezeshwe na waelimishwe vizuri kwamba huu mtaji athari yake ni hivi na hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wenzangu walikuwa wanasema kwamba mtu akipata hizi hela labda anapata shilingi milioni moja, hajawahi kupata anaona hizi hela ni nyingi sana anaweza kununua gari, kuongeza mke wa pili sawa lakini hili ni tatizo la vile vyombo vya fedha kwamba havimjulisha**,** anaweza akaona kwamba pengine nikiwa na watoto wengi baadaye huenda ukawa ni mtaji baadaye watakuja kunisaidia. Kwa hiyo siyo wakulaumu. Kwa hiyo, suala la msingi hapa nasema kwamba ni vizuri elimu itangulie kwamba unapewa hii shilingi milioni moja lakini fanya biashara ambayo inalipa, labda kama ni kusafirisha mazao unaenda kuuza uhakikishe kwamba soko unakoenda ni la uhakika, lakini siyo sasa hivi mtu anarundikiwa hela haelewi cha kufanya. Kwa hiyo, ni vizuri sana tunaposema tunakopesha watu tuangalie kwamba elimu iwe ya kutosha na vyombo ambavyo vinapewa fedha wasichukue sehemu ambayo inariba kubwa kwa sababu inamu-*affect* mtu wa chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu suala la *SIDO* wengi wameizungumzia na kuitetea sana. Lakini hii *SIDO* mimi niko kule kwenye viwanda na

biashara kwa kweli inanyanyaswa kwani hela inazopewa inatia huruma ni ndogo sana lakini majukumu ni makubwa sana, Taifa linategemea *SIDO* sasa sielewe kwa nini tufanye utani na mambo ya *SIDO*. *SIDO* inafika mpaka kule kijijini kwangu kabisa. Lakini kuna Benki nyingine haziwezi kufika mpaka kule kwetu, kwa mfano, nizungumze ukweli kuhusu hii mikopo ya JK, hii mikopo ilikuwa ni mizuri sana lakini imeishia mjini kwenye Jimbo langu, kwa kweli hawakufaidika imeishia Makambako na Njombe Mjini, kule kwangu haikufika, kule Ilembula pia haikufika watu waliomba lakini hawakupata. Lakini *SIDO* ninavyoelewa inaweza ikasaidia sana. *(Makofi)*

Nilikuwa naongea na Mkurugenzi kuhusu kutuletea viwanda vya *SIDO* kule Jimboni kwangu akawa mwepesi sana yule Mkurugenzi na sielewi kwa nini yule Mkurugenzi mpaka leo anakaa na hicho cheo ilitakiwa apandishwe iwe ni *model* kwa sababu anafanya kazi nzuri sana. Nimemueleza nina tatizo la wananchi wangu kule Isindagosi kule, Itulahumba Njombe wale ni wafinyanzi wazuri wa vyungu, vile vyungu kama *SIDO* ikienda pale wakapeleka zile mashine za kuwawezesha mtaji, wawezeshwe masoko, wawezeshwe utaalamu basi vile vyungu tunaweza tuka *export*, tunaweza kupeleke Japan, Korea, Marekani, *South Africa* vile vyungu ni vizuri sana wale akina mama wanatengeneza vyungu vizuri sana. Nikamueleza vile vile kuhusu suala la kuleta viwanda vidogo vidogo kuhusu alizeti. Yule baba wa watu akasema Bwana nitatuma wataalamu, kwa hiyo, suala la *SIDO* siyo vitu vya kuchezea. Kwa hiyo, akituletea ule mtambo kiwanda cha kutengeza mafuta ya alizeti wananchi wetu watapunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna suala la mbao eneo langu kama kule Imalinyi kuna mbao, Kata ya Wangama pale Imalilo kuna mbao nzuri tu na kuna mandhari tu kwa hiyo, pale vikipelekwa viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya mbao watu wetu wataondokana na umaskini na kuna viwanda vidogo vidogo pale vinatakiwa viongezewe nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumze kuhusu suala la viwanda vikubwa, tuna mwekezaji amekuja kule Njombe anatoka Marekani anataka kutuletea kiwanda kikubwa tu cha *organic fertilizer*, hiki kiwanda nimezungumza sana mara kwa mara *through Tigi Company Limited*. Hawa watu wana mwekezaji ambaye amekuja jimboni kwangu anataka kuwekeza na sisi tumeamua kumpa eneo kubwa tu kama ekari 150 pale Muhelenge, Kata ya Wanging'ombe, Njombe. Sasa kile kiwanda kama Wizara ikishirikiana naye basi itakukuwa ni mkombozi mkubwa sana wa mwananchi wa kawaida kupata mbolea. Kwa hiyo, tunakuwa na kiwanda pale vinasaidiana na kiwanda kingine cha Minjingu. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba suala hili la kiwanda hiki kikubwa tusifanye kama ni utani, kiwanda hicho kipo kinachotakiwa ni kuwezeshwa ili tuweke umeme pale yaani miundombuni, umeme uwe wa gridi siyo umeme ule wa kukati kakati ambapo ni jirani na Makambako inawezekana. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri tuliongea naye akasema ata-*support* sana kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, hicho kiwanda ni *product* yake ni kutumia haya maganda ya karanga na maji machafu, sasa maganda ya karanga mtu anajiuliza yatapatikana wapi, maganda ya karanga yapo sehemu mbalimbali na zile karanga zenyewe tungetengeneza kiwanda cha sabuni hizi za kuongea na kufulia. Kwa hiyo, wenzetu ambao wanalima Dodoma,

Singida, Iringa na maeneo mbalimbali hiki kiwanda kitakuwa ni mkombozi sana kupata soko la karanga na kiwanda kitaendeshwa kwa faida kubwa *at the same time* tutakuwa na mbolea ya kutosha kiasi kwamba itasaidiana na hizi mbolea za chumvi chumvi na hizi za *organic*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naishauri Serikali inisaidie sana suala la hicho kiwanda kwamba isichukuliwe kwamba ni kitu cha mzaha mzaha, hapana, kwamba tusaidiane kiwanda hiki tukiweke mwaka 2009/2010 kianze *operation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie kuhusu suala la Ilembula pale kwamba ule ni mji mdogo, kuna wajasiriamali wengi, kuna kituo cha polisi pale kwa hiyo, tulikuwa tunashauri kwamba benki zianze kuwekeza pale...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili hiyo.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yono Kevela, sasa nilipokuita Mheshimiwa Yono Kevela nilimruka Mheshimiwa Benson Mpesya sasa nitamrejeshea hiyo nafasi yake ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Margreth Mkanga ajiandae.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kwa kuniona kwa jicho lako la huruma. Naomba na mimi nitumie nafasi hii kwanza kabisa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Viwanda na Biashara na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha gurudumu la kutimiza na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe salaam za pekee hasa hasa kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii Dr. Stergomena Tax, nimetumwa na wananchi wa Mbeya hasa wale ambao walikuwa ni wahanga wa moto wa soko la Mwanjelwa. Ni Wizara yako kwa sababu ya kuwa na Katibu Mkuu mahiri alitoa maeneo ya *SIDO* Mbeya yatumike kwa ajili ya soko la dharura kwa ajili ya wananchi waliounguliwa na soko la Mwanjelwa, wana Mbeya kwa ujumla tulifarijika sana na uamuzi wa haraka aliochukua Naibu Waziri na Katibu Mkuu aka *act* chini ya saa 24 jibu likawa limetolewa. Hao ndiyo watu tunaowataka katika dunia ya leo. Nakuomba sana Katibu Mkuu upokee shukrani hizi lakini Waziri naomba upokee kwa sababu mimi najua na wewe ni mchapakazi pamoja na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado naamini kuamini kabisa mnalo jukumu pia la kuhakikisha kwamba mnasukuma na kujenga mazingira ya kurahisisha fedha kutoka Hazina ziende kujenga soko jipya kwa sababu Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeomba

kama mkopo na hatuoni sababu uwezo wa kurudisha mkopo huo tunao tunachotaka Wizara itusaidie ku-*facilitate* hilo liwezekane ili tuwajengee wananchi wale soko la kisasa lakini wakati huo huo wakiendelea kutumia maeneo yale ya *SIDO* ambayo tulipatiwa. Lakini vile vile hata mdogo lazima umshukuru, naomba nimshukuru Meneja wa *SIDO* mkoa wa Mbeya, nilifanya naye kazi karibu siku mbili za matatizo yale naye alinipa msaada mkubwa sana. Naomba nimpongeze kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walau nimesimama na nikushukuru kwa kunipa nafasi hii tena. Ninaomba nirejee kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 58 juu ya ahadi ya kufufua viwanda ndani ya Jiji la Mbeya na bahati nzuri ukipitia Ilani yote moja kati ya majukumu ambayo Wizara hii imepewa na lipo *specific* mno kuliko mambo mengine ni kufufua viwanda ndani ya Jiji la Mbeya, *so specific!* Lakini mwezi wa nne niliuliza lile swali nilipokuwa nauliza swali kwamba ni lini hatua zitachukuliwa za kufufua viwanda Mbeya lengo langu lilikuwa ni kuikumbusha Serikali kwamba mliwaahidi wananchi wa Mbeya sasa mnapaswa kutekeleza hilo lakini jibu nililojibiwa hata kule Mbeya walishangaa sana halikuwa la makini mnao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lilikuwa linauliza juu ya kufufua viwanda Mbeya, hii ni *Ministry of Industries,* matokeo yake mnazungumza habari ya viwanda vya chai Rungwe ambavyo hivyo ni *Agro Based Industries* ambavyo mahali popote kwenye mazao hivyo ndivyo viwanda vya kwanza hivyo. Viwanda vilivyopo Mbeya ambavyo tulitakiwa tupate majibu ni Zana za Kilimo (ZZK) lini kitafufuliwa? Katika mapinduzi haya tunayozungumza juu ya *green revolution* hatuwezi tukabadilika kama tutaendelea kuagiza majembe kutoka China, Sepeto kutoka *South Africa*, matoroli kutoka China wakati tulikuwa na ZZK na kilikuwa kinatoa zana zote hizo na zilikuwa ni bora na imara, hicho ndiyo kitu cha kwanza wanachotaka kusikia wananchi wa Mbeya ni lini ZZK itafufuliwa? Kama mwekezaji alinunua kiwanda hicho na ameshindwa kukiendeleza ninafahamu *role* ya Wizara ni *facilitation* mmehakikishaje hilo kwamba linatekelezeka? *(Makofi)*

Wananchi wa Mbeya wanataka kuona kiwanda cha kusindika mafuta cha *Mbeya Industries* kinafufuka, zile mashine zilizong'olewa na kupelekwa kusikojulikana zirudi ili wale watu wapate ajira pale. Watu wa Mbeya wanachotaka kuona ni kiwanda cha sabuni cha *Hi - Soap* kinafufuliwa *whether* mwekezaji ni Serikali au ni nani lakini ni lazima kiwanda kile kifufulie na kifanye kazi, hayo ndiyo ambayo wanadai watu wa Mbeya. Mheshimiwa Waziri watu wa Mbeya wanataka kiwanda cha nguzo kilichokuwa pale Iyunga kirudi badala ya ninyi kukazana kuagiza nguzo kutoka *South Africa* wakati kiwanda tulikuwa nacho, malighafi ya viwanda hivyo tunavyo, wananchi wa kufanya kazi hiyo tunao, uki-*process* nguzo ya Tanzania haifiki hata shilingi 50,000/= lakini mnaagiza *South Africa* na inakuwa shilingi 500,000/= nguzo moja. Kiwanda cha nguzo kirudi pale Mbeya. Nataka nimkumbushe Waziri kwamba kingine ambacho wananchi wa Mbeya wanasema kifufuliwe ni kiwanda cha nyama, walitoa mashamba yao wakasema na kiwanda kije! Wanataka kuona vitu hivi vinatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha mwisho katika viwanda vya kufufuliwa ni kuongeza malighafi ya *Mbeya Textile* yaani kiwanda cha nguo cha Songwe pale Mbeya.

Kiwanda kile tumeki-*input* wenyewe, walikuwa wanategemea pamba kutoka Chunya ilikuwa ndiyo malighafi yao pale na wakati huo *capacity* ilikuwa ni kuwaajiri Watanzania zaidi ya 3,000 lakini leo hii wanaajiri watu 500 tu wanakuambia Mheshimiwa Mbunge pamba tunayosindika inatoka Cameroon na Nigeria *all the way* kutoka kule. Nilipopiga kelele katika Bunge hili kuhusu kilimo cha pamba Chunya nikaambiwa mtatoa zao la mbadala na zao la mbadala ni lipi? Na nikawapa mifano namna gani Msumbiji na Zambia wameweza kupambana na huyu mdudu miaka 40 ya uhuru tunashindwa na huyu mdudu mmoja tu huyu, si tukusanye Maprofesa wote wamshughulikie akina Mwalyosi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeona niwakumbushe kwamba viwanda tunavyozungumza siyo vile vya kusindika chai mnasema vimefufuliwa na ninaomba niwakumbushe kwamba kiwanda cha *Pepsi Cola* cha vinywaji na *Cocacola* vile tayari ndiyo tulichokuwa tunatamba kama Chama cha Mapinduzi kama ndiyo uzuri wa sera ya ubinafsishaji, hilo lilishapita tulishabinafsisha matunda yake ni pamoja na kufufuliwa kwa viwanda hivyo tulichokuwa tunasubiri sasa ni hivi viwanda ambavyo nimevizungumza. Lakini naomba nimwambie Waziri kwamba katika hili kwa sababu liko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tupo pamoja siyo la kwake peke yake. Mimi tu naomba nitoe ushauri. Naomba niishauri Wizara, cha kwanza katika kutimiza hii ahadi *EPZ*, kwenye *min tiger plan* ya mwaka 2020 *out rich* ya Mbeya ilikuwa ni mwaka 2008 na tatizo mlisema kwamba ni eneo, tumetoa ekari za kutosha pale Iwambi kwa ajili ya *EPZ*, naomba hili liharakishwe kwa sababu lina mustakabali wa Taifa. Tusingependa kumuona Rais wetu mwaka 2010 anatangatanga, tunataka tumsukume tu amalize kipindi chake cha pili bila migogoro haya yote yatimie, kama kuna watu mnanyemelea sisi katika utaratibu wetu tunajua ana miaka yake mitano inakuja tumuombee kheri tu na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba kiwanda cha nyama cha Mbeya ni muda mrefu sasa kifufuliwe, wale wananchi waliacha kulima wakaitii Serikali na ninyi basi timizeni basi nafasi yenu, kile kitendo cha kusema unajua sasa tumeachia *private sector*, *private sector* haikuomba kura tulioomba kura ni sisi tunayo *role* ya *facilitation* Serikali iliyo imara ina vigezo vinne tu vigezo hivyo vingine ni vikorombwezo. Kwanza ni *democratic*, *efficient*, *effective* na halafu vile vile ni *facilitative* na ndiyo hapo ninapotaka kuwabana ninyi *role* yenu ya ku-*facilitate* kila jambo liende hata kama ni la *private sector* ndiyo hapo tunapogombana na mimi lakini tupo pamoja. Naomba tupate majibu ya pamba ya kusindika pale *Mbeya Textile Mills* haiwezekani utafiti uchukue miaka mitano bado jibu halijatoka la yule mdudu wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninaomba kupitia kwako Kiwanda cha ZZK, *Hi-Soap* na bahati nzuri nikwambie tu maeneo haya ninayoyazungumza yote yamekaa pamoja yakitekelezwa haya Mbeya imekwenda na Tanzania imekwenda, Malawi, Zambia, *DRC* wote tutakuwa tumeteka. Ninawaomba kipindi hiki tufanye kazi inayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtakie Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wetu utekelezaji mwema katika kuhakikisha kwamba viwanda vinafufuliwa kwenye Jiji la Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze na pongezi. Kwanza naomba kuchukua fursa hii, kuwapongeza Wananchi wa Jimbo langu la Ludewa, kwa kuwa na imani na Mbunge wao katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Niwapongeze kwa maandalizi na mapokezi mazuri waliyomwandalia na kumfanyia Mheshimiwa Rais, alipotembelea Ludewa wiki moja iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashukuru kwamba, kwenda kwake kumethibitisha haya yaliyojitokeza katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa vile mambo haya yanayohusu Mchuchuma na Liganga yalizungumzwa kirefu sana Ludewa na kwa kweli ndivyo yalivyojitokeza katika Hotuba hii. Kwa hiyo, vilevile naishukuru sana Wizara, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa kuja na hotuba ambayo binafsi imenikuna sana na nimeridhika. Nimekuwa nafuatilia mambo ya Wizara hii, kwa sababu ya mambo ya Mchuchuma na Liganga; kwa kweli mmeniridhisha na kunifurahisha sana na *Wananchi* wa Ludewa wanawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nakishukuru chama changu cha Mapinduzi, kwa kuweka katika Ilani yake msimamo na mwongozo kwamba, madini ya Liganga na Mchuchuma yaanze kufanyiwa kazi katika kipindi cha miaka mitano hii. Ishara zinaonyesha kwamba, inatekelezwa, bila shaka isingewekwa kwenye Ilani pengine tungekuwa tunazugumza mengine, lakini kwa sababu ya msisitizo huo, nashukuru kwamba sasa mambo yanaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mchango wangu utajikita katika kuzungumzia Liganga na Mchuchuma, maana sehemu kubwa ya hotuba hii ni masuala ya Liganga na Mchuchuma. Nianze kwa kuzingatia maneno aliyoyatumia Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kuanzia kifungu cha 32 – 40 ambapo kwa mfano katika ukurasa wa 22 anasema: "Wizara inakamilisha mchakato wa kuwapata wawekezaji katika miradi ya makaa ya mawe na Mradi wa Liganga." Inakamilisha mchakato wa kuwapata wawekezaji, na-*note* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nanukuu: "Mchakato wa kuwapata wawekezaji wa Kitanzania, watakaoingia ubia na *NDC*, umefikia hatua ya mwisho." Kwa hiyo, mchakato wa kuwapata wawekezaji wa Kitanzania watakaoingia ubia na *NDC* kuzalisha chuma ghafi, umefikia mwisho. Kinachoonekana hapa ni kwamba, wawekezaji wapo, kwa hiyo, uwezo upo na nia inaanza kuonekana ipo, *political will* inaelekea ipo, sioni sababu kwa nini miradi hii isianze sasa. Nataka kuwa na imani si kama Thomaso anayezungumzwa katika Biblia, naamini kwamba, tumeshajiweka vizuri kuhakikisha kwamba miradi hii inaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba, *NDC* itahakikisha kwamba, inawatambua na kuwaandaa Watanzania na italinda maslahi ya Wananchi wa Taifa hili; nitalizungumzia huko mbele kwa nini hili naliunga mkono.

Mwisho, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema: "Wizara itakamilisha zoezi la uwekezaji katika Miradi ya Chuma na Makaa katika mwaka 2008 na 2009." Hizi kwangu ni *statements* nzito, zenye mwelekeo mzuri wa kuleta maendeleo Tanzania kwa kutumia Miradi ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe kule Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzingatia maslahi ya Watanzania, ili kutambua uwepo wa Watanzania na Wanaludewa na ili kuwaandaa Watanzania hawa katika miradi hii ambayo sasa inaelekea kuanza, natoa mawazo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika miradi hiyo, ningependa kuona kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Serikali Kuu na Wananchi wa Ludewa wenye uwezo na Watanzania wengine, wanakuwa na hisa katika miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vilevile nitapenda kuona katika mchakato mzima wa kufikia maamuzi makuu ya mwisho, Wananchi wa Ludewa kupitia mwakilishi wao ambaye ni Mbunge, anahusishwa kikamilifu kujua maslahi ya Wananchi wa Ludewa na Watanzania katika mikataba hiyo imekaa kaa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, pia tuombe wawekezaji hao wawe na bajeti ya kutosha kuweza kuwaelimisha Wanaludewa na Watanzania kuhusu miradi inayokuja ili wajiweke sawa na kuweza kufaidika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kwa kuwa Serikali imekubali kujenga Chuo cha Ufundi Ludewa, kwa kuhusisha madini ya Liganga na Mchuchuma, tunaomba basi Serikali ifanye hima kuhakikisha kwamba, Chuo hicho kinaanza kujengwa mara moja ili vijana wetu wapate mafunzo ya ufundi, waweze kushiriki katika maendeleo haya yanayoletwa na migodi hii miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba, kwa vile kiwanda cha chuma ghafi kinaweza kuanza muda wowote kutoka hivi sasa, naomba nizungumzie suala la fidia. Mheshimiwa Rais, alipokuwa Ludewa alilizungumzia suala hili kwamba, Wizara na *NDC* wahakikishe kwamba, Wananchi wa Mkomang'ombe na Liganga wanafidiwa kikamilifu. Wapate fidia yao kabla miradi haijaanza, hivi ndivyo alivyoelekeza. Nami kama Mbunge wa kule, nipo imara kweli kweli kufuatilia hilo kuhakikisha kwamba, fidia zile zinatolewa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumze kwamba, fidia zile hazitatosha kwa mfano, kwa kuwaambia wananchi wale kwamba, mwembe watawalipa Sh. 20,000, itakuwa ni kuwaonea kwa sababu mwembe ni mmea ambao umekuzwa kwa zaidi ya miaka hata mia moja na unazaa matunda kwa miaka zaidi ya mia moja na matunda ni mengi ambayo kwa msimu mmoja unaweza kupata zaidi ya Sh. 20,000.

Kwa hiyo, kumfidia mtu Sh. 20,000 kwa mwembe ni kumwonea. Kwa hiyo, haya ni kati ya mambo ambayo itabidi tuelewane vizuri kuhakikisha kwamba, *proper* fidia kwa wananchi wale inafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kutokana na uwekezaji na viwanda hivi kuanza kule Ludewa kwa kutumia makaa ya mawe, Mchuchuma na Chuma cha Liganga na kwa kuwa naamini kwamba, itavuta watu wengi sana kwenda kule, najua Watanzania wengi sana watahamia kule, naomba vitu vifuatavyo vizingatiwe, pengine Serikali iangalie itayafanya vipi haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuna haja ya kuwa na *land use plan* ya maeneo yanayozunguka maeneo ya migodi hii ili kusiwe na fujo katika matumizi ya ardhi. Tungependa Ludewa kuonyesha *best practices* katika *mining* na viwanda kwa kuwa na mipangilio mizuri, wapi watu walime chakula cha kulisha wafanyakazi, wapi kuwe na mifugo kwa ajili ya kupata maziwa na nyama na wapi kuwe maeneo ya makazi. Itakuwa ni vyema tukijiandaa mapema kabla fujo hazijaanza, haya mambo yawe yamewekwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni hili linalokwenda na hilo; kwa vile tunazungumzia miundombinu, viwanda vya chuma na umeme na katika miundombinu kuna reli na barabara, naomba tuanze kufanya *strategic environment assessment* ili tuweze kujua mapema wananchi walioko kule wataathirika vipi na kufaidika vipi na pia Mkoa na Taifa vitafaidika vipi katika miradi hiyo yote *in an integrated fashion.* Vilevile kwa kuzingatia kuwa kiwanda cha kuzalisha chuma ghafi huenda kitaanza, kitahitaji kupeleka mitambo na mashine nzito kule Liganga, barabara iliyopo ni nyembamba sana, haiwezi kustahmili kubeba mizigo hiyo.

Tulizungumza na Mheshimiwa Waziri kuhusu kuwasilisha hoja katika Wizara ya Miundombinu, kuhusu kutengeneza barabara ikiwezekana ipanuliwe au kuwekwa lami kutoka Itoni – Mkiu - Liganga. Sisi katika Mkoa wetu kupitia *RCC* tuliwasilisha na nina imani kabisa wenzetu wa miundombinu wanalishughulikia suala hilo lakini naomba Wizara hii iweke msukumo kwenye suala hilo la sivyo kusema viwanda hivi vitaanza kesho au keshokutwa ni ndoto za alinacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nizungumzie suala ambalo lipo nje ya Ludewa; Kiwanda cha Magadi Lake Natron. Nanukuu hapa kwenye hotuba imesemwa: "NDC imejielekeza katika kukamilisha uchambuzi wa masuala ya mazingira…" Naomba niseme hivi; hapa tunapozungumzia suala la mazingira, naamini kwamba ni *broad terms.* Nimesema mara nyingi na nitaendelea kusema na *NDC* ni rafiki zangu sana wasinielewe vibaya, lakini kutetea mazingira ni kwa faida ya nchi hii na kutetea rasilimali za nchi hii ni kazi yetu. Tunaojua madhara ya kufanya vitu bila mpangilio tunasema, Serikali lazima iandae *baseline data* kuhusu hali ya *hydrology*, *biology* na *ecology* ya maeneo yale ili taarifa hizo zitumike kuweza kujua kitatokea kitu gani iwapo kiwanda hicho kitatekelezwa. Nitaomba sana Mheshimiwa Waziri, alizingatie hili la sivyo hata ikifanya *EIA* sisi wengine bado tutaipinga mpaka tuone tutafikishana wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ingawa si la mwisho kwa umuhimu ni suala la stakabadhi maghala. Nimesoma katika ukurasa fulani ambapo wanasema kuna makampuni karibu matatu yanaomba kuandikishwa, moja likiwa ni MBICCCO Makambako; naomba hawa waandikishwe upesi iwezekanavyo. Hawa ni kwa ajili ya kahawa, sisi Ludewa tumeanza kwa *speed* sana kilimo cha kahawa mpya inayomudu magonjwa na inayozaa haraka. Tunategemea kujiunga na utaratibu huu wa stakabadhi maghalani ingawa Ludewa tuna maghala yaliyojengwa na Wajapani mara nyingi yanatumiwa na watu wa *SGR*, lakini ni maghala yetu. Ingawa ni mali ya Wizara ya Kilimo, lakini tungeyatumia yale. Pengine tuje na hoja ya kutaka kuandikisha sisi wenyewe tuwe na kampuni yetu ili tuweze kuyatumia yale maghala vizuri kwa utaratibu huu mzuri ambao utatuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema nimeifurahia sana hotuba hii na nina imani sasa maendeleo makubwa yataanza kupatikana kwa Ludewa na vilevile kwa Tanzania, kwa kutumia rasilimali hizi kubwa za Kitaifa ambazo kwa miaka mingi zimekaa *idle* bila kutuletea faida yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Kwanza, naipongeza Wizara kwa kupitia Watendaji wake nikianzia na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi zote muhimu ambazo zipo chini ya Wizara hii, kwa kazi zao nzuri na kutuandalia hotuba nzuri. *(Makofi)*

Kwangu hotuba hii ni nzuri, kama ikitekelezeka sidhani kama miaka miwili ijayo ningekuwa na haja ya maswali au kitu chochote kwa sababu ina matumaini kiasi kwamba, unaona Minjingu inajengwa leo, reli ya kwenda Mchuchuma itajengwa kesho kutwa, yaani *is so excite;* inatia matumaini sana. Basi nawatakia kila la kheri katika haya ambayo yametufanya tuweze kusisimka, Mungu awasaidie muweze kuyatimiza; nadhani atatimiza kidogo kidogo kwa sababu nitakazozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Wizara kwa kupitia Wakala wake wa Vipimo na utaratibu wa stakabadhi ghalani umesifiwa. Suala la vipimo lumbesa halijakwisha lakini limepungua. Kwa kweli wamejitahidi hata wafanyabiashara wengine sasa wanatii kwa kuweka ujazo unaotakiwa na Serikali na ambao hautawapunja wakulima ambao ndio mara nyingi walikuwa wanaibiwa kwa njia hiyo. Kwa upande wa mafanikio ya utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ya maghala tunaendelea kuusifu, tunaomba uenezwe si kwa haya mazao yaliyosemwa bali uenezwe kwa kila kitu. Maghala tunaweza kuyajenga, ili kila kitu kiwe *sold* kiweze kupata amana na nyongeza ya fedha inapouzwa ili wahusika waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Shirika la *BET,* lililoandaa na litakaloendelea kuandaa Maonyesho ya Sabasaba kule Dar es Salaam. Kwa nini nawashukuru? Katika jitihada ya kuona kwamba, kuna umuhimu wa akina mama wenye ulemavu nao wanaweza kushiriki kikamilifu katika Maonyesho hayo kwa

kupeleka bidhaa, nilionana na Mheshimiwa Waziri, akanipeleka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, naye akanielekeza kwa wahusika. Kwa taratibu za siku mbili tu nilifanikiwa, akina mama wenye ulemavu wa Shirika la Sauta waliweza kupatiwa sehemu ya kuuzia bidhaa zao. Wakurugenzi wa taasisi hii waliweza kupeleka matangazo *TBC*; nawashukuru sana *TBC* walitangaza kana kwamba kile kikundi ni kikubwa na kimetengeneza mambo ya maajabu, wakauza bidhaa zote, wakaishiwa ikawa hawana cha kuuza. Nawashukuruni sana kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lile waliwapa bure na waliahidi kwamba litakuwa la bure kwa miaka yote ambayo vikundi vya akina mama wenye ulemavu wataweza kushughulika au kushiriki kikamilifu katika Maonyesho yale. Nawashukuru, huko ndiko kuwawezesha; kumwezesha mtu usimpe pesa, kumwezesha mtu umpe namna ya kuweza kuzalisha na kuuza kila siku. Sasa wameshapata soko, ninalowaomba waendelee kutengeneza vitu vizuri zaidi kusudi waweze kumudu ushindani wa bidhaa ambazo watazitengeneza pamoja na akina mama wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kubwa, inaanzia tangu Mchuchuma mpaka Lake Natron, inakwenda kwenye samaki mpaka kwenye kasa, yaani ina majukumu makubwa; ina wajibu wa kuhamasisha na kuwezesha hata sekta binafsi ziweze kuimarisha au kujenga viwanda vipya na vikubwa na mambo yote hayo. Pamoja na uhamasishaji huo, ambao Wizara hii imepewa jukumu kwa upande wa viwanda, naona kwa muda huu wa sasa, kwa Watanzania walio wengi kumudu kuanzisha viwanda sawasawa ni tatizo.

Tunajua hawana mitaji ya kutosha, lakini hata taratibu za uanzishaji viwanda hivyo naona bado urasimu wake ni mkubwa. Mtu unazunguka na taratibu mpaka unakata tamaa, kile kijimtaji ulichokiweka mwisho unakila, kwa hiyo, hakuna kinachofanyika.

Licha ya hayo, wafanyabiashara hawa wa viwanda hata hivyo vidogo vidogo, bado wanalalamika kwamba, kodi ni nyingi kwao ukilinganisha hata na wawekezaji kutoka nje. Kwa hiyo, hili naomba tuliangalie vizuri kwa sababu linakatisha tamaa na hivyo basi katika sekta hii ni Watanzania wachache ambao watamudu labda kwa kununua hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana pale hotuba ilipoeleza kwamba, kuna mpango wa kuandaa maeneo maalum ya kibiashara ambayo baadaye yatakuwa ni *satellite towns* ndani ya viwanda, makazi na mengine yote ambayo yatawezekana. Ni kama Shajra ya namna yake ya Dubai kule ambayo sasa tunataka kuileta hapa nyumbani, hayo ni maendeleo. Naendelea kushauri katika maeneo hayo yote mapya ambayo yatajengwa, tujiimarishe katika mambo ya uzalishaji ya kibiashara. Mahitaji maalum kwa watu wenye ulemavu yazingatiwe kwa sababu katika maeneo hayo tunaweza kupata wafanyabiashara wenye ulemavu, wataalam wenye ulemavu na taasisi zao. Hilo lizingatiwe kikamilifu ili miundombinu hiyo iweze kufaidisha wote ambao tunahusika katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la fidia. Katika maeneo hayo hayo ambayo yatatwaliwa ili *EPZ* au *SEZ* zianzishwe, kuna maeneo naamini watu itabidi wahamishwe kwa sababu ni mipango ya sasa na watu walikwishatulia bila kujua nini kitatokea baadaye lakini vyote ni maendeleo. Ninachoomba, nikiungana mkono na mchangiaji aliyenitangulia kwamba, watu walipwe fidia zao zote kikamilifu kabla ya shughuli kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni desturi kila tunapoanzisha kitu kipya, wananchi wanahangaika na kulipwa fidia, wanalipwa ama pungufu au hakuna kabisa, hebu tukwepe migogoro mapema kabisa kati yetu sisi na wananchi, kati ya Serikali na wananchi na kati ya wawekezaji na wananchi. Kwa hiyo, malipo yafanyike mapema kabisa kabla chochote kile hakijaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wamachinga wenzangu wamelizungumzia, lakini ukiona jambo linazungumziwa na wengi; ujue ukweli unakuwa mwingi zaidi. Hawa tunawafahamu, maduka ya mabegani na wengine wana mikopo na wametulia kidogo kwenye maeneo finyu ya kubanwa banwa, hii desturi ya kuwahamisha bila mpangilio tuiache na hata hizi *EPZ* zinazojengwa kama tutajenga sehemu za biashara, hebu basi tuwafikirie kuwapangia vizuri zaidi, pamoja na kwamba hapa Wizara inatoa maelekezo, wanaohusika ni Halmashauri zetu; Halmashauri nyingi hazitekelezi haya, zinangoja wametulia halafu baadaye wanawatimua timua. Ile mikopo midogo midogo wanayoikopa watailipaje? Kwa hiyo, tuwafikirie na kuwaandalia vizuri; tumekiri hapa wana-*contribute* kiasi kikubwa kabisa kwenye mambo ya biashara na Pato la Taifa ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba kabisa hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inashughulikia mambo ya viwanda na mengi haya yatakwenda Halmashauri ndiko viwanda vitajengwa huko na vitu kama hivyo. Sina uhakika kama tuna Maafisa Biashara wangapi katika Halmashauri zetu? Naomba nihakikishiwe je, tuna Maafisa Biashara katika Halmashauri zetu na kama hawapo; maendeleo haya huko chini nani atakayeweza kuya-*monitor* sawasawa na kuwaelekeza wananchi cha kufanya?

Kama hawapo, mkakati maalum ufanyike kwa sababu naona kama sasa tupo katika hali ya kujaribu kujiendeleza katika mambo ya biashara, viwanda na masoko; hawa waweze kuchukua nafasi yao ya kufanya kazi kikamilifu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 31 wa hotuba, nalipongeza Shirika la Viwanda Vidogovidogo *(SIDO),* limetoa mafunzo kwa watu kama elfu tano na mia saba hivi kwa mwaka uliopita na nadhani Mradi huu au jitihada hizi zitaendelea. Sasa napenda kufahamu; kati ya hawa wajasiriamali elfu tano na mia saba waliofaidika na mafunzo ya *SIDO*, ufundi na mengineyo; ni watu wangapi wenye ulemavu walifaidika na mafunzo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni ufinyu wa Bajeti wa Wizara. Kama wenzangu walivyotangulia kusema, hapa ndipo ninaposhindwa kuelewa kwamba; hivi tuna nia kweli katika mipangilio yote hii tuliyoiweka au tunayojiwekea au tunayozungumzia kwa fedha hizo chache; si *TIRDO* ambako ndiko utafiti unafanyika

huko, Wizara yenyewe, hizo *satellitetown* sawa. Tunasema kwamba, mengine tutapata mikopo kutoka maeneo mbalimbali lakini sisi wenyewe nguvu yetu zaidi iko wapi?

Kama wengine walivyochangia, tukitegemea wafadhili; je, wakigotesha fedha zao, Wizara hii isiletewe vya kutosha kama walivyoahidi; hivi tunafanyaje na bado tuna hamu ya kubadilisha mambo mengi katika viwanda, biashara zetu na masoko yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, mimi ni Mjumbe mmojawapo katika Kamati hii, lakini kwa kweli mwakani Serikali ifikirie vipaumbele na Wabunge tutajaribu kusaidia; kwamba, pamoja na elimu na maji, nadhani Wizara hii nayo inapaswa kusonga mbele kidogo kwa sababu ndiyo tumeambiwa sekta kipaumbele itakayoweza ku-*link* mambo mengine yote; mkulima atazalisha lakini bila kuuza itakuwaje? Mkulima atazalisha, tunahangaika hapa, bila kuongeza thamani kwa viwanda vya kuongeza ile thamani, mambo yatakuwaje? Kwa hiyo, tutarudi pale pale. Nashauri na naomba sana bajeti ya Wizara hii mwakani iweze kuongezeka ili iweze kumudu majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina mengi, hii hotuba imeandikwa vizuri sana, kama nilivyosema, tumekuwa *excited;* sasa lini atatimiza tuombe Mungu yatimizwe haraka haraka ili Watanzania tuweze kufaidika. Naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kwanza kabisa, kabla muda wangu haujakwisha, naomba niulize swali ambalo nategemea litajibiwa. Kwa nini Kiwanda cha Sementi katika Mikoa ya Ziwa hakijajengwa? Sula hili limetufikisha mahali tunarudi nyuma katika *construction industries* na huwezi kujenga viwanda kama huwezi kujenga mahali pa kufanyia kazi. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo linahitaji majibu, tunaweza kujenga viwanda vingine vyote; kwa nini tusijenge Kiwanda cha Sementi na ni suala ambalo limeulizwa muda mrefu katika Bunge hili na kuna ahadi ambazo zilizokuwa zinatolewa za kujenga kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ningependa nifahamu kwa nini usindikaji wa samaki wananchi wa kawaida hawajawezeshwa, ambao wanafahamu namna ya kuvua samaki na wanaishi na hao samaki ili tuongeze ajira tuliyoizungumza katika mpango wetu na mkakati wetu wa kuongeza ajira; na pia kuongeza thamani ya mavuno?

Ukiangalia watu wanaotoka Kanda ya Ziwa Victoria na hasa wanaotoka katika Mkoa wa Mwanza ambako kuna harakati nyingi za uvuvi na ukaangalia wanaotoka katika Ukanda ya Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na katika Bahari ya Hindi, tatizo ni kwamba, Sekta hii ya Uvuvi imeachwa nyuma hasa katika kusindika mazao ya samaki ambayo yangetuletea kipato kikubwa sana; kwa sababu mazao ya samaki yanahitajika sana duniani. Hakutakosekana soko la kuuza samaki. Sasa mimi ningependa nijibiwe; hasa tatizo ni nini; kwa nini tusiwawezeshe wavuvi kuifanya hiyo kazi; kama wanaweza kuvua samaki; kazi ambayo ni ngumu zaidi; kwa nini wasiwezeshwe kwa kufundishwa kusindika mazao yao katika hali ya ubora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ambazo zimepiga hatua katika viwanda, wana utaratibu; ukiangalia historia ya India, India walienda hatua kwa hatua, walichagua kwanza mazao ya ngozi, wakachagua *Textile Industry* ili waweze kutengeneza nguo kwa sababu walikuwa na uwezo wa kulima pamba, wakaenda hatua kwa hatua na katika maeneo hayo wakapeleka nguvu ambayo iliwawezesha kuwa na viwanda vya kuweza kutengeneza mazao katika maeneo hayo. Je, isingekuwa vizuri kama Wizara inayohusika na sisi ingekuwa na ratiba maalum?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitumie mfano wa Jiji la Mwanza. Jiji la Mwanza bahati nzuri lina maji ya kutosha, lina umeme wa kutosha, lina watu wa kutosha na wanalima pamba, wanavua samaki na kuna madini; sasa kama tungekuwa na utaratibu kama wa India eneo hili lingesaidiwa kwamba liwe maarufu katika utengenezaji wa nguo. Sasa swali MWATEX na MUTEX vipo katika hali gani? Je, tunaposema ubinafsishaji tutafika kweli kama hatutabinafsisha na kuweka jicho la Taifa katika viwanda ambavyo ni muhimu vya kutuondoa katika umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi Mheshimiwa Mbunge mmoja kutoka Zanzibar aliuliza swali juu ya Viwanda na akajibiwa karibu viwanda vyote vimekufa wakati viwanda hivyo vilikuwa na nguvu sana. Nadhani vimekufa kwa sababu ya kuamini ubinafsishaji. Kiwanda cha Ngozi Mwanza kiko wapi? Sasa hatukatai ubinafsishaji, lakini ukishabinafsisha ni kama unamwambia mtu ya kwamba ninakupa eneo hili ulifanyie kazi. Kweli Taifa tunaweza kujivua majukumu ya kuangalia waliochukua hivyo viwanda wamefanya navyo nini, kwa sababu tumerudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata jibu kuhusu Kiwanda cha Tanneries Mwanza na ninarudi pale pale ya kwamba, katika Jiji la Mwanza kuna mazao ambayo wangeweza kuambiwa tu Wananchi wa Jiji la Mwanza wangetegemewa kutengeneza viatu, mikanda na vitu vyote vinavyotokana na ngozi ili kuweza kukidhi mahitaji ya soko la nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia kwa makini tunanunua vitu hivyo kutoka nje na Waziri ameleta *quotation* nzuri katika hotuba yake ya kwamba, lazima tununue kilicho chetu. Sasa hivi ukienda madukani hakuna kitu kilicho chetu! Sasa tutakapokuwa tunazalisha tumekwishabana soko na siasa za Wazungu walipokuwa wanafanya *industrialization* hawakuwa wapumbavu, walibana kwanza masoko wakahakikisha kwamba, wameacha nafasi ya kutosha katika eneo lao ili waweze kuzalisha na kununua bidhaa zao na Wachina walifanya hivyo hivyo na katika kufanya hivyo sasa wanaitawala dunia; kwa sababu walijiimarisha, wakatosheleza soko la ndani na baadaye sasa wakasambaa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuwezi kufanya yote mawili; huwezi kuacha biashara holela halafu ukategemea kuwa na soko la bidhaa unazozalisha. Nadhani masuala haya yote lazima tuyaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nisisitize la muhimu ni kuwa na ratiba ya *industrialization* Tanzania. Wizara itusaidie, iwepo ratiba ya kwamba mwaka huu mpaka mwaka huu tunajikita katika mazao yafuatayo na mwaka huu mpaka mwaka huu tunafundisha wataalam wa aina Fulani; hao wataalam waliotajwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni wachache mno. Ukifundisha watu 90 kusindika samaki ni kama mchezo, lakini unahitaji ukijite hapo na uandalie wataalam watakaoweza kuifanya hiyo kazi, lakini uandae na wakulima, wavuvi na wafugaji waweze kufanya kazi hizo katika sehemu zao. Kwa sababu *industrialization* haikuanzia kwenye viwanda vikubwa; ilianzia katika familia ikaenda katika Jumuiya mpaka ikawa ya Kitaifa. Kwa hiyo na sisi tusije tukajidanganya ya kwamba, *industrialization* tunaizungumza, tutaweka viwanda vya Kitaifa bila ya kuwa na viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niungane mkono na Mheshimiwa Basil Mramba, ambaye amezungumza vizuri sana juu ya viwanda vidogo vidogo. Tungekuwa na viwanda vidogo vidogo kwa mfano vya pamba, nyuzi zingeweza kutengenezwa katika jumuiya ndogo ndogo na tukahakikisha kwamba nyuzi hizo zimetengenezwa kwa ubora na ndivyo China walivyofanya; tukazipeleka katika soko ambalo ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, watu hao wangekuwa wanajiajiri katika mazao wanayoyazalisha na tunaweza kwenda hivyo hivyo katika mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa pia nizungumzie kidogo kuhusu uwekezaji. Tunamwezeshaje Mtanzania kutengeneza hata kiwanda kidogo? Nimekuwa nikiuliza kiwanda kidogo cha Maji, naambiwa mtambo mzima ni shilingi milioni 40. Kwa hiyo, unakuta kwamba, kama Wilaya ya Ukerewe tuna chemchemi nzuri tu za maji safi; nilikwishayapima katika *Bureau of Standards* ni maji safi. Leo unaenda kumwambia Mkerewe wa kawaida ajenge kiwanda cha shilingi milioni 40! Tutakachokipata, kama hatuangalii hatutakuwa tunajenga uwezo wa watu waliopo katika eneo ambalo linatoa mazao hayo, tutakuwa kila mara tunaleta mtu kutoka mahali pengine kuja kuzalisha na kutengeneza, ingawa hatukatai uwekezaji, lakini nadhani tumelemaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno uwekezaji tumelizidisha mno, imekuwa kila mtu anafikiria mwekezaji atoke nje ya nchi, mwekezaji wa kumjenga ndani ya eneo letu hatujamfikiria na kama ni katika kilimo cha korosho, mwekezaji awe ni yule mkulima wa korosho yeye ndiye awe anawekeza. Tuna mifano, wakati pamba ilipokuwa imenawiri, *ginning* na kila kitu, kilikuwa kinafanywa na wakulima wenyewe ikiwa ni mali yao. Kwa nini sasa tusirudishe mawazo yetu kwa wananchi wetu na kwa vijana wetu ambao hawana ajira; tawaandae ili waweze kuwa ndiyo wawekezaji na kama ni kuleta taaluma basi tuweze kuleta taaluma ya kuwasaidia tukiwa na matumaini ya kwamba wale wataondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa tumelemaa; tafsiri ya uwekezaji imekuwa kwa Kiingereza ningesema, *replacement* ya mzawa. Najua wengi wanalitafsiri vibaya neno hili, mimi nitalitumia vizuri tu; mzawa ni yule kama ni Msukuma kwenye dhahabu mfundishe basi ajue kuichonga hiyo dhahabu, lakini anaona dhahabu inampita tu mradi anaambiwa wewe pisha au kama analima pamba akishafunga lile furushi ni kupeleka

*ginnery* hana habari tena na ile pamba, hafundishwi kwamba na yeye ile pamba angeweza kuitumia namna gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani tunajinyima nafasi ya kujenga uwezo wetu sisi wenyewe na kwa maana hiyo, ukitulinganisha Tanzania na Kenya; wenzetu wamejenga vipaji vya ngazi ya kati na ya juu. Usipokuwa na vipaji vya kati ambavyo vinatumia rasilimali iliyopo katika eneo, huwezi kufanya *industrialization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningependa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam waliopo katika Wizara hii, watusaidie kuwa na ratiba ya *industrialization* mkoa kwa mkoa, eneo kwa eneo, sekta kwa sekta na mazao kwa mazao ili angalau tuweze kupima kila mwaka Wizara inapowasilisha bajeti yake hapa iwe inatuambia mwaka jana tulikuwa tumelenga kufanya yafuatayo na katika eneo hili tumeweza kujenga viwanda kadhaa ama tumewahamasisha watu kadhaa kuweza kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuhusu masoko; nadhani tumeyapa tafsiri ambayo si sahihi. Tunafikiria masoko makubwa ya nje ambapo mengi hatuyajui; tuseme masoko ya kutoa samaki Ukerewe kwenda Songea hatuyazungumzii. Masoko ya kutoa korosho Mtwara kupeleka Ukerewe nao wakatafune korosho hatuyazungumzii; yale ambayo yangeweza kutupa faida kubwa sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya kuchukua mahindi kutoka Ruvuma kupeleka kwenye maeneo ambayo yana upungufu wa chakula hatuyazungumzii! Kwa hiyo, mimi ningependa tuzungumzie masoko yaliyo karibu na wananchi. Unakuta wananchi wanauza bidhaa zao chini ya mti, Wizara hii ingeanza kidogo kidogo kuwasaidia. Tukijifunza hapo ndiyo pale unapokuta kwamba, tumeweza kumudu mambo ambayo tunaweza sasa tukaingia katika ngazi za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningependa niishie hapo kwa kusema kwamba, najua Mheshimiwa Waziri ni mchakarikaji, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wataalam wake waliopo Wizarani. La muhimu Kiwanda cha Sementi; kama wameweza kutujengea Kiwanda cha Bia kweli watashindwa kutujengea Kiwanda cha Sementi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao hautoshi kumpa nafasi mchangiaji anayefuata na kwa kuwa hakuna matangazo kabla sijawataja Wabunge watano wa mwanzo watakaochangia kesho; nimepata ki-*note* kutoka kwa Mbunge mmoja kinasema, hawa Waheshimiwa Wabunge leo wanatusakama mno Wamachinga; kwa nini hawawaiti wafanyabiashara ndogo ndogo? Sasa nadhani nikimtoa wasiwasi pia huyo Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kwamba, sasa Wabunge wataanza kujizowesha kuwaita wafanyabiashara ndogo ndogo. Wanachokusudia kusema hapa ni *matching guys*, kwa

maana ya vijana wenye kurandaranda au wenye biashara za kutembeza tembeza. Sasa hili neno la kiingereza kidogo limefanana na hilo kabila la Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa tano wa kesho asubuhi; wa kwanza kabisa atakuwa Mheshimiwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, pamoja na Mheshimiwa Gaudence Kayombo.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho Siku ya Jumanne, tarehe 12 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 12 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*